ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tano – Tarehe 17 Juni, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka 2010-2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka 2010-2011.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary (Waziri Kivuli wa Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka 2010-2011. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 65

Msamaha wa Wafungwa Kwenye Sherehe ya Muungano

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika Sherehe za Maadhimisho ya siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kutimia miaka 46, Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Kikwete kwa uwezo alionao kikatiba alitoa msamaha kwa wafungwa wapatao 3,101 kwa makosa mbali mbali ya jinai.

(a) Je, Mhe. Waziri, kati ya wafungwa waliopata msamaha huo, wafungwa wangapi kutoka Zanzibar walifaidika?

(b) Ni nani anayetoa sifa na vigezo vya wale wanaofaa kupata msamaha kwa mujibu wa sheria?

(c) Baada ya msamaha huo kutokana na wahusika kupata fursa ya kuishi maisha ya kiraia, Serikali huchukua hatua gani ili kuwabadilisha tabia wafungwa hao kisaikolojia na kuwawezesha kuishi maisha mema na ya amani zaidi katika jamii?

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, utaratibu huu ni maarufu unaotumiwa na Marais wetu katika maadhimisho yote ya sherehe za kitaifa. Kwa maadhimisho ya sherehe hii ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano pia hutoa msamaha wa kuwaachia huru wafungwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapotoa msamaha wa kuwaachia huru wafungwa katika sherehe yoyote ya Kitaifa ikiwemo ya Muungano wa Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar haihusishi wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo vya Zanzibar.

Mhe. Spika, nadhani tunafahamu kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile tuna Mahakama za Zanzibar ambazo ziko kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na tuna Mahakama za Muungano wa Jamhuri ya Tanzania ambazo ziko kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo, Mahakama za Zanzibar ziko chini ya utawala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo mwenye haki ya kuweza kutoa msamaha kwa wafungwa wa Zanzibar ni Rais wa Zanzibar ndio maana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapotoa msamaha katika sherehe ya muungano hagusii wafungwa walioko katika jela za Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Naelewa kwamba Zanzibar tuna Mahakama Kuu na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna Mahakama ya Rufaa, hivyo kutokana na majibu yake haya anakusudia kuniambia kwamba hakuna Mzanzibari aliyechukuliwa hatia na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ambaye angepaswa kupata msamaha huo.

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, ingawa Mhe. Mwakilishi anasema hakunifahamu nilipokuwa nikimjibu suala lake lakini nilijaribu kumuelezea mamlaka ya Zanzibar na mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tofauti yake, ndio maana tukawa tuna serikali mbili. Nadhani ufafanuzi wangu ulikuwa ni huo kwamba kwa upande wa Mahakama za Zanzibar Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yeye ndiye mwenye mamlaka ya kuweza kutoa msamaha kwa wafungwa wa Zanzibar. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yeye ana mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa waliokuwepo katika magereza ya upande wa muungano.

Kwa hivyo, nikijibu swali lake la nyongeza ni kwamba pamoja na Tanzania kuna Mahakama ya Rufaa na wajibu mfungwa ambaye amehukumiwa kwa kupitia katika Mahakama ya Rufaa bado Rais wa Jamhuri ya Muungano anapotoa msamaha kama mfungwa huyo atakuwa yupo katika jela za Zanzibar basi atawasiliana na Rais wa Zanzibar ili katika sherehe yoyote itakayotokea ya kitaifa hapo ndipo atakapopewa msamaha. Lakini kwa mfungwa yoyote ambaye yuko katika magereza ya Zanzibar kiutaratibu Rais wa Muungano anakuwa hapaswi kuweza kutoa msamaha kwa sababu Mahakama za Zanzibar ziko chini ya Mamlaka ya Zanzibar haziko katika Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais wa sehemu zote mbili na kwa kuwa sherehe ile imegusa pande zote mbili Zanzibar na Tanganyika ndio iliyounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mamlaka hiyo aliyokuwa nayo Rais wa Muungano analolifanya pale huwa anafanya kwa jamhuri nzima ya muungano na haidhuru kama mfungwa huyu kafungwa kwa Serikali ya Zanzibar na awe amefungwa kwenye Serikali ya Muungano.

a) Je, haoni Mhe. Waziri kama Mhe. Rais akashauriwa inapofikia sherehe za muungano kama panatolewa msamaha wa wafungwa basi na Zanzibar watolewe?

b) Hivi kwa kuhakikisha suala hili limewekewa utaratibu mzuri panahaja ya kuangalia zaidi ili kuhakikisha huko mbele tunakokwenda lisitokee tena, ni kwamba kuna utaratibu gani utaandaliwa ili kumshauri Mhe. Rais?

Mhe. Waziri wa Nchi Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, Marais wote wawili wanaouwezo wa kutoa misamaha kwa watu waliomo katika maeneo yao. Rais wa Jamhuri ya Muungano anatoa msamaha kwa wafungwa walioko

katika magereza ya Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar anatoa msamaha kwa wafungwa walioko katika vyuo vya mafunzo na hili linatekelezwa zinapotokea sherehe zote.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Rais wa Muungano ni Rais wa pande zote mbili, upande wa Zanzibar na upande wa Muungano. Kwa hivyo, sherehe iliyofanyika pale na msamaha uliofanyika pale ilikuwa ni wa sherehe za muungano na muungano ni pande mbili.

Je, kutoa msamaha kwa upande mmoja Rais wa Muungano haionekani kama Rais wa Muungano anafanya kazi upande mmoja. Na nidhahiri kwamba atakubaliana na mimi waziri kama kufanya hivyo inaonekana kama Serikali ya Muungano inafanya kazi upande mmoja tu ni ya Tanganyika peke yake Zanzibar haiko.

Mhe.Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo ya ziada kwa suala hili la Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kuna mgawanyo wa madaraka maalum, yako mambo ambayo tumekubaliana yako chini ya Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na yako mambo ambayo kwa mujibu wa Katiba na Sheria tumekubaliana kwamba haya ni mambo ambayo yako chini ya mamlaka ya Zanzibar. Katika mambo hayo ni kwamba vyuo vya mafunzo viko chini ya Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, linapokuja suala la kwamba umefika wakati kwamba kuna wafungwa au wanafunzi wa vyuo vya mafunzo wanatakiwa kupewa msamaha, basi nasema kama Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora alivyosema ni kwamba hakuna ubaya wowote kama kutakuwa na haja hiyo zinapofanyika sherehe hizo za muungano. Kama ipo haja wafungwa hao walioko Zanzibar basi jambo hilo litafanywa kwa mujibu wa taratibu zilizopo zinazosimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hilo linaweza kufanyika, lakini kama tulivyosema kwamba kila upande una mamlaka kamili. Waheshimiwa Wajumbe hili kidogo linanishangaza maana sisi hapa Wajumbe wa Baraza hili tukufu mara nyingi tumekuwa tukipiga kelele hapa kwamba tusitanue wigo, mambo ambayo yako chini ya Mamlaka ya Zanzibar basi yabakie kuendelea kuwa chini ya mamlaka hiyo. Lakini mimi

linanishangaza kwamba jambo hili lile ambalo mlikuwa mkiishauri serikali ndilo ambalo linaendelea kufanywa.

Hili kidogo linanishangaza lakini narudia kusema kwamba Rais wa Zanzibar ndiye mwenye mamlaka kamili ya kutoa misamaha kwa wanafunzi walioko kwenye vyuo vya mafunzo kwa mujibu wa katiba na kwa mujibu wa sheria zilizopo Zanzibar. Na Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa upande wake yeye ana mamlaka ya kutoa misamaha pamoja na kwamba ,ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, ndio lakini katika jambo hili ambalo anatoa msamaha linasimamiwa na Serikali ya Muungano kwa masuala yanayohusu Tanzania Bara. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 20

Ufufuaji wa Zao la Karafuu

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi - Aliuliza:-

Hivi sasa miti mingi ya mikarafuu imezeeka, jambo ambalo linachangia kushuka kwa kasi kwa uzalishaji wa zao la karafuu, ukitoa idadi kubwa ya mikarafuu inayokatwa kwa matumizi mbali mbali.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa muda umefika wa kuanzisha mradi maalum wa kufufua uzalishaji wa zao hili hasa ikizingitiwa kuwa zao hili bado linachangia uchumi wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa sana.

(b) Kama hivyo ni sawa, utakubaliana na mimi kuwa ni muhimu kuwahamasisha wakulima wa zao hilo kwa njia mbali mbali ikiwemo kuanzisha mashindano maalum kwa wakulima wa zao hilo na kwa kuwazawadia wale wanaofanya vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

a) Mhe. Spika ni kweli kwamba zao la karafuu limeshuka kwa kukabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo maradhi, kuzeeka, pamoja na kukatwa kwa mikarafuuu. Aidha, Serikali imeliona suala hilo na kushuka pato la karafuuu, hivyo mradi maalum wa kufufua na kuimarisha zao la karafuu umeanzishwa tangu mwaka 2001, na umekuwa ukizalisha miche ya mikarafuu na kuitoa kwa wananchi bila ya malipo, pamoja na kutoa elimu kwa wakulima; na

b) Mhe. Spika wizara yangu imeliona shauri hilo la kushajiisha wakulima wa Mikarafuu, na kufikiria kuanzisha utaratibu wa kuwapa zawadi

kwa wale wakulima wataofanya vizuri, ili kukuza zao hilo humu visiwani mwetu na mpango huu umo katika matayarisho na kutafuta nyenzo.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Mhe. Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipatia nafsi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba tayari wameshaanza kushajihisha wakulima katika zao hili la karafuu. Mhe. Naibu Waziri anaweza kutwambia tangu kuanza kushajihisha mwaka 2001 mpaka leo ni mikarafuu mingapi ilipandwa na mikarafuu mingapi imeweza kunawiri na sasa inavunwa au inachukua miaka mingapi mpaka mikarafuu iweze kuvunwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, moja katika jamii ambayo naishukuru kwa kujishajihisha wenyewe ni hawa *Zanzibar Fitness Association* ambao ni jamii iliyojikubalisha wenyewe kupanda mikarafuu na pia imesema kwamba lile shamba la mikarafuu wapewe wao wataweza kuliendeleza. Hili ndio moja katika tatizo ambalo tulilonalo watu wanajua kupanda mikarafuu lakini katika kuiendeleza inakuwa ni jambo gumu.

Mhe. Spika, mikarafuu imegawika sehemu mbili, mikarafuu ya mibotea ambayo inatokana na mkarafuu wenyewe ule ukiupanda mara nyingi unakubali, lakini mikarafuu inayotoka *nursery* inataka uangalifu wa hali ya juu na bado wizara inalifanyia kazi suala hili. Lakini naiomba jamii wanapopanda mikarafuu ile waipande katika hali ya uangalifu wa ziada na kuifanyia kazi ya ziada ili iweze kukua. Mhe. Spika, na yale masuala mengine tutayajibu kwa maandishi kwa sababu yanataka takwimu.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nakumbuka huko nyuma kulikuwa na mradi maalum wa kufufua mikarafuu na ulikuwa ni mradi wa muda mrefu hasa kwa ile mikarafuu iliyokuwa imekufa wenyewe.

Je, Mhe. Naibu Waziri mradi ule umefikia wapi na yale maradhi yameondoka au bado mradi unaendelea?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nataka niseme kwamba yale maradhi ambayo yanakuja moja kwa moja na kupata mkarafuu na unakufa na yale maradhi mengine mkarafuu ulikuwa unakufa kidogo kidogo. Lakini mara nilivyofanya uchunguzi wangu kwa kipindi kile kwamba ulikuwa unakatwa mkarafuu halafu wanatia dawa kumbe ule mkarafuu unakufa kidogo kidogo. Kwa kweli kitengo kile sasa hivi kimeondoshwa hakipo na wafanyakazi wale sasa hivi wameajiriwa wamekuwa ni wafanyakazi wa kawaida na wengi tumewapeleka kupanda hii mikarafuu.

Lakini maradhi ya mikarafuu ni kwamba bado hayajaondoka.

Kwa hivyo, naomba kupitia Baraza hili tukufu suala la ulinzi tulifanye ni letu sasa, nawashukuru baadhi ya waheshimiwa wamekuwa wakitupatia ripoti nzuri na tunafanya kazi katika maeneo yale ya Pemba, sina haja ya kuwataja majina yao wakienda kupata tabu katika majimbo yao.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika historia ya mikarafuu tunaambiwa kulitokea kipindi kikaja kimbunga kikubwa sana Zanzibar na mikarafuu mingi sana ilianguka kwa wakati mmoja. Lakini lilipotokea hilo ilichukuliwa hatua ya dharura ya kupanda mikarafuu mingi sana kwa wakati mmoja. Haoni Mhe. Naibu Waziri kwamba umefikia wakati sasa kuchukua hatua hiyo kama ile iliyochukuliwa wakati wa kimbunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli wakati huo kiliwahi kutokezea kimbunga lakini na sasa hivi kama nilivyojibu mwanzo kimbunga kilichopo sasa hivi ni ukataji wa mikarafuu uliokithiri. Wakati ule tukizuia upepo ukaangusha mikarafuu sasa hivi imejitokeza misumeno au kuwepo kwa matumizi makubwa sana ya mikarafuu.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema zaidi ni kwamba serikali inachukua jitihada kubwa sana kwa sasa hivi kupitia Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo zinashirikiana kwa kila mwaka mmoja tunazalisha miche ya mikarafuu isiyopungua laki 300,000. Mikarafuu hiyo yote ukienda katika vituo vyetu kwa sababu tunaitoa bure yote inachukuliwa. Kazi iliyokuwepo ni jukumu letu sisi Wizara ya Kilimo na wananchi wanaochukua ile mikarafuu kuhakikisha kwamba mikarafuu ile inakuwa vizuri na kuiweka katika mazingira yanayokubalika na hatimae ituletee tija kubwa hapa Zanzibar.

Nam. 58

Ukusanyaji wa Mapato Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika miaka ya karibuni Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanzisha utaratibu wa kukusanya mapato kutokana na vianzio vya ndani kama vile maegesho ya vyombo vya moto.

(a) Je, utaratibu huo wa ukusanyaji wa mapato upo kisheria na unatambuliwa na vyombo vya kodi?

(b) Mapato yanayopatikana ni kiasi gani kwa mwezi na je yanaingia kwenye mfuko wa hazina?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 58 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, utaratibu wa ukusanyaji mapato ya maegesho ya magari katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni utaratibu wa kuwashirikisha wananchi wachangie huduma afya. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia hospitali ya Mnazi Mmoja ilishirikiana kwa karibu katika kulitekeleza suala hili na Baraza la Manispaa, kwani kabla ya kuanzishwa utaratibu huu Baraza la Manispaa lilitoa maelekezo ya kufanya kazi hiyo pamoja na kutuwekea alama za maegesho ya gari (*Parking*). Katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Utaratibu huu unakubalika Kisheria.

(b) Mapato yanayopatikana hutofautiana kwa kila mwezi na hayaingizwi kwenye mfuko wa hazina bali hutumika kugharamia mambo mbali
mbali ikiwemo kununulia vifaa vya usafi.

Makusanyo ya mapato hayo kwa wastani ni kama ifuatavyo katika kipindi cha Juali – Disemba 2009:-

KITENGO	JULAI' 09	AGOSTI' 09	SEPTEMBA' 9	OKTOBA' 09
MAEGESHO	789,650/-	1,116,600/-	1,215,800/-	3,122,000/-
MLANGONI	144,000/-	244,000/-	198,000/-	586,000/-

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Ni maeneo gani ambayo fedha hizi zimetengwa kutumika kama yapo kisheria;

b) Kama mapato hayo ni kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kwa nini baadhi ya vifaa vimeshindwa kufanya kazi kwa ukosefu wa *stabilizer* ambayo mapato ni zaidi ya milioni sita kwa mwaka; na

c) Kama yapo kisheria Kamati ya *PAC* lini imewahi kuyakagua mapato hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: (a) Mhe. Spika, katika jibu langu mama nimeelezea kwamba fedha hizi zinatumika kwa kununulia vifaa vya usafi wa mazingira ya nje pamoja na usafi wa mazingira ya ndani ya hospitali yetu.

a) Mhe. Spika, vifaa ambavyo vimekufa kwa *stabilizer* kwa kweli hili suala lilitokana na tatizo la umeme, na fedha za kufanyia shughuli ziko fedha zake maalum zinazotengwa katika maeneo husika yanayopatikana. Kwa mfano, kama *stabilizer* iliyokufa baadhi ya maeneo *labour* kule kunakuwa na fedha zake, lakini ni kwamba tunazo fedha nyengine tunazipata kwa ajili kitengo chetu hiki cha Mnazi mmoja hospital ili kuweza kushughulikia mambo hayo. Kwa hivyo, fedha hizi hatukutaka kuzitia kwenye ununuaji wa vifaa hivi, fedha hizi zinatumika kwa ajili ya usafi tu.

(c) Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* haijawahi kukagua, lakini kamati hiyo tuliwahi kuwapa matumizi yote haya yanavyotumika. Mnazi Mmoja Hospitali tuliandaa orodha nzima ya mujibu wa fedha zinazopatikana kwa kila mwezi, kwa kila mwaka, si chini ya miaka miwili tulifanya utaratibu huo na tukawakabidhi makisio hayo. Kwa hivyo, utaratibu wa kufanya uchunguzi sijui kwa utaratibu gani, lakini kama kuwakabidhi *PAC* pesa zilizopatikana na jinsi gani zimetumika shughuli hiyo ilifanyika.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kidogo niongezee ili niweze kumfahamisha vizuri sana Mhe. Hija Hassan Hija.

Ni kwamba palipotokea tatizo la umeme baadhi ya vifaa vya maabara viliharibika. Tatizo hili si la Wizara ya Afya, bali na yule aliyetuletea vifaa vile, *stabilizer* aliyoleta ilikuwa na nguvu ndogo ukilinganisha na umeme wenyewe. Na hiyo ni Kampuni ya *ICA* ndio waliohusika na mambo hayo na wamelijua tatizo hilo na wamekwishalitatua. Pia tuna mkataba wa kufanyia matengenezo vifaa vyote vilivyoharibika kwa hivyo, hakuna tatizo lolote wameshughulikia. Natumai kamati ya Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej ilipokuja kutembelea maabara hiyo ilielezwa haya na inafahamu suala hili.

Kuhusu fedha zinazopatikana, zote zinakaguliwa na *Internal Auditor* wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wanaangalia matumizi yote yanayofanyika na hakuna tatizo lolote Mhe. Spika.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kuuliza swali moja la nyongeza, Mhe. Spika, katika kupitisha bajeti kunakuwa na mafungu mawili, fungu la mapato na la matumizi. Lakini kwa utaratibu fungu la matumizi linakuwa ni vile vianzio ambavyo vimo ndani ya wizara yake na moja kati ya vianzio vinavyoonesha dalili nzuri ni huu ukusanyaji wa pesa kwa vyombo vinavyowekwa pale.

Hivyo haoni Mhe. Waziri ingekuwa vyema kwamba pesa hizo zikafika Mfuko Mkuu wa Serikali baadaye wakapewa *retention*.

Lakini pili, kwa kuwa walipokwenda Kamati ya *PAC* kwa mujibu wa maneno ya Mhe. Naibu Waziri walioneshwa orodha tu ya matumizi. Lakini kiutaratibu wa ukaguzi *PAC* inapokwenda hutakiwa ioneshwe zile risiti ambazo huorodheshwa kwenye *ledger book*. Utaratibu huo Wizara ya Afya bado hawajautumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, fedha hizi kwa utaratibu tulioupata tumeruhusika kuwa zitumike pale pale katika shughuli zetu kwenye Idara yetu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na hali ya matumizi yalivyokuwa makubwa katika hospitali yetu hii. Kwa hivyo, fedha hizi hatuzipeleki kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Jibu la pili, *PAC* hawakuoneshwa zile nyaraka, *ledger* na mambo mengine. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Waziri, taratibu zote za ukusanyaji wa fedha na matumizi pale zipo na zimeandaliwa. Kama hilo litataka lionekane kama hayo ma-*ledger* na vitu vingine, basi Kamati ya *PAC* ikija sisi tuko tayari kuwaonesha kila kitu watachokihitaji. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Mhe. Spika, katika nchi yetu mambo ya mapato na matumizi yanaongozwa na sheria ya fedha ya mwaka 2005 na kanuni yake. Suali langu. Je, makusanyo hayo yanayofanywa na mamlaka aliyopewa waziri ya kutumia, na mamlaka aliyochukua ya kutumia, ametoa katika sheria ipi, kifungu gani na kanuni ya kifungu gani cha sheria hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mjumbe kwa kuzifuatilia na kuzijua vizuri hizi sheria za mamlaka ya fedha. Nasema pamoja na taratibu hizo zilizowekwa na mamlaka ya fedha, ndio taratibu hizo hizo zilizotumika na sisi kuweza kutusaidia ili hizi fedha ziweze kutumika kwa ajili ya shughuli zetu. Fedha zina utaratibu wake, lakini katika taratibu hizo wakaona kwa kiwango hiki kidogo kinachopatikana na matumizi makubwa yanayotakiwa, zikiingizwa huku utaratibu wa kuja kuzipata tena inawezekana mambo yakazidi kuwa magumu. Kwa hivyo,

tumepatiwa fedha hizi ili tuweze kutatua matatizo yetu yaliyopo pale yanayotutokezea kila wakati.

Nam. 40
Msako wa Gari za Daladala

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Mnamo tarehe 14/04/2010 ulifanywa msako mkubwa kwa gari za daladala ambazo hazifuati sheria katika utozaji bei na mambo mengine. Katika msako huo gari 9 zilipatikana na makosa na waziri aliamuru gari hizo zifutiwe leseni. Baada ya msako huo ilitolewa taarifa katika vyombo vya habari kuwa utafika muda daladala zote zenye maringi manne zitafutiwa vibali vya kutoa huduma.

(a) Je, Mhe. Waziri baada ya kufutiwa leseni hakuna adhabu nyengine iliyotolewa kwa wahusika?

(b) Ni tatizo gani lililosababisha gari za maringi manne kufutiwa leseni?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza kutekeleza majukumu yetu kama tulivyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Abdalla Ali swali lake nambari 40 lenye vifungu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Kufuatia msako uliofanywa kwa gari ya aina za Daladala ambazo hazifuati sheria katika utozaji wa bei ya nauli na mambo mengine, adhabu kadhaa zimechukuliwa zikiwemo kufutiwa leseni na kuzuiliwa kutoa huduma kwa muda wa mwezi mmoja. Aidha, gari zilizozuiliwa wamiliki wake hutakiwa kufika Idara ya Usafiri na Leseni kwa kupatiwa maelezo zaidi juu ya kanuni za uendeshaji wa shughuli za biashara hiyo ; na

b) Gari zenye maringi manne zitafutiwa leseni za kufanya biashara ya Daladala ifikapo tarehe 31/04/2011. Hilo linatokana na sababu za kiusalama, "*Specification*", kwani muundo wa magari hayo sio kwa ajili ya kuchukulia abiria, ni kuchukulia vitu vyepesi kama vile ma-*box* na mfano wa vitu kama hivyo. Magari hayo mara yanapoingizwa nchini hubadilishwa matumizi na kutumiwa kwa

matuizi mengineyo kama kuchukulia abiria kinyume na usajili wa vyombo hivyo.

Hata hivyo, Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, msamaha huo hadi April, 2011 ni kwa zile gari ambazo tayari zinatoa huduma hivi sasa. Wizara yangu imesimamisha utoaji wa ruhusa kwa magari mapya yanayoingizwa nchini ya maringi manne. Aidha, gari hizo haziruhusiwi kuchukua abiria isipokuwa zinaruhusiwa kufanya biashara za *Tax* na kutumika kwenye maskuli kubeba wanafunzi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika ulimwengu wa sasa tuliokuwanao ukitembea katika nchi mbali mbali, au mimi nilizobahatika kutembelea, nimekwenda Nairobi, Rwanda, Zambia, Uganda, Tanga, daladala zimeundwa kisheria zisafirishe abiria kutokana na umbile lake.

Tukizingatia hasa Tanzania Bara wameaandaa mpango maalum wa kuhakikisha kwamba daladala kuondoa adha katika maeneo ya miji wameweka magari yanayoanzia kuchukua watu 28 na kuendelea. Zile ndogo ndogo zimeruhusiwa watembelee sehemu nyengine kuchukua abiria wa vichochoroni au sehemu mbali mbali za mji wetu.

Lakini kwa kuwa wananchi waliitikia wito wa serikali kuhakikisha kwamba daladala zinawasaidia wanyonge, kwa asilimia kubwa watu wanafaidika na manung'uniko yameondoka katika nchi yetu.

Je, hivyo Mhe. Waziri atalieleza nini Baraza hili na wananchi wa Zanzibar. kwa kuwa daladala zipo katika huo mwambao nilioutaja mimi hapa kwetu ziondoshwe. Swali la kwanza.

La pili, ni sababu gani za msingi hasa zinazosababisha daladala hizi kutoka Magomeni kwenda Darajani au Kiembesamaki/Darajani ziwe hazina usalama. Ni ajali ngapi ambazo zimesababisha maafa kutokana na daladala hizo hadi hivi sasa. Naomba tuelezwe Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, sheria ambayo inaturuhusu kupiga marufuku utoaji wa leseni kwa gari za daladala za maringi manne ni Sheria ya Usafiri wa Barabarani ya mwaka 2006 ambayo imepitishwa na Baraza lako hili tukufu, ambayo inampa mamlaka waziri mhusika kutunga kanuni za kuzuia suala hili.

Mhe. Spika, lengo letu sio kutoa adhabu kwa wenye gari, matajiri au wowote wale, lengo letu ni kuweka usalama wa barabarani. Kama alivyosema Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi gari hizi zile ambazo zinafanya kazi, mpaka sasa hivi zinaruhusiwa kufanya kazi mpaka mwaka 2011. Lakini zile mpya zikifika hapa tunawashauri waingize katika shughuli nyengine sio daladala, kama vile *private* hire, *Tax* na kuchukua wanafunzi skuli na taasisi zozote, katika biashara ambayo haina ushindani sana kama daladala.

Katika utafiti wetu tumeona kwamba gari hizi zinasababisha ajali sana, hata huko alikosema Mheshimiwa Dar es Salaam daladala hizi za vipanya sasa hivi haziruhusiwi kuingia mjini. Lakini sio kila linalofanyika Tanzania Bara na sisi tutalifanya, kwa sababu hizi ni nchi mbili tofauti na kila mtu ana taratibu zake za kisheria. Wenzetu wameruhusu mpaka vibajaji, sisi haturuhusu kuchukulia abiria. Kwa sababu tukiruhusu hapa mjini patakuwa na mashaka makubwa sana.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Amesema hizi daladala wameziruhusu kupakia wanafunzi. Wanafunzi nao watu tena wanene kuliko watu wazima na wazito. Je amefanya vigezo gani kwa hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwamba gari za skuli au *privare hire* na *Tax,* kwanza zinakuwa na utaratibu maalum, hazifukuzii abiria, hazina mashindano ya kwenda mbio za kasi kufika Michenzani au Darajani haraka. Kwa mfano, mtu anatoka mjini anapelekwa Chwaka kwenye skuli yake anajua kwamba naondoka saa moja mpaka saa mbili nimefika. Kwa hivyo, usalama wao ni mkubwa zaidi na siaghalabu gari za wanafunzi kupata ajali kama hizi gari za daladala.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nikauliza swali dogo tu la nyongeza. napenda nimuulize waziri kwamba, alizungumzia kuhusu gari za maringi manne, lakini leo kuna jambo ambalo limejitokeza zaidi ya hilo la magari ya maringi manne. Kuna hivi vibaskeli ambavyo vinachukua mizigo vina maringi matatu Mhe. Spika, lakini badala ya kupakia mizigo wanaweza kupakiwa hata watu 10 mle ndani ya ile gari. Ile ni sheria? Kama si sheria basi wazuilieni leseni wafanye kazi walizoambiwa wafanyie. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, vigari vile vya mizigo haviruhusiwi kuchukua abiria. Kwa hivyo, tumekusikia na tunaomba taasisi zote zinazoshughulika na usafiri wa barabarani wawazuie kuchukua abiria watu hao.

Nam. 75

Sheria ya Kudhibiti Wanyama

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika mwaka 1999 serikali chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, Idara ya Mifugo ilipitisha Sheria ya Usimamizi wa Wanyama (*Animal Resources Management Act 1999*) ili kudhibiti wanyama wanaozurura ovyo na wanaoingia nchini kwa kuwaweka katika eneo la Karantini. Kufuatia sheria hiyo, idara iliahidiwa kupewa eneo maalum lipatalo ekari 100 (*Animal Pond)* huko Tunguu. Lakini eneo hilo halikutolewa.

(a) Zipo taarifa kuwa eneo hilo la ekari 100 sehemu kubwa imepimwa viwanja kwa makaazi ya watu. Je, suala hilo ni kweli; na

(b) Iwapo ni kweli, utakubaliana nami kuwa serikali yenyewe ndio inayokwamisha utekelezaji wa sheria hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kupitia Idara ya Upimaji na Mipango Miji ilitayarisha matumizi ya ardhi ya Mji wa Tunguu wote kitaalamu. Ni kweli katika mpango huo ulitenga eneo la *"Animal Pond"* lenye ukubwa wa ekari zipatazo 100, kwa ajili ya kuwezesha usimamizi wa wanyama wanaozurura ovyo na wanaoingia nchini kwa kuwaweka katika eneo la karantini.

Mhe. Spika, napenda kukuhakikishia kuwa eneo hilo bado lipo salama na wala hakuna upimaji wowote uliofanyika ndani ya eneo hilo.

Kwa hivyo, nawaomba watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, Idara ya Mifugo kufika Idara ya Upimaji na Mipango Miji na kufuatilia taratibu za kulipima eneo hilo ili kupatiwa hatimiliki ya eneo hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu a na b. amesema kwamba eneo hilo la Tunguu ambalo ni kwa ajili ya kuhifadhia wanyama, bado liko salama. Lakini mimi nikiwa Mjumbe wa *PAC* pamoja na kamati yangu yote na Mkurugenzi wa Mifugo wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, tumekwenda kwenye field na tumethibitishiwa kwamba eneo lote limepimwa na tunaziona *beckon* kwa ajili ya majengo. Sasa Mhe. Naibu Waziri anatwambia eneo hilo liko salama.

(a) Je, suala hilo ameambiwa au amekwenda kuliona.?

(b) Kwa sababu mimi naamini kwamba Idara ya Ardhi na Upimaji ndio iliyotoa viwanja hivi. Atakubaliana nami kwamba idara yake ndio inayosababisha upotevu wa maeneo haya kama lile la Amani, Viwanda Vidogo Vidogo ambako sasa kuna majengo ya biashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, bado narudia kusema eneo la Tunguu kwa ajili ya wanyama lipo salama na Idara ya Mifugo wafike idarani kwa taratibu nyengine za kupatiwa hatimiliki.

Ningeomba suala lake (b) arudie kidogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali (b) nimesema kwamba, atakubaliana nami kwamba Idara ya Ardhi na Upimaji ndio inayosababisha kupotea kwa maeneo muhimu ya serikali kama lile la Amani Viwanda Vidogo Vidogo ambalo sasa limejengwa jengo kubwa la biashara na eneo lile lilikuwa ni la Viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, jengo hilo ambalo limejengwa pale liko nje ya eneo la Viwanda vidogo vidogo na limejengwa kufuatana na taratibu ambazo idara imekubaliana nazo.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli Kamati ya *PAC* tulikwenda huko tukifuatana na watu wa Idara ya Mifugo, na kuna bwana mmoja ambaye ndiye aliyekuwa amekabidhiwa hilo eneo, anaitwa mkulima jina tulilopewa pale, na alitupa salamu za Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Kuhakikisha kwamba yeye anamuelewa toka hapo walipokuwa kilimo.
Tumethibitishiwa kwamba eneo lile limeshachukuliwa halipo tena salama kwa ajili ya mifugo. Sasa Mhe. Naibu Waziri anatuambia Mkurugenzi na huyo bwana ambaye ndiye aliyekuwa mdhamini pale wameidanganya Kamati ya *PAC*.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, mimi simfahamu huyo bwana anayeitwa mkulima, lakini inawezekana ikawa yeye ni mtu wa kawaida. Lakini bado narudia kusema eneo hilo liko salama.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri fuatilia kazi yako hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 45

Kushindwa kwa Malengo ya Maeneo Huru

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha Maeneo Huru ya Uchumi (*EPZ*) mwaka 1986 na kutangaza sehemu tatu *Amani Industrial Park.* Fumba na Micheweni Pemba kuwa ni Maeneo Huru ya Kiuchumi kwa madhumuni ya kutoa ajira zaidi kwa wananchi, kuongeza pato la taifa, kutumia rasilimali tulizonazo na kukuza nguvu kazi iliyopo. Serikali iliahidi kupeleka miundombinu ya kisasa katika maeneo hayo ikiwemo maji safi, barabara, umeme na mawasiliano. Lakini mpaka sasa mambo hayo hayajatekelezwa.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa nini serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kupeleka miundombinu ya uhakika katika maeneo hayo?

(b) Je, kwa kuwa miundombinu bado haijafikishwa hasa Micheweni, huoni kuwa hicho ndio kikwazo kwa kilichowafanya wategauchumi wasivutiwe na kuwekeza katika maeneo hayo?

(c) Je, Mhe. Waziri unajua kuwa eneo huru la Micheweni liko hatarini kumalizika kwa kuchimbwa matofali ya jiwe kwa kuwa malengo yaliyokusudiwa hayakufikiwa?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kufanya marekebisho kwamba, Maeneo Huru ya Uchumi yalitangazwa rasmi katika mwaka 1992 kwa sheria Nam. 16 ya mwaka huo na sio mwaka 1986.

(a) Serikali kwa upande wake imefanya jitihada kwa hatua ya kwanza kuweka miundombinu ya barabara, maji, na umeme kufikia maeneo ya Micheweni. Kwa hatua ya pili, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali ambayo haitoshi kutekeleza mipango hiyo, wazo liliopo ni kukaribisha wawekezaji binafsi katika kufikisha miundombinu katika maeneo huru yenyewe kule Kiuyu Maziwa Ng'ombe kwa njia ya ubia na serikali.

Mamlaka ya ukuzaji vitega uchumi inakamilisha matayarisho ya mpango wa matumizi (*Master Plan*) ya maeneo hayo, ambao ndio utakaokuwa dira ya majukumu ya wawekezaji katika miundombinu. Mazungumzo pia yanaendelea baina ya Mamlaka/Serikali, Mamlaka ya Maeneo Huru ya Dubai (*Jabal Ali Free Economic Zone)*. Vile vile mazungumzo yanafanywa na Jimbo la Guandong nchini China, kwa mashirikiano ya Ofisi ya Balozi Mdogo wa China hapa Zanzibar, ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo.

(b) Kama ilivyoelezwa awali, pindi tukifanikiwa na jitihada za serikali zinazoendelea kufanywa, basi zitawezesha miundombinu hiyo kutika katika maeneo huru na maeneo yale kutumika kama yalivyopangiwa.

(c) Eneo la Micheweni, hususan Maziwa Ng'ombe, sawa na sehemu nyengine kadhaa za Pemba, limechimbwa matofali na wananchi ikiwa ni njia yao ya kujitafutia riziki. Jambo hilo si tu, linaharibu maeneo ya uwekezaji, bali pia linasababisha uharibifu wa mazingira ya asili ya nchi ambayo ni muhimu kwa maisha yetu na vizazi vijavyo. Mamlaka kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira, inaendelea kuwafunza wachimbaji wa matofali wa Maziwa Ng'ombe ambao nao wameahidi kufuata maelekezo ya Idara ya Mazingira kunusuru uharibifu huo.

Mhe. Spika, wachimbaji wa matofali hawakukatazwa kuchimba matofali, bali wanaelekezwa na Idara ya Mazingira kufikia kiwango fulani cha uchimbaji wa matofali na sio kufanya mashimo katika eneo lile. Ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011 - AFISI YA WAZIRI KIONGOZI

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye liidhinishe Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nifanye masahihisho yafuatayo katika hotuba yangu hii iliyomo katika kitabu ambacho tayari Waheshimiwa Wajumbe wameshapewa.

Ukurasa wa 24, mstari wa 15 naomba isomeke asilimia 48 badala ya asilimia 29.

Ukurasa wa 27, kifungu kidogo cha 35(3) mstari wa 5 isomeke Benki ya Dunia badala ya Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Ukurasa wa 30, kifungu cha 40 mstari wa 10 kwenye mahesabu pale naomba isomeke shilingi 4,665,737,216 badala ya shilingi 4,595,737,216.80.

Mhe. Spika: Labda kurahisisha baadae Mhe. Waziri Kiongozi tupatie hayo marekebisho ili tuyachapishe tuwape Waheshimiwa Wajumbe wapate kufanya marekebisho vizuri.

Mhe. Waziri Kiongozi: Ahsante. Mhe. Spika, kabla sijatoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kuhudhuria Mkutano huu wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011.

Pili, namshukuru Mhe. Dkt. Amani Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kunipa dhamana ya kusimamia Shughuli za Serikali.

Tatu, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Serikali kwa kunisaidia kusimamia shughuli mbali mbali za serikali. Mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kufuatilia utendaji wa shughuli za serikali kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kufuatilia utendaji wa shughuli za serikali. Kamati hizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mhe. Haji Omar Kheir, Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu.

(2) Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inayoongozwa na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni.

(3) Kamati ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni.

(4) Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inayoongozwa na Mhe. Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani.

(5) Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali inayoongozwa na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mwakilishi wa Jimbo la Mji mkongwe.

Mhe. Spika, hapana shaka kamati hizi zimetoa mchango mkubwa katika kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Ninauthamini sana ushauri uliotolewa na Kamati hizi. Ninawahakikishia Wajumbe wa Kamati hizo kuwa nitauzingatia na kuufuata ushauri wao ili kuimarisha utendaji wa Afisi ya Waziri Kiongozi na Serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, mkutano huu wa bajeti ni wa mwisho katika utawala wa Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume. Ninaamini kuwa wakati wa kuijadili bajeti hii Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watapata muda wa kutosha kutathmini utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA).

Mhe. Spika, nimeona nianze na utangulizi huu ili kuonesha umuhimu wa bajeti hii katika kutekeleza mipango yetu ya maendeleo. Namshukuru sana na kumpongeza Rais Karume kwa kusimamia vyema utekelezaji wa mipango ya maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapiduzi ya Mwaka 2005. Rais Karume amekuwa akinipa ushauri na maelekezo ya mara kwa mara ili niweze kusimamia vizuri majukumu ya Serikali. Nakiri kuwa maelekezo yake yamenisaidia sana katika kusimamia shughuli za Serikali kwa kipindi chote cha miaka 10.

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali yenu itakuwa na matumizi mengi ya fedha. Kama mnavyoelewa mwaka huu Wajumbe wa Baraza lako tukufu na Mawaziri watastahiki kulipwa mafao yao baada ya kumaliza muda wao wa kuwatumikia wananchi. Vile vile mwaka huu tunakabiliwa na zoezi la kuendesha kura ya maoni kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mwaka huu pia ni mwaka wa uchaguzi, Serikali italazimika kutumia fedha nyingi kugharamia uchaguzi huo. Mambo yote haya niliyoyataja yanahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo, nawaomba Watendaji Wakuu wa Serikali wasimamie kwa makini matumizi ya Serikali katika taasisi zao kama inavyoelekezwa katika sheria ya usimamizi wa fedha ili Serikali iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi zaidi. Nawaomba pia watumishi wa Serikali wafanye kazi kwa

bidii na nidhamu ili waweze kutekeleza vizuri mipango ya maendeleo. Hatua hii itawapa imani na faraja kubwa wananchi na washirika wetu wa maendeleo ili waendelee kuamini kuwa sisi ni watu makini na tuna dhamira ya dhati ya kusimamia maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2009/2010, nchi yetu inatarajiwa kufanya Uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka huu wa 2010. Narudia kutoa wito kwa vyama vya siasa, wanachama na wananchi wote wadumishe umoja na amani wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi ili nchi yetu iendelee kuwa nchi ya amani. Nawaomba sana viongozi wa vyama vya siasa vitakavyoshiriki katika uchaguzi huo vishirikiane na Tume ya Uchaguzi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2009/2010

Hali ya Uchumi wa Dunia

Mhe. Spika, mwaka uliopita hali ya uchumi wa dunia haikuwa ya kuridhisha sana kutokana na msukosuko wa fedha duniani. Takwimu za Shirika la Fedha Duniani zinaonesha kuwa uchumi wa dunia ulishuka kwa wastani wa asilimia 0.6 mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa asilimia 3.0 kwa mwaka 2008. Kwa nchi zinazoendelea uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 2.4 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2008. Kwa nchi zilizo katika jangwa la Sahara uchumi ulitarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 2.1 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2008.

Hali ya Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Spika, katika mwaka 2009 uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2008. Pato la Taifa liliongezeka na kufikia thamani ya shilingi milioni 878,400 ikilinganishwa na thamani ya shilingi milioni 748,100 mwaka 2008. Thamani hii ya pato la Taifa imelifanya pato la mwananchi wa kawaida kupanda na kufikia Dola za Kimarekani 557 (sawa na shilingi 728,361) kutoka thamani ya Dola za Kimarekani 534 (sawa na shilingi 638,819) mwaka 2008. Ukuaji wa pato la Taifa umechangiwa na vichocheo kadhaa ikiwemo kuimarika kwa shughuli za mawasiliano, kuimarika kwa shughuli za kilimo, kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji rasilimali na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar. Halikadhalika, kuimarika kwa sekta ya fedha kumesaidia sana kukuza shughuli za uchumi wa Zanzibar. Amana za mabenki zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 194 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 239 mwaka 2009.

Mhe. Spika, licha ya matatizo ya msukosuko wa fedha duniani na ukosefu wa umeme uliotokea Zanzibar mwaka jana, Serikali yenu iliweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Serikali ilikabiliana na hali hiyo kutokana na utekelezaji mzuri wa mipango ya maendeleo na usimamizi wa matumizi ya fedha za serikali. Umakini wa Serikali ya Rais Karume katika kusimamia mageuzi ya kiuchumi, taratibu za fedha na mipango ya maendeleo umewavutia sana wananchi na washirika wetu wa maendeleo kwa jumla. *(Makofi)*

Mfumko wa Bei

Mhe. Spika, kiwango cha mfumko wa bei kilishuka kutoka asilimia 20.6 mwaka 2008 hadi kufikia asilimia 8.9 kwa mwaka 2009. Hali hii imechangiwa na kupungua kwa bei za baadhi ya vyakula vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi, hali nzuri ya hewa iliyosababisha ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia katika kipindi hicho.

Sekta ya Biashara na Utalii

Mhe. Spika, katika mwaka 2009 hali ya biashara ya Zanzibar haikuwa mbaya sana licha ya matatizo makubwa ya uchumi duniani. Idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 5.0 kutoka watalii 128,440 kwa mwaka 2008 hadi kufikia watalii 134,954 mwaka 2009. Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi ulipungua kidogo kutoka thamani ya shilingi 30,189 milioni mwaka 2008 hadi shilingi 29,744 milioni. Kwa upande wa uagiziaji wa bidhaa kutoka nchi za nje, uliongezeka kutoka shilingi 93,439 milioni mwaka 2008 hadi shilingi 120,882 milioni mwaka 2009.

UIMARISHAJI MIUNDOMBINU

Mhe. Spika, Serikali yenu inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu mijini na vijijini. Hivi sasa Serikali inakamilisha ujenzi wa barabara za Mazizini - Fumba, Pwanimchangani - Mshelishelini na Mkoani - Makombeni. Mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani-Dunga, Wete-Konde na Mtambile-Kengeja-Mwambe unaendelea baada ya kusita kidogo kutokana na matatizo ya mvua. Kwa upande wa usafiri wa anga, mradi mkuu wa matengenezo ya barabara ya kurukia ndege ili kuongeza urefu wake kutoka mita 2046 hadi mita 3022 unaendelea vizuri. Kuhusu ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi huo tayari zimekamilika. Halikadhalika, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za bandari ya Malindi kwa kununua zaidi zana za kisasa kwa ajili ya kufanyia kazi. Ni matarajio ya Serikali kuwa kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu inayotarajiwa kutekelezwa mwaka huu wa fedha kutatusaidia kukuza uchumi na ustawi wa jamii.

UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA JAMII

Sekta ya Elimu

Mhe. Spika, elimu ni nyenzo muhimu sana katika kupambana na umaskini. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali katika kuinua kiwango cha elimu hapa Zanzibar. Kwanza, Serikali inaendelea kuongeza idadi ya walimu wenye kiwango cha shahada ya kwanza katika masomo ya sanaa na sayansi. Pili, Serikali inasambaza vitabu vya kusomea na vifaa vyengine vya kufundishia katika skuli za msingi na sekondari. Tatu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inafanya mipango mbali mbali kupata vifaa vya maabara kwa ajili ya mazoezi ya vitendo ili kurahisisha ufundishaji wa masomo ya sayansi. Kutokana na juhudi hizo zinazochukuliwa na Serikali, idadi ya wanafunzi wanaofaulu na kujiunga na vyuo vikuu imeongezeka. Mwaka uliopita vijana 1,373 walijiunga na vyuo vikuu ndani na nje ya Zanzíbar. Hali hii itatusaidia sana kuongeza idadi ya wataalamu hapa Zanzibar.

Sekta ya Afya

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali yenu ilichukua hatua mbali mbali katika kuimarisha huduma za afya. Hospitali ya Mnazimmoja imepatiwa mashine ya *X-rays, CT Scan, Fluoroscopy, Ultra sound* na vifaa vya tiba ya macho. Hospitali ya Chake Chake nayo imepatiwa mashine ya kuchunguza Virusi vya UKIMWI, mashine ya kuangalia mwenendo wa damu kwenye moyo na vifaa vya upasuaji. Kupatikana kwa vifaa hivi kutarahisisha uchunguzi wa maradhi mbali mbali na tiba zake hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Serikali pia inafanya juhudi kubwa za kupambana na ugonjwa wa malaria kwa kupiga dawa majumbani na kugawa vyandarua Unguja na Pemba. Hali hii imetusaidia sana kupunguza idadi ya wagonjwa wanaougua malaria. Hivi karibuni tulizindua kituo kipya cha udhibiti wa Malaria chenye maabara ya kutafiti mwenendo wa mbu na tabia zao ili kutafuta dawa bora katika kutibu malaria. Kutokana na mafanikio ya kituo hicho, watafiti kutoka nchi mbali mbali ikiwemo Chuo Kikuu cha San Fransisco Marekani na Chuo cha Karolinska cha Sweden wameomba kuja kufanya utafiti wa ugonjwa wa Malaria hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika jitihada za kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Serikali inaendelea kutoa huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa kuwapatia dawa za kurefusha maisha. Huduma hizi zinatolewa katika vituo mbali mbali Unguja na Pemba. Serikali imefungua vituo vya huduma za upimaji wa hiari wa damu kutoka 10 hadi 46 ili kuchunguza damu za wananchi wanaohitaji huduma hiyo. Jumla ya watu 56,894 walichunguzwa damu zao. Serikali pia imeanzisha huduma za kuzuwia maambukizo ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto katika vituo 19 vilivyomo katika wilaya zote 10 za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kama mnavyoelewa idadi ya vijana wanaotumia madawa ya kulevya inaongezeka kwa kasi hapa Zanzibar. Mwaka uliopita Baraza lako Tukufu liliifanyia marekebisho Sheria ya Madawa ya Kulevya na kuzuia usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya namba 16 ya mwaka 2003, ili kuondoa kasoro za sheria hiyo na kutunga Sheria ya Madawa ya Kulevya na kuzuia usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya namba 9 ya mwaka 2009. Tangu tulipoupitisha Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya mwaka jana,

Tume ya Taifa ya Madawa ya Kulevya imekutana mara mbili ili kupanga mikakati na mbinu za kudhibiti matumizi ya madawa ya kulevya. Ili kudhibiti vitendo vya uuzaji na utumiaji madawa ya kulevya, Kamati ya Taifa ya Madawa ya Kulevya imeliagiza jeshi la Polisi kufanya msako maalum kwa wauzaji na watumiaji wa madawa ya kulevya. Baada ya kuanza kwa kazi hii baadhi ya watu wameanza kulalamika kuwa wanafuatiliwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Nawaomba wananchi na raia wema wawe wastahamilivu na washirikiane na askari wa Jeshi la Polisi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

HUDUMA YA MAJI SAFI

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi inaendelea kusambaza maji safi mijini na vijijini. Ili kuimarisha huduma za maji safi, Serikali inatekeleza awamu ya pili ya mradi wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Kazi za uchimbaji wa visima vitano, ujenzi wa matangi mawili - tangi la Dole lenye uwezo wa kuhifadhia lita milioni moja na laki tatu (1,300,000) na tangi la Kinuni lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni mbili na laki saba (2,700,000) na kazi ya uwekaji wa mabomba ya urefu wa kilomita 21.5 zinaendelea vizuri. Tangi la Dole linatarajiwa kuwahudumia wananchi wa Bububu, Mfenesini, Mtoni na Dole. Tangi la Kinuni linatarajiwa kuwahudumia wananchi wa Magogoni, Fuoni, Mwanakwerekwe, Kiembesamaki na Dimani. Sambamba na juhudi hizo, Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kushirikiana na *UN HABITANT* wamekubali kuipatia Zanzibar msaada wa kutekeleza mradi wa maji safi na usafi wa mazingira katika miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani.

HUDUMA YA NISHATI YA UMEME

Mhe. Spika, tarehe 10 Disemba hadi 9 Machi, 2010 wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Unguja walifikwa na janga la kukatika kwa umeme kufuatia kuungua kwa waya wa umeme katika kituo cha kupokelea umeme huko Fumba. Kutokana na tukio hilo, Serikali ilichukua hatua za dharura kuweka majenereta katika vituo vya maji ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya maji safi katika kipindi chote cha ukosefu wa umeme. Tunawashukuru sana wananchi kwa ustahamilivu waliouonesha wakati wa tatizo hilo la umeme. Vile vile tunawashukuru wataalamu wa ndani na nje ya nchi kwa juhudi kubwa walizozifanya katika kutengeneza waya huo na kurudisha huduma za umeme.

Mhe. Spika, matatizo ya ukosefu wa umeme yalisababisha kero kubwa kwa wananchi. Katika baadhi ya maeneo wananchi wasiokuwa waaminifu waliharibu na kuiba waya za umeme. Vile vile baadhi ya wenzetu walipoteza ndugu na jamaa zao kutokana na hitilafu za majenereta. Kwa niaba ya Serikali ninachukua fursa hii kuwapa pole watu waliofikwa na msiba wa kuwapoteza jamaa na ndugu zao. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu pahala pema peponi. Amin.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na huduma za umeme wa uhakika siku zijazo, Serikali imeshaagiza majenereta 32 yenye uwezo wa kuzalisha *megawatt* 25. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 50 ya mahitaji yetu ya umeme hapa Zanzibar. Majenereta haya yamegharimu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 12.9 sawa na shilingi bilioni 17 za Tanzania. Fedha hizi zimetolewa na Serikali yenu pamoja na Washirika mbali mbali wa Maendeleo. Kuhusu mradi wa kupeleka umeme kisiwa cha Pemba kutoka Tanga unaofadhiliwa na Serikali ya Norway, napenda kuliarifu Baraza hili Tukufu kuwa mradi huu umekamilika na ulizinduliwa na Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume tarehe 03/06/2010 huko Pemba. Hatua hii itawasaidia sana wananchi wanaoishi kisiwa cha Pemba kupiga hatua kubwa za maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile Serikali yenu ilitiliana saini mkataba na kampuni ya *VISCAS* ya Japan ili kutengeneza waya wa umeme kwa ajili ya Kisiwa cha Unguja. Waya huu utachukua nafasi ya waya unaotumika sasa ambao umeshachakaa sana. Sherehe za utiaji saini zilifanyika tarehe 05/04/2010 Ikulu Zanzibar.

SEKTA YA KILIMO

Mhe. Spika, sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa katika kupunguza matatizo ya umaskini. Katika mwaka 2009/2010, sekta ya kilimo ilichangia asilimia 31 ya pato la Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya kilimo umepanda hapa Zanzibar. Uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 20,569 mwaka 2008 hadi tani 26,962 mwaka, 2009. Zao la muhogo limeongezeka kutoka tani 149,192 mwaka 2008 hadi kufikia tani 155,546 mwaka 2009. Uzalishaji wa viazi vikuu umepanda kutoka tani 3,413 mwaka 2008 hadi tani 11,372 mwaka 2009. Halikadhalika, uzalishaji wa viazi vitamu umeongezeka kutoka tani 50,267 mwaka 2008 hadi tani 53,587 mwaka 2009.

Mhe. Spika, Serikali yenu inaendelea kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ili kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Katika jitihada za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji visima saba vimechimbwa, Bumbwisudi (visima 4), Kibokwa (visima 2) na Cheju (kisima 1). Mitaro ya umwagiliaji maji yenye urefu wa mita 520 (Kibokwa mita 120 na Bumbwisudi mita 400) imejengwa kwa saruji. Halikadhalika, mitaro ya udongo ya kumwagilia maji yenye urefu wa mita 100 imejengwa katika bonde la Kibokwa. Serikali yenu ina dhamira ya kukamilisha utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Kilimo cha Umwagiliaji ifikapo mwaka 2015 ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, halikadhalika Serikali inachukua hatua za kupambana na nzi wa matunda ili iweze kuwatokomeza wadudu hawa. Dawa za kemikali zimeanza kusambazwa kwa wakulima wa matunda. Serikali pia ina mpango wa kushirikiana na wakulima wazalendo waliogundua dawa za asili za kuulia nzi wa embe ili kuwaongezea utaalamu katika kuzalisha dawa hizo. Hapana shaka ugunduzi huu utaleta mapinduzi makubwa katika uzalishaji wa matunda hapa Zanzibar.

MPANGO WA KUWAWEZESHA WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetoa kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2010 jumla ya shilingi 1,283,640,000 zimeshatolewa kwa Vikundi vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na watu binafsi, Unguja na Pemba. Unguja zimetolewa shilingi 883,770,000 na Pemba shilingi 399,870,000. Vile vile Serikali kupitia Mfuko wa Kujitegemea imetoa mikopo kwa wajasiriamali 121 (Unguja 77 na Pemba 44) yenye thamani ya shilingi 59,345,050. Nazishukuru sana taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa wananchi na wajasiriamali kwa lengo la kuwaimarisha kiuchumi.

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII *(TASAF)*

Mhe. Spika, utekelezaji wa awamu ya pili ya miradi ya *TASAF* uko katika hatua za mwisho kumalizika. Katika mwaka 2009/2010 Afisi yangu imefanya kazi ya kuratibu miradi 86 (16 Unguja na miradi 70 Pemba). *Angalia Kiambatisho Namba 1*. Miradi hiyo inahusiana na kilimo, mifugo, viwanda vidogo vidogo na uvuvi. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa muda wa utekelezaji wa mfuko huo umeongezwa hadi mwaka 2012 baada ya kupata fedha za ziada kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Uhakika wa Chakula. Jumla ya shilingi 780,000,000 zinatarajiwa kutumika katika kipindi cha miaka miwili. Fedha hizi zitagawiwa sawa sawa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, maandalizi ya programu ya uhakika wa chakula yalianza mwaka 2009. Hadi sasa jumla ya miradi 17 yenye thamani ya shilingi 470,554,110 imeibuliwa katika shehia mbali mbali. Unguja miradi 9 yenye thamani ya shilingi 252,287,255 na Pemba miradi 8 yenye thamani ya shilingi 218,266,855. *Angalia Kiambatisho Namba 2.*

HIFADHI YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, vitendo vya uharibifu wa mazingira vinaendelea kwa kasi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu Unguja na Pemba. Baadhi ya wananchi wanakata miti maarufu ya matunda ikiwemo miembe, midoriani, mishelisheli, mitofaa na minazi kwa ajili ya shughuli za kibiashara. Hali hii inaathiri sana kiwango cha uzalishaji wa matunda kwa matumizi ya binadamu. Vile vile ukataji wa miti ya asili kwa matumizi ya kuni na ujenzi nao umeshamiri sana katika maeneo mbali mbali. Inakadiriwa kuwa kiasi cha hekta 1000 za misitu zinafyekwa kila mwaka.

Mhe. Spika, Serikali inaelewa kuwa baadhi ya wananchi hasa wenye kipato cha chini wanategemea sana kuni na mkaa kwa ajili ya kuendesha maisha yao. Hata hivyo, Serikali inawataka wananchi hao wawe waangalifu katika kutunza na kuvuna rasilimali za misitu ili rasilimali hizi ziendelee kutuhudumia kwa muda mrefu ujao. Inakadiriwa kuwa Zanzibar inahitaji mkaa na kuni zinazofikia mita za ujazo milioni 1.5 kwa mwaka. Wataalamu wanatuambia kuwa misitu yetu ina uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 723,727 kwa mwaka ambazo ni wastani wa asilimia 48 ya mahitaji halisi. Kwa hiyo, kiasi kilichobaki cha mahitaji yetu ya kuni kinatoka Tanzania Bara. Kwa mnasaba huo, tunao wajibu mkubwa wa kuendelea kupanda miti zaidi ili tukidhi mahitaji yetu ya nishati na kutunza mazingira.

Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukiadhimisha siku ya mazingira Pemba tarehe 05/06/2010 vikundi vya mazingira vilituonesha shughuli mbali mbali za

utunzaji wa mazingira. Jambo hili linaonesha kuwa wananchi wameanza kuwa na mwamko mzuri katika kutunza mazingira yao. Hivi sasa jumla ya miradi 25 ya mazingira imeibuliwa yenye thamani ya shilingi 457,968,075 kwa mikoa ya Kaskazini na Kusini, Pemba. *Angalia Kiambatisho Namba 3.*

Mhe. Spika, maeneo ya ukanda wa bahari ni muhimu sana kwa shughuli za kilimo, uvuvi na utalii. Hata hivyo, uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo ukiwemo uchimbaji wa mchanga, mawe, kifusi na kokoto kandokando ya fukwe unasababisha mmong'onyoko wa ardhi na kupanda kwa kina cha maji ya bahari. Hivi sasa maji ya bahari yameanza kuingia kwenye mashamba huko Wingwi, Tumbe, Tibirinzi na maeneo mengine mbali mbali katika visiwa vya Unguja na Pemba. Naziomba taasisi zinazosimamia mazingira zijitahidi kutekeleza sheria ya mazingira ili kudhibiti uharibifu wa mazingira. Iwapo taasisi hizo zinashindwa kutekeleza wajibu wao kwa sababu sheria za mazingira zina kasoro basi zinapaswa kuzifanyia marekebisho vyenginevyo nchi yetu itaangamia. Vile vile, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali kuimarisha hifadhi ya mazingira. Kwanza, Serikali itawahimiza wananchi wapande miti kwa wingi. Pili, Serikali itaendelea kusambaza huduma za umeme katika maeneo mbali mbali ya vijijini. Tatu, Serikali itafanya utafiti kuhusu matumizi ya nishati ya jua, upepo na gesi. Nne, Serikali itahimiza matumizi ya majiko yanayotumia kuni kidogo kwa lugha rahisi ‘majiko sanifu’.

MIRADI MIKUBWA ILIYOTEKELEZWA NA SERIKALI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Serikali ilitekeleza miradi mikuu ifuatayo:-

1. Mradi wa Matengenezo makubwa ya uwanja wa michezo Amani uliofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.
2. Mradi wa Usambazaji maji safi katika Mkoa wa Mjini Magharibi uliofadhiliwa na Serikali ya Japan.
3. Matengenezo ya barabara ya kurukia na kutulia ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar uliofadhiliwa na Benki ya Dunia.
4. Mradi wa Upelekaji wa umeme Pemba kutoka Tanga uliofadhiliwa na Serikali ya Norway.
5. Ujenzi wa Jengo jipya la Baraza la Wawakilishi unaofadhiliwa na kampuni ya Al - Yousef.
6. Mpango wa kilimo cha Umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, utekelezaji wa miradi hii unatusaidia sana kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Miradi iliyotekelezwa mwaka jana na ile itakayotekelezwa mwaka 2010/2011 itatuwekea msingi madhubuti sana katika kutekeleza

malengo ya MKUZA, malengo ya milenia na dira ya maendeleo ya mwaka 2020.

UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFISI YA WAZIRI KIONGOZI

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Waziri Kiongozi.

MUUNDO WA AFISI YA WAZIRI KIONGOZI

Mhe. Spika, muundo wa Afisi ya Waziri Kiongozi unaundwa na taasisi 9 zilizogawika kwa utaratibu ufuatao:-

1. Baraza la Wawakilishi.
2. Tume ya Uchaguzi.
3. Tume ya UKIMWI.
4. Idara ya Mipango na Sera.
5. Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali.
6. Idara ya Maafa.
7. Idara ya Shughuli za Watu wenye Ulemavu.
8. Idara ya Huduma za Waziri Kiongozi.
9. Afisi Kuu ya Waziri Kiongozi, Pemba.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi ni chombo kilichoanzishwa kikatiba kwa ajili ya kukuza demokrasia ya Uwakilishi. Majukumu ya Baraza yanatajwa katika Kifungu cha 88 (1) cha Katiba kama ifuatavyo:-

1. Kutunga Sheria,
2. Kujadili shughuli za Bajeti,
3. Kuiuliza Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar, maswali.
4. Kuidhinisha Mipango na Sera za Wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, mwaka 2009/2010 Baraza la Wawakilishi liliidhinishiwa kutumia shilingi 7,941,328,000. Shilingi 7,871,328,000 zilitengwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Shilingi 70,000,000 zilitolewa kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2010 Baraza liliingiziwa jumla ya shilingi 4,665,737,216 ambazo ni sawa na wastani wa asilimia 58 ya bajeti. Shilingi 1,884,765,820 zilitumika kulipia mishahara ya wafanyakazi. Shilingi 2,710,971,396 zilitumika kwa shughuli za utawala,

vikao vya Baraza na Kamati. Halidhalika, Baraza liliingiziwa shilingi 70,000,000 kwa kazi mbali mbali za maendeleo.
Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Baraza lilitekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kutunga miswada 15 ya sheria *Angalia Kiambatisho Namba 4.*
(2) Kujadili Bajeti ya Serikali ya 2009/2010.
(3) Kuwapatia Wafanyakazi 16 wa Baraza mafunzo, *Angalia Kiambatisho Namba 5.*
(4) Kufuatilia utendaji wa shughuli za Serikali.
(5) Kusimamia ujenzi wa jengo jipya la Baraza, Mbweni.
(6) Kusimamia Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi ya Spika.
(7) Kuimarisha Kitengo cha Hansard.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Baraza la Wawakilishi linakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kutunga Sheria.
(2) Kufuatilia Utendaji wa Taasisi za Serikali.
(3) Kujadili Bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/2011.
(4) Kuwapatia wafanyakazi wa Baraza mafunzo.
(5) Kusimamia Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi ya Spika.
(6) Kuimarisha Kitengo cha *Hansard*.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinishiwa jumla ya shilingi 7,946,000,000. Shilingi 3,999,832,000 zitatengwa kwa matumizi ya kazi nyenginezo, shilingi 3,899,125,000 kwa kulipia mishahara na maposho ya wafanyakazi na shilingi 47,043,000 ni mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, vile vile naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,500,042,000 kwa shughuli za maendeleo. Shillingi 1,450,042,000 zikiwa ni mchango wa Washirika wa maendeleo kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNDP* na shillingi 50,000,000 ni mchango wa Serikali kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Baraza la Wawakilishi, Mbweni na programu ya kuimarisha Mabunge.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ili kuendeleza demokrasia. Tume ina majukumu yafuatayo:-

(1) Kuendesha Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Uchaguzi wa Madiwani.
(2) Kusimamia Ukataji wa Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi ya Zanzibar.
(3) Kuendesha na kusimamia Elimu ya Wapiga kura.
(4) Kusimamia Uandikisihaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 659,073,000. Hadi kufikia Machi, 2010 Tume iliingiziwa jumla ya shilingi 444,222,411 ambazo ni sawa wa asilimia 67 ya makadirio. Shilingi 88,815,000 zilitumika kwa shughuli za utawala Unguja na Pemba. Shilingi 354,407,411 zilitumika kulipia mishahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Tume ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(1) Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga kura kwa kuwaandikisha wapiga kura 408,267. *Angalia Kiambatisho Namba 6.*
(2) Kutoa mafunzo ya shughuli za Uchaguzi kwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi na Watendaji wake.
(3) Kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kitaifa na ya Kimataifa kuhusiana na masuala ya uchaguzi.
(4) Kuanza maandalizi ya Kura ya maoni kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.
(5) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa Wajumbe na Watendaji wa Tume ya Uchaguzi kuhusu Uendeshaji wa Uchaguzi na utatuzi wa migogoro ya uchaguzi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tume ya Uchaguzi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kufanya Kura ya Maoni kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.
(2) Kuendelea kutoa elimu ya wapiga kura kwa wananchi kupitia Vyombo vya Habari, Semina na makongamano,
(3) Kutoa mafunzo kwa Wajumbe na Watendaji wa Tume ya Uchaguzi.
(4) Kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, ili Tume ya Uchaguzi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 695,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi

219,401,000 zitatumika kwa ajili ya kazi nyenginezo, shilingi 462,498,000 kwa matumizi ya malipo ya mshahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 13,101,000 ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI ina jukumu la kusimamia mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kama ilivyo kwa nchi nyengine zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, UKIMWI bado unaendelea kuwateketeza wananchi hasa vijana. Kuna sababu mbali mbali zinazochangia kuongezeka kwa maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Sababu hizo ni kushamiri kwa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana, biashara ya ukahaba na kiwango kidogo cha mabadiliko ya tabia. Pamoja na kwamba kiwango cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwenye jamii kiko chini ya 1%, bado juhudi zinahitajika kuchukuliwa ili kukabiliana na ugonjwa huu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Tume ya UKIMWI iliidhinishiwa jumla ya shilingi 258,000,000 kwa utekelezaji wa majukumu yake ambapo kati ya hizo, shilingi 205,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 53,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010, Tume ilishaingiziwa jumla ya shilingi 128,026,348 ambazo ni wastani wa asilimia 63 ya makadirio yote. Shilingi 68,718,577 zilitumiwa kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na shilingi 59,307,771 kwa matumizi ya kazi nyenginezo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Tume ya UKIMWI ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(1) Kusimamia Uandaaji wa Mkakati wa Pili wa kupambana na UKIMWI Zanzibar,.

(2) Kutoa mafunzo kwa sekta za Serikali na baadhi ya taasisi za kiraia kuhusu masuala ya ufuatiliaji na tathmini ya UKIMWI.

(3) Kuhamasisha jamii kujikinga na UKIMWI kupitia njia mbali mbali ikiwemo vipindi vya redio, televisheni, sanaa za maigizo na magazeti.

(4) Kushirikiana na taasisi za kiraia katika kuyaelimisha makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa UKIMWI wakiwemo watumiaji wa dawa za kulevya na makahaba kujikinga na UKIMWI.

(5) Kuandaa mafunzo kwa Makamishna wapya wa Tume ya UKIMWI juu ya mbinu bora za mawasiliano katika kujikinga na UKIMWI.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Tume ya UKIMWI imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kutekeleza Mkakati wa Pili wa kupambana na UKIMWI.
(2) Kuwapatia wananchi elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.
(3) Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa shughuli za kupambana na UKIMWI.

Mhe. Spika, ili Tume ya UKIMWI iweze kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 382,000,000 kwa kazi za kawaida. Shilingi 253,215,000 zitatumika kwa matumizi ya kazi nyenginezo, shilingi 118,163,000 kwa malipo ya mishahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 10,622,000 ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, pia naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,408,000,000 kwa shughuli za maendeleo, shilingi 1,350,000,000 zikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la UNDP na shilingi 58,000,000 ni mchango wa Serikali katika programu ya udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 600,335,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, malipo ya mshahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 Idara imeingiziwa shilingi 496,233,065 sawa na asilimia 82. Shilingi 392,131,130 zilitumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 104,101,935 kulipia mishahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Vile vile Idara ilipewa shilingi 155,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Mipango na Sera imefanikiwa kutekeleza malengo kama ifuatavyo:-

(1) Kulifanyia matengenezo jengo la Afisi ya Waziri Kiongozi, Vuga kwa kuezekwa upya.
(2) Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Afisi Kuu ya Waziri Kiongozi, Pemba.
(3) Jumla ya wafanyakazi 8 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. ***Angalia Kiambatisho Namba 7.***

(4) Kuwapatia mafunzo ya uongozi wajumbe 15 wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI.

(5) Wajumbe watatu wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI walihudhuria mafunzo ya programu ya UKIMWI kupitia mafunzo ya maendeleo ya uongozi.

(6) Kuratibu vikao 2 vya Sekreterieti ya Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

(7) Kufanya vikao vitatu vya kamati ya wataalamu wa UKIMWI, Kifua Kikuu ili kutafuta mbinu za kuwapunguzia matatizo waathirika wa magonjwa ya Kifua Kikuu na UKIMWI.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Mipango na Sera inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo na sera.

(2) Kusimamia utekelezaji wa miradi katika Afisi ya Waziri Kiongozi.

(3) Kulifanyia matengenezo ya ndani jengo la Afisi ya Waziri Kiongozi, Vuga.

(4) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi tisa wa Idara.

(5) Kuwapatia wafanyakazi vifaa vya kutendea kazi.

(6) Kuimarisha kazi za sekreterieti ya Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

(7) Kuwapatia wafanyakazi wa Afisi ya Waziri Kiongozi elimu ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 549,100,000 kwa kazi za kawaida. Shilingi 167,000,000 zitatumika kwa malipo ya mshahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 370,000,000 kwa kazi nyenginezo na shilingi 12,100,000 ni mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali inaratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi na taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 456,613,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010, Idara iliingiziwa shilingi 212,371,809. Shilingi 97,148,809 zilitumika kwa kazi za kawaida na shilingi 85,223,000 zilitumika kulipia mishahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Vile vile Idara iliidhinishiwa shilingi 30,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo ambazo zimeingizwa kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imeweza kutekeleza yafuatayo:-

(1) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010.

(2) Kuwapatia vibali vya utafiti kwa watafiti 71 vinavyohusu masuala ya bahari, mazingira, kilimo, elimu, historia na afya.

(3) Kuratibu malalamiko tisa ya wananchi yanayohusu nyumba na mashamba. Kati ya hayo malalamiko saba yamepatiwa ufumbuzi na mawili yako katika vyombo vya sheria.

(4) Kuratibu kikao kimoja cha Mawaziri wa Muungano na Zanzibar kilichofanyika tarehe 03/05/2010, hapa Zanzibar.

(5) Kununua vespa tatu kwa matumizi ya Waratibu wa Wilaya za Magharibi, Kusini na Kaskazini "B".

Mhe. Spika, katika kikao cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi chini ya Uwenyekiti wa Makamo wa Rais kilichokutana tarehe 2/06/2010. Kikao hicho kilijadili mambo yafuatayo:-

(1) Wataalamu wa Wizara ya Nchi (Ofisi ya Rais) Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wameagizwa wakae pamoja ili wazipitie sheria zinazohusu ajira katika taasisi za Muungano ili kutafuta mbinu ya kutekeleza agizo la kuwapatia Wazanzibari mgao maalum wa ajira katika taasisi za Muungano.

(2) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kupewa mgao wa asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kutoka kwa wafadhili kuanzia mwaka 2009/2010.

(3) Bidhaa zinazoingizwa na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote cha forodha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zihesabiwe kuwa zimeshafika sokoni. Kwa hiyo, bidhaa zinazotoka Zanzibar na kuingia Tanzania Bara hazistahiki kutozwa kodi tena. Mamlaka ya Mapato Tanzania imeagizwa iwachukulie hatua za kinidhamu wafanyakazi wasiokuwa waadilifu katika kutoza kodi ili kudhibiti vitendo vya rushwa.

(4) Wizara za Fedha ya Muungano na Zanzibar zimetakiwa ziangalie kwa pamoja nyaraka za kuthibitisha kuwepo hisa za Zanzibar Benki kuu ya Tanzania (BOT). Taarifa ya suala hili itapelekwa kwa Makamo wa Rais, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi tarehe 24/06/2010.

(5) Waziri Kiongozi ameshamwandikia Waziri Mkuu kuhusu mapendekezo ya Zanzibar juu ya kuondolewa kwa suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika orodha ya mambo ya Muungano. Waziri Mkuu analifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015.
(2) Kuratibu vikao vya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano vinavyowakutanisha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi.
(3) Kuratibu vikao vya pamoja vya ushirikiano kati ya wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(4) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara na vitendea kazi.
(5) Kupokea malalamiko ya wananchi na kusaidia kuyapatia ufumbuzi.
(6) Kuratibu na kufuatilia shughuli mbali mbali za awamu ya pili ya mfuko wa maendeleo ya jamii yaani TASAF II.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali iweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 340,448,000. Kati ya fedha hizo shilingi 250,000,000 zitatumika kwa kazi nyenginezo. Shilingi 83,114,000 zitatumika kwa malipo ya mshahara na posho za wafanyakazi na shilingi 7,334,000 ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, vile vile naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 1,432,000,000 kwa kazi za maendeleo. Shilingi 1,332,000,000 zikiwa ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Benki ya Dunia na shilingi 100,000,000 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi kwa programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa inaendelea na jukumu la kuratibu masuala ya maafa hapa Zanzibar kama ilivyoelezwa katika Sheria Namba 2 ya mwaka 2003 ya Maafa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara iliidhinishiwa

jumla ya shilingi 294,758,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010 Idara imeiingiziwa jumla ya shilingi 88,011,426 ambazo ni asilimia 30 ya makadirio yote. Shilingi 62,266,793 zilitumika kwa matumizi ya kawaida na shilingi 25,744,633 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Kukabiliana na Maafa imeweza kutekeleza malengo kama ifuatavyo:-

(1) Jumla ya Shehia 30 (12 Pemba na 18 Unguja) zimefanyiwa utafiti mdogo wa kujua uwezo wake katika kukabiliana na Maafa.
(2) Idara imeweza kuendelea kulipia gharama za mafunzo kwa wafanyakazi wawili wanaosoma masomo ya Sheria na Usimamizi wa Rasilimali watu.
(3) Kuandaa mpango wa dharura wa kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Kukabiliana na Maafa imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kuzipatia mafunzo jumla ya Shehia 50 za Unguja na Pemba kuhusu elimu ya kukabiliana na maafa.
(2) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kukabiliana na Maafa ya Zanzibar.
(3) Kuifanyia mapitio Sheria Nambari 3 ya Maafa ya mwaka 2003.
(4) Kuipatia Idara vitendea kazi na mafunzo ya wafanyakazi.
(5) Kuanzisha kitengo cha Kuratibu hali ya dharura.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 198,586,000 kwa matumizi ya Idara ya Kukabiliana na Maafa. Shilingi 161,000,000 zitatumika kwa matumizi ya kazi nyenginezo na shilingi 34,377,000 zitatumika kulipia mshahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 3,209,000 ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, halikadhalika naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha shilingi 274,725,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa kazi za maendeleo. Fedha hizo zitatumika katika mpango wa dharura wa kukabiliana na maafa na kuendesha mafunzo ya kukabiliana na maafa katika shehia mbali mbali Unguja na Pemba.

IDARA YA SHUGHULI ZA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Idara imeidhinishiwa jumla ya shilingi 225,705,000. Hadi kufikia mwezi Machi Idara imeingiziwa shilingi 65,160,839 sawa na asilimia 30 ya makadirio. Shilingi 51,307,940 zilitumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 13,852,899 zimetumika kwa malipo ya mshahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilitekeleza yafuatayo:-

(1) Kufanya vikao 5 kwa wajumbe wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu.
(2) Kukusanya taarifa za awali za watu wenye ulemavu kupitia taasisi zao.
(3) Idara imefanya semina na wadau 25 kutoka taasisi mbalimbali na kubadilishana mawazo ili kuanzisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu kwa Watu Wenye Ulemavu.
(4) Idara ilikutana na waratibu wa Umoja wa Mataifa hapa Zanzibar kwa lengo la kujitambulisha.
(5) Kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya Watu Wenye Ulemavu kupitia vyombo vya habari vya Serikali na binafsi.
(6) Idara ilifanya semina kwa Maafisa Tawala wa Wilaya, Pemba na kuzitembelea taasisi za Watu Wenye Ulemavu Pemba.
(7) Mfanyakazi mmoja alipatiwa mafunzo ya muda mrefu ya ukatibu muhtasi ngazi ya cheti katika Chuo Cha Utawala wa Umma Zanzibar na wafanyakazi wawili wamepata mafunzo ya wiki moja kuhusu uwezeshaji wa Watu Wenye Ulemavu.
(8) Idara ya Watu Wenye Ulemavu pia imefanikiwa kutoa misaada ya kielimu kwa Watu Wenye Ulemavu. ***Angalia Kiambatisho Namba 8.***

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Idara ya Watu Wenye Ulemavu imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(1) Kuanzisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu *(Data Base Management).*
(2) Kuendelea kuhamasisha jamii juu ya haki na fursa za Watu Wenye Ulemavu.
(3) Kujenga uwezo wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu na Idara ya Watu Wenye Ulemavu.
(4) Kuanzisha mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 211,615,000 kwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Shilingi 179,000,000 zitatumika kwa matumizi ya kazi nyenginezo na shilingi 28,079,000 zitatumika kulipia mishahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 4,536,000 ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

IDARA YA HUDUMA ZA WAZIRI KIONGOZI

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 idara iliidhinisha shillingi 402,467,000/- kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2010 idara iliingiziwa shillingi 125,675,000/- sawa na asilimia 32 ya makadirio.

Mhe. Spika, Idara ya Huduma za Waziri Kiongozi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010 ilitekeleza malengo yafuatayo:-

1. Idara iliweza kuweka samani mpya katika Afisi ya Faragha ya Waziri Kiongozi pamoja na Nyumba ya Walinzi, Unguja.
2. Wafanyakazi wanne wanaendelea na masomo ya Utunzaji Nyumba, uhudumu na Upishi katika Chuo cha Utalii.
3. Mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya Shahada ya Kwanza katika fani ya uongozi katika Chuo Kikuu cha Zanzibar, Tunguu.
4. Dereva mmoja amehudhuria mafunzo ya udereva wa Viongozi wa Kitaifa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Dar es Salaam.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2010/11 idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea kuzifanyia ukarabati nyumba ya makaazi ya Waziri Kiongozi Unguja na Dar es Salaam na kuweka samani mpya katika nyumba ya Dodoma.
2. Kuwaendeleza wafanyakazi watano kimasomo.
3. Kununua vespa kwa matumizi ya Maofisa wa Idara ya Huduma.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 345,699,000/- kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa Idara ya Huduma. Shilingi 230,000,000/- zitatumika kwa kazi nyenginezo. Shillingi 108,819,000/- zitatumika kulipia mishahara na maposho ya wafanyakazi. Shilingi 6,880,000/- ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

AFISI KUU YA WAZIRI KIONGOZI – PEMBA

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Baraza la Wawakilishi liliidhinisha matumizi ya shilingi 329,036,000/- kwa ajili ya Afisi Kuu ya Waziri Kiongozi, Pemba. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010 afisi iliingiziwa jumla ya shilingi 223,920,780/- sawa na asilimia 68.0 ya makadirio.

Katika mwaka wa 2009/2010 Afisi Kuu ya Waziri Kiongozi Pemba imeweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na kufuatilia utendaji wa shughuli za serikali Pemba;
2. Kusimamia ujenzi wa afisi ya Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba;
3. Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Jamii *TASAF*;
4. Kusimamia na kuratibu shughuli za Watu wenye Ulemavu;
5. Kuratibu shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI Pemba;
6. Kusimamia shughuli za kukabiliana na Maafa. Angalia Kiambatisho Namba 9;
7. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 14 wa kada mbali mbali. Angalia Kiambatisho Namba 10 na
8. Kununua vespa 2 kwa matumizi ya maafisa wake.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Kisiwani
Pemba;
(ii) Kuendelea kutoa mafunzo na kusimamia shughuli za kukabiliana na Maafa;
(iii) Kusimamia na kuratibu shughuli za Watu wenye Ulemavu;
(iv) Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya UKIMWI;
(v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya *TASAF*;
(vi) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 9 wa kada mbali mbali na
(vii) Kununua vespa 2 kwa maofisa wake.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo hayo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 305,552,000/- kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa ajili ya Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba. Shilingi 210,000,000/- zitatumika kwa kazi nyenginezo na shilingi 87,947,000/- kwa kulipia

mishahara na maposho ya wafanyakazi. Shilingi 7,605,000/- ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA AFISI YA WAZIRI KIONGOZI, 2010/2011

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 10,974,000,000/- kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa Afisi ya Waziri Kiongozi. Shilingi 5,872,448,000/- zitatumika kwa kazi nyenginezo, shilingi 4,989,122,000/- kwa kulipia mishahara na posho za wafanyakazi. Shilingi 112,430,000/- ni michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Angalia Kiambatisho Namba 11 kwa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, halikadhalika naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 4,614,767,000/- kwa kazi za maendeleo. Shilingi 4,406,767,000/- ni mchango wa Washirika wa Maendeleo na shilingi 208,000,000/- ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendesha miradi ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Angalia Kiambatisho Namba 12.

SHUKRANI

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhim kumshukuru sana Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kunisaidia kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Pia namshukuru sana Kaimu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mipango na Sera na watendaji wake wote kwa kusimamia utekelezaji wa kazi za kila siku za Afisi ya Waziri Kiongozi *(Makofi)*.

Halikadhalika, nawashukuru wafanyakazi wa Afisi ya Waziri Kiongozi kwa juhudi wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yao. Nawaomba waendelee kufanyakazi kwa bidii ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi zaidi. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi, nawashukuru sana washirika wa maendeleo kwa namna walivyoisaidia kwa misaada ya kibajeti.

Mhe. Spika, mwisho kwa niaba ya serikali natoa shukrani zangu za dhati kwa nchi marafiki, jumuiya na taasisi za kimataifa na washirika mbali mbali kwa kutupatia misaada inayotuwezesha kupambana na umaskini. Nchi na mashirika hayo ni :-

Al-Yousef Foundation, Benki ya Maendeleo ya Afirika, Benki ya Maendeleo ya Kiislamu, *BADEA,* Benki ya Dunia, *Clinton Foundation,* China, Denmark, Finland, Jumuiya Afrika ya Mashariki, India, Japan, Libya, Marekani, Misri, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria na UKIMWI, Norway, Oman,

Sweden, Uingereza, *UNAIDS, USAID, UNDP, UNESCO, UNICEF, UNFPA, WHO,WFP, na WIPO (Makofi).*

Mhe. Spika, kabla sijafikia tamati ya hotuba yangu, ninayo heshima kubwa kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Karume kwa kunipa ushauri, maelekezo na miongozo ya mara kwa mara iliyonisaidia kutekeleza majukumu ya serikali kwa ufanisi *(Makofi)*.

Vile vile nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa juhudi unazozichukua kuliongoza Baraza lako tukufu. Umakini wako umetusaidia sana kutekeleza malengo na shabaha ya Baraza lako tukufu *(Makofi)*.

HITIMISHO

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waitafakari na waichangie hotuba hii ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Ninaamini michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana, kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi)*.

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo hii, ili kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, halkadhalika, napenda kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya awali kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii muhimu inayoratibu na kusimamia shughuli za serikali.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na watendaji wote waliochini ya Afisi ya Waziri Kiongozi *(Makofi)*.

Wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya wizara hii katika kamati, nathubutu kusema kuwa kamati yetu ilipata ushirikiano wa kutosha kukamilisha majukumu yake kutoka kwa watendaji wote wa wizara hii. Hivyo, kamati yetu

inawashukuru wote hao kwa pamoja kwa mashirikiano mazuri waliyotupa kwa muda wote *(Makofi).*

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina Wajumbe 10, ambao walihusika kikamilifu katika kuipitia bajeti hii. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omar Kheri	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Haji Mkema Haji	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Zahra Ali Hamad	-	Mjumbe
4. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Mjumbe
6. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	-	Mjumbe
7. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	-	Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
9. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe
10. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	-	Mjumbe
11. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
12. Ndg. Abdalla Ali Shauri	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa muhtasari sana kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza Idara ya Mipango na Sera kwa kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la ghorofa mbili la Afisi ya Waziri Kiongozi huko Pemba, kama walivyoahidi kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010. Sambamba na kumlipa Msimamizi wa Ujenzi kutoka Serikalini (*Consultant Engineer*) asilimia 100.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa masikitiko makubwa inaliarifu Baraza lako tukufu kuwa haikuridhishwa kabisa na umaliziaji (*finishing)* ya ujenzi huo. Hivyo, inaiomba afisi husika kumtaka mjenzi wwa jengo hilo kuendelea kufanya matengenezo ya kasoro zote zilizobainika na kamati hii, ili kuliweka jengo hilo katika hadhi inayostahiki.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kwamba wakati wa kupitia bajeti tuliarifiwa kwamba marekebisho yamefanyika. Lakini hatujayaona, basi muda muafaka utafikia kwa ajili ya kwenda kujiridhisha na hilo.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, kamati yetu inatoa pongeza maalum kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa juhudi kubwa inazozichukua za kusimamia na kuratibu vyema shughuli za Baraza. Sambamba na kusimamia vyema utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Demokrasia Tanzania unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (*UNDP*) kupitia Mradi wa Kuimarisha Demokrasia Tanzania.

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo iliyojipangia afisi hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ni kusimamia ujenzi wa jengo jipya la Baraza huko Mbweni. Ingawa mjenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi aliahidi kukabidhi jengo hilo katika mwezi wa Aprili, 2010 na kushindwa kukabidhi jengo hilo hadi leo. Kamati yetu kwa sauti moja inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuzidi kuwa na subra, ili mjenzi huyo atukabidhi jengo zuri la kisasa tena la uhakika, kwani hatua iliyobaki inahitaji umakini zaidi.

TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Mhe. Spika, tunaipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kuratibu na kusimamia vyema zoezi la kuendeleza daftari la kudumu la wapiga kura, kwa kuwaandikisha wapiga kura wenye sifa na kuwafuta wale wote waliokosa sifa za kuandikishwa. Mpango huu utamuwezesha kila mwananchi mwenye sifa kutumia haki yake ya msingi aliyopewa Kikatiba, wakati wa kupiga kura utakapofika na kuondosha baadhi ya malalamiko yanayojitokeza.

Sambamba na hayo, kamati inaipongeza tume hii kwa kuendelea vyema na matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, kwa kutekeleza mambo mbali mbali.

Mhe. Waziri Kiongozi ametueleza katika mwaka wa fedha ujao Tume ya Uchaguzi inategemea kufanya Kura ya Maoni kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, kamati yetu inaunga mkono lengo hili muhimu kwa mustakbali mzima wa kuzidi kuleta amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, tunaiomba tume hii kutekeleza suala hili kwa umakini zaidi kama Sheria Namba 6 mwaka 2010 na Sheria Namba 11 mwaka 1984 zinazoelekeza kwa lengo la kuleta umoja na mshikamano wa wananchi wetu wa Zanzibar.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Afisi ya Waziri Kiongozi kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Miradi ya *TASAF* kwa mwaka wa 2009/2010, pamoja na uaminifu wao mkubwa wanaouonesha kwa maslahi ya maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Kwa kuwa idara hii inaendelea kuratibu na kufuatilia shughuli za *TASAF II* kwa mwaka wa fedha ujao. Hivyo, kamati inaiomba serikali kuingizia fedha za kutosha kwenye kasma ya mradi huu, ikiwa ni mchango wa serikali, kwani kiwango cha fedha au mchango unaotolewa hivi sasa ukilinganisha na kile kinachotolewa na wahisani au washirika wa maendeleo.

Jambo hili litawawezesha waratibu wa mradi huu kuzidi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia wananchi elimu ya kutosha juu ya uendeshaji wa shughuli zao. Kwani imebainika kuwa baadhi ya viongozi wa miradi hii hawa taaluma ya kutosha na kupelekea kushindwa hata kujua gharama halisi walizotumia na faida wanayoipata.

Mhe. Spika, kwa kuwa miradi hii inaanzishwa kwa lengo la kuleta maendeleo ya wananchi na nchi kwa jumla.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaziomba wizara za serikali kusimamia utekelezaji wa Miradi ya *TASAF*. Jambo hili litadhihirishia wazi tunazithamini juhudi za washirika wa maendeleo. Mchango wa serikali unaoutoa kupitia fedha za walipakodi za wananchi pamoja na nguvu za wananchi wetu, ambao wameanzisha miradi husika. Vile vile itaipelekea miradi hii kuwa endelevu.

Mhe. Spika, kamati inatoa ushauri hii huu baada ya kugundua kwamba miradi ya *TASAF* na mengineyo hukosa mashirikiano ya kutosha kutoka katika wizara na sekta husika.

TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu ya Tume ya UKIMWI Zanzibar ni kuunganisha harakati za Jumuiya Zisizo za Kiserikali (*Non-Governmental Organisation, (NGO's)* zinazoshughulikia masuala ya UKIMWI Zanzibar. kwa mwaka ujao wa fedha tume hii inakusudia kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za kupambana na UKIMWI.

Kamati hii inaishauri Tume ya UKIMWI ijitahidi kutoa mafunzo ya kutosha juu ya uwekaji wa taarifa za hesabu kwa *NGO's* husika. Aidha kamati yetu

inashauri kuwa taaluma hii itolewe kwa walengwa au kwa wale wanaosomesheka na sio kwa mtu yeyote, ili kuhakikisha kuwa lengo lililokusudiwa linafikiwa, badala ya kulazimisha kutumia fedha zilizotolewa na washirika wa maendeleo hata kama malengo hayakufikiwa ipasavyo.

IDARA YA HUDUMA ZA WAZIRI KIONGOZI

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi ametueleza kwenye hotuba yake kuwa kwa mwaka wa 2010/2011 miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kutekelezwa na idara hii ni pamoja na kuendelea kuzifanyia ukarabati nyumba za makaazi ya Mhe. Waziri Kiongozi Unguja na Dar-es-Salaam.

Kamati yetu inaunga mkono malengo hayo, kwani nyumba za makaazi hutakiwa mara kwa mara zifanyiwe ukarabati, ili kulinda haiba ya jengo hilo, lakini pia zinatakiwa ziendane na yule anayestahiki ndani ya nyumba hiyo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pamoja na kuunga mkono huko kamati hii kwa sauti moja inamuomba Mhe. Waziri Kiongozi kufikia kwenye nyumba mpya iliyotengwa katika eneo la Masaki na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya maakazi ya Mhe. Waziri Kiongozi huyo wakati anapokuwa Dar-es-Salaam.

Jambo hili litazidi kuonesha kuwa tunathamini na kuzienzi juhudi za wenzetu hawa. Vile vile itapelekea nyumba hiyo kufanyiwa usafi, kwani hivi sasa mazingira yake hayaridhishi kwa kuwa hakuna wahudumu wa kufanyakazi hiyo.

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Spika, kamati inaishukuru serikali kwa kuwapatia msaada wananchi mbali mbali wanaokabiliwa na majanga yanayotambulika kisheria.

Mhe. Spika, imeamua kamati yetu kuandika haya, kwa sababu kumezuka mtindo sasa, mfano mtu akivujiwa basi inahesabiwa kama ni maafa au mtu akipata hitilafu ya umeme nyumbani kwake inahesabiwa ni maafa. Nadhani katika Baraza hili tulipitisha sheria inayofafanua yepi maafa, majanga na zipi ajali.

Mhe. Spika, kamati yetu kwa furaha kubwa inaishukuru sana serikali kwa kuutengea fedha Mfuko wa Maafa ya jumla ya shilingi 15 milioni kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kasma 29.037 iliopo ukurasa wa 131 wa Mswada wa

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011 inathibitisha kauli yangu hiyo *(Makofi).*

Kwa hivyo, tunatoa shukurani zetu hizo kwani kamati yetu ilikuwa inasononeshwa sana na kitendo cha serikali cha kutotenga fedha kwenye mfuko huu kama kifungu cha 22 cha Sheria Namba 2 ya 2003 inavyoelekeza.

Pamoja na zetu hizo kamati yetu inazidi kuiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi kutekeleza hili kwa vitendo. Kwani tutakumbuka katika mwaka wa fedha 2008/2009 Mfuko wa Maafa ulikisiwa na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutumia jumla ya shilingi 20 milioni kwa ajili ya shughuli za maafa endapo yatatokea.

Jambo la kusikitisha hadi mwaka 2009 unamalizika basi mfuko huu haukuingiziwa hata senti moja. Kitendo hicho kilipelekea idara hii kutumia fedha zake za matumizi mengineyo (*other charges*), ili kutoa msaada kwa wahanga mbali mbali na kusababisha baadhi ya malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha husika, kushindwa kutekelezeshwa kwa ufanisi zaidi.

Halikadhalika tunalishukuru Shirika la Umoja wa Kitaifa linaloshughulikia watoto (*UNICEF*) kwa kuitengea taasisi hii jumla ya shilingi 274,700,25,000/- kwa kazi za maendeleo. Fedha hizi zitatumika katika Mpango wa Dharura wa Kukabiliana na Maafa na kuendesha mafunzo ya kukabiliana na maafa katika shehia.

Mhe. Spika, tunaishauri taasisi husika kuzitumia fedha hizi kwa madhumuni yote yaliyokusudiwa. Kwa maana hiyo, tunamaanisha fedha hizi zisitumike kwa ajili ya mafunzo pekee, ili kuepusha hamkani na tafrani pale maafa yanapotokezea.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali itoe mchango wake kwenye fedha hizi za washirika wa maendeleo. Kwani tukiangalia *graph* ya kitabu cha Mhe. Waziri Kiongozi kwenye eneo lile la mchango wa serikali utakuta hapana kitu, lakini mchango wa wahisani kuna fedha hizo.

IDARA YA WATU WENYEULEMAVU

Mhe. Waziri Kiongozi ametueleza kuwa Idara ya Watu Wenyeulemavu inatarajia kuanzisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu *(Database Management)* kamati yetu inaliunga mkono hili. Endapo tutakuwa na mfumo huu, utatuwezesha kujua kupanga mipango vizuri tena ya uhakika pamoja na

kutuwezesha kufanya tathmini ya kujua mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza.

Afisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, inaipongeza Afisi Kuu Pemba kwa kusimamia vyema malengo yake iliyojipangia mwaka wa fedha 2009/2010.

Mhe. Waziri Kiongozi katika hotauba yake kwenye ukurasa wa 60 ametueleza kuwa Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba inakusudia kusimamia na kuratibu shughuli za watu wenyeulemavu, kamati yetu imefarajika na lengo hili. Hata hivyo, tunaiomba Serikali katika mwaka wa fedha ujao kuipatia Watendaji wa kutosha Taasisi hii ili iweze kumudu kutekeleza malengo yake iliyojipangia bila ya usumbufu wowote. Kwani Afisi hii ina mfanyakazi mmoja tu kwa upande wa shughuli za Watu Wenye Walemavu ambaye hatoshi katika kuleta ufanisi unaotakiwa.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kwa muhutasari kama nilivyosema, naomba sasa uniruhusu kuwasilisha maoni ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu kama ifutavyo;

Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbatu napenda kumpongeza sana na kumshukuru Mhe. Waziri Kiongozi kwa yale yote ambayo yamefanyika kwa wananchi wa Jimbo la Tumbatu kupitia Afisi yake na usimamizi wake, baada ya shukurani hizo natambua sana maelezo ambayo ameyatoa yanayohusu suala zima la kura za maoni au kura ya maoni ya kuchagua mfumo gani wa nchi yetu kuelekea mwaka 2010 baada ya uchaguzi mkuu. Nayasema haya nikiwa na haki ya kikatiba kisheria kuwasemea na kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Tumbatu sisemei jimbo jengine nasemea Jimbo la Tumbatu tu, wanayo haki ya kunihoji uhalali huu ni wananchi walionichagua wa jimbo la Tumbatu.

Nalipongeza sana Baraza lako tukufu Mkhe. Spika, kwa kupitisha azimio la kuitaka serikali kuitisha kura ya maoni na vile vile nawapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja kwa kupitisha sheria Na. 11 ya sheria za maoni, wananchi wa Zanzibar wanayo haki ya kututhamini na kutupongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya ya kutafuta mustakabali mwema wa nchi yetu.

Kama nilivyosema kwa sababu wananchi wa jimbo la Tumbatu wamenileta Barazani siwezi kusema peke yangu wala siwezi kuamua peke yangu, tunaamua kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizojiwekea sisi wenyewe. Niliunga mkono azimio nikaunga mkono sheria napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Tumbatu kumpongeza na kumshukuru

sana Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake aliyoitoa pale Maisara siku ya kumuenzi baba wa taifa hili la Zanzibar marehemu Mzee Abeid Aman Karume.

Kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Tumbatu nachukua fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru sana Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi anayefanyia kazi zake Zanzibar na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Aman Abeid Karume, kwa hotuba yake aliyoitoa pale Bwawani kwenye ukumbi wa salama *hall* wakati alipokuwa akizungumza katika kuzindua Mkoa wa Chama cha Mapinduzi wa vyuo vikuu. Aliyafanya yale au wote waliyafanya yale kutokana na maamuzi halali yaliyofanyika na Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo kila kiongozi wa Chama cha Mapinduzi nikiwemo mimi nawajibika kutetea maamuzi yale.

Utaratibu wa kuendesha chama, utaratibu wa kuendesha shughuli hupitia vikao halali viliomo katika katiba za vyama. Mkutano wa Halmashauri kuu ya Taifa uliofanyika Butiama na mingine iliyofanyika Dodoma na Dar es Salaam iliamua kwamba nchi yetu kutokana na mambo yalivyo tuelekee katika hali hiyo.

Kwa hivyo nimesimama hapa kuwawakilisha wananchi wa jimbo la Tumbatu kwa sababu ndio walionileta lakini nimesimama hapa kuwawakilisha wanachama wa CCM wa Jimbo la Tumbatu kwa kufuata maamuzi ya Chama cha Mapinduzi na wala sio vyenginevyo, ni imani yangu kwamba imani waliyonionyesha wananchi na wanachama wa Jimbo la Tumbatu wakati wa kuelimisha juu ya umuhimu wa jambo hili wataionyesha vile vile itakapofika tarehe 31 Julai, 2010 kama ilivyotangazwa na Tume ya Uchaguzi.

Narejea tena kusema nawasemea wananchi wa Jimbo la Tumbatu, nimelazimika kusema haya sitaki kumuingiza mtu nataka kujisemea mimi mwenyewe, nasema haya kwa sababu mimi ndio Mtumbatu najua kinachowaathiri Watumbatu, moja kati ya jambo ambalo linatuathiri na kuwaathiri Watumbatu basi ni mifarakano. Kwa hivyo nachukua fursa hii kukupongeza Mhe. Waziri Kiongozi kuliweka katika hotuba yako lakini kama nilivyosema nimewapongeza viongozi wawili wakubwa kwa kulisimamia kidete hili ili liweze kuleta mustakbali mwema wa nchi yetu.

Mhe. Spika, ni imani yangu wananchi wa Tumbatu walio wema hawatanikosesha kura za maoni kwa sababu eti nimeuza nchi hapana, tumekubaliana na wananchi wa Tumbatu kwamba hili jambo kwetu zuri sasa mwengine yoyote akiona jambo hili kwake sio zuri huo ni uhuru wake, huo ni uwezo wake na hizo ndizo fikra zake ambazo Mwenyezi Mungu amemjaalia.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Kamati yetu iliidhinishia Afisi ya Waziri Kiongozi jumla ya Tsh. 10,974,000,000/- kwa kazi za Kawaida na Tsh. 4,614,767,000/- kwa kazi za Maendeleo. Hivyo, kama ilivyokuwa kwenye Kamati naliomba na Baraza lako Tukufu liyakubali makisio haya na kuwaidhinishia Afisi ya Waziri Kiongozi na Taasisi zake ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, Kimsingi huu ndio mukhtasari unaohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Tunawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili nao waichangie vizuri hotuba hii kwa madhumuni ya kuiimarisha zaidi lakini hatimae wayakubali na kuyaidhinisha makisio hayo bila ya pingamizi. Baada ya kutamka hayo Mhe. Spika, natamka kuwa mimi binafsi, na kwa niaba ya Kamati yangu na Wapiga kura wa Jimbo la Tumbatu, naiunga mkono hotuba hii ya Bajeti kwa asilimia zote mia moja.

Ahsanteni kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary (Waziri Kivuli Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, niwajibu wetu sote tuliopo hapa kumshukuru Mwenyezi Mungu wetu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa wenye afya na uzima. Pia tumtakieni rehma, Mtume wetu Muhammad (S.A.W).

Naomba pia niwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa mashirikiano yetu mazuri tunayokwenda nayo. Dalili hii ya umoja wetu ni kuona kwa mwanga kijani katika tundu lililokuwa limegubikwa na kiza. *Inshaalla* Mwenyezi Mungu aijaalie taa hii iwake na kungara zaidi ili tuzidi kuwa kweupeni.

Mhe. Spika, miaka 5 sio kidogo. Katika kipindi hichi wenzetu wengi walipatwa na maafa, na wengine kutangulia mbele ya haki kama vile Mhe. Soud na Mhe. Daud ambao sasa hatunao. Viwiliwili vyao sasa vimekuwa ni sehemu ya udongo. Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema wale wote waliokwisha tangulia mbele ya haki, na pia Mwenyezi Mungu awape afueni waliopatwa na ajali na mitihani mbali mbali. Kwa wafiwa na waathirika wa mitihani hiyo, naomba kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Kambi yangu, kuwapa mkono wa pole. Ni yeye alietuumba na ni kwake tutakako rejea.

Mhe. Spika, napenda pia hapa niwashukuru sana sana wananchi wote wa Pemba kwa uvumilivu mkubwa waliouonesha kwa mtihani wa umeme. Naishukuru Serikali kwa jitihada zake, pamoja na Serikali ya Norway na ya Jamhuri ya Muungano kwa msaada wao mkubwa katika kufanikisha suala hilo.

Changa moto sasa iko kwetu kwa kuutumia umeme huo ipasavyo. Naamini tukiwa wabunifu basi maisha yetu yatakuwa mazuri zaidi kwa kuanzisha miradi midogo midogo ambayo umeme utachangia kwa sehemu kubwa. Sasa yule mfanya biashara mkubwa wa vifaa vya umeme alienadi kuwa ***'Usimuuwe mkeo – wacha umeme ufanye hivyo"***– yaani ***"don't kill your wife, let electricity do it".*** atapata nafasi nzuri huko Pemba Mfanya biashara huyu hakukusudia kumuua mkeo "fofofo" bali ni mbinu ya kibiashara ya kwamba usimtwike makazi mengi au shughuli nyingi sana kama vile kupika, kufua nguo, kupiga pasi, kufanya juice n.k. kwa kutumia mikono yake mama huyo lakini yote yanawezekana kwa kutumia umeme. Basi Mhe. Spika, tujaribuni hivyo, tusiwauwe wake zetu! Umeme upo na tuutumieni upasavyo.

Mhe. Spika, hali ya umeme kwa ujumla Unguja na Pemba hivi sasa sio mbaya. Lakini tunahitaji hatua za makusudi kuwa na umeme wa akiba kwa kutumia njia nyengine isiokuwa ya umeme kutoka Tanzania Bara. Tusikae tukajibweteza tu kwa kuona tunapata umeme huu kutoka kwa ndugu zetu. Cha ndugu si chako, na mifano ipo jinsi wanavyo tutoza gharama kubwa za malipo ya mtumiaji wa kawaida kwa karibuni mara nne na nusu kuliko zile gharama za mtumiaji wa kawaida wa Tanzania Bara.

WANANCHI WANGU WA JIMBO LA MGOGONI.

Mhe. Spika**,** ninachukua fursa hii kuwashukuru sana sana wananchi wote wa jimbo la Mgogoni lakini zaidi wanachama wangu wa CUF kwa imani yao kubwa walionipa na kunionesha. Mhe. Spika; CCM mara zote hushinda kwa kishindo, lakini kwa taarifa yako na kwa taarifa ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako, mimi nimewashinda CCM maana nimeshinda kwa ***TSUNAMI***, maana mshindi wa pili wa mchakato wetu alipata kura ***305*** na watatu ***291*** tu ukilinganisha na mimi nilietokea wa kwanza kwa kupata kura ***2105.***

Niheshima kubwa sana walionipa na imani kubwa kabisa walionionyesha wanachama wangu, na ninawashukuru sana sana. Nina waahidi kuzidi kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na ya Zanzibar yetu kwa ujumla.Wale watani wangu waliovumisha eti kuwa nimeshindwa kwa kura mbili tu sasa wameona ukweli wa mambo na ukweli wa mwakilishi anaewahudumikia watu wake katika jimbo.

Ingawa bado mchakato wetu haujamalizika, kwani ni Baraza Kuu la Uongozi ndio lenye kauli ya mwisho katika uteuzi. Lakini ninaimani kuwa mapendekezo ya wananchi na wanachama wa Jimbo la Mgogoni yatatizamwa na Baraza Kuu kwa jicho la Rehema ili Baraza hilo liweze kuamua kulingana na kauli ya wanachama wa Mgogoni walivyopendekeza.

MAKUBALIANO NA MARIDHIANO YETU.

Mhe. Spika, sote tunaelewa historia muhimu ya maridhiano iliowekwa na Rais wetu wa Zanzibar, Mhe. Amani A. Karume pamoja na Katibu Mkuu wa CUF maalim Seif Sharif Hamad siku ya tarehe 5 Novemba 2009. Naomba niwashukuru kwa dhati viongozi hawa wawili na kuwaombea kila la kheri katika maisha yao.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo nilipongeze Baraza lako Tukufu vile vile kwa kuyapa nguvu maridhiano hayo kwa lengo la kustawisha umoja na mashirikiano miongoni mwa Wazanzibari na kujenga misingi imara ya amani na utulivu wa kudumu hapa Zanzibar na kupendekeza kuwe na mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha Vyama vya kisiasa vyenye wajumbe katika Baraza la Wawakilishi. Utaratibu huu utahitaji uridhiwe na wananchi kwa kupiga kura ya maoni.

Kwa maana hiyo, mimi binafsi nachukua fursa hii kwa niaba ya Chama changu, na kwa niaba yangu binafsi kuwaomba wanachama wote wa Chama changu CUF wakubali kuunga mkono pendekezo hili lililotolewa na Wawakilishi wao ndani ya Baraza. Vile vile nawaomba wanachama wa vyama vyengine wote tuungane pamoja katika suala hili muhimu kwa maslahi ya nchi yetu na vizazi vyetu. Mimi ninaamini katika kura hii ya maoni basi angalau asilimia tisiini ya wazanzibari, kwa nia ya kuitakia mema nchi yetu, watasema na kuipigia kura ya ***ndio*** kwamba iwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, nilidhani kwamba katika hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi angalau angaliwatanabahisha wazanzibari umuhimu wa kuwa wamoja na kuwataka wazanzibari wote wanaopenda amani na utulivu katika nchi kukubaliana na jambo hili la heri na hivyo kuwanasihi kulikubali, kama walivyofanya Rais Kikwete na Rais Amani na Rais Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi katika nyakati mbali mbali.

Lakini pengine kwa kutumia maneno aliyoyasema Prof. Denge "computer"imeyaruka baadhi ya maneno ya mhe. Waziri Kiongozi. Hata hivyo nichukue tena nafasi hii ya kuwaomba wananchi na Wazanzibari wote kwamba waone suala hili kama ni suala la kuiokoa Zanzibar yetu katika matatizo ya kila siku na ambayo hayana maana. Na hivyo maamuzi yao ya ndio kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ndio yatakayoiondoa Zanzibar katika misukosuko ya kila siku na hivyo kuijenga Zanzibar yetu kiuchumi, kimaendeleo, kisiasa, kijamii, kielimu na kadhalika. *Inshaalla* Mwenyezi Mungu atujaalie kuyatekeleza na kuyakamilisha hayo kwa salama na amani. Amin.

Mhe. Spika, wapo wachache wasioitakia mema nchi hii, wanaotaka kila uchao tuwe na mtafaruk na kugombana, ambao wanataka kupinga suala hili. *Inshaalla* Mungu awatie ilhamu ya kupenda nchi yao na kukubali mapendekezo ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na bilisi huyo mbaya basi awaondokee. Amin.

HALI YA KIUCHUMI

Mhe. Spika, hali ya ukuaji wa uchumi duniani umeathirika sana kutokana na mtikisiko wa fedha ulioikumba dunia hivi karibuni. Kwa maana hii bado tunahisi kuwa watu wetu bado wako katika dhiki na maisha ambayo bado hayajaridhisha.

"Mkuza" bado inahitaji kufanya kazi sana ili lengo lililokusudiwa lipatikane na kufikiwa. Mhe. Spika, ingawa pato la mtu limeongezeka na kufikia $ 557 kutoka $ 260 katika mwaka wa 2000, lakini mfumko wa bei na ulizidi kuwaumiza wananchi wetu. Vyakula navyo vimepanda kwa kiwango fulani ambapo nayo inafanya sehemu moja ya kuwazidishia mzigo watu wetu.

Mhe. Spika, sasa tufanyeje? Ili kuwaondoa watu wetu katika tatizo hili basi ni lazima tutilie mkazo katika sekta za kilimo na uvuvi ambazo katika Bajeti ya Serikali, sekta ya kilimo na uvuvi haikutiliwa mkazo sana hata kidogo. Wananchi wetu lazima wasaidiwe kupata nyenzo zitazowasaidia katika kujiendeleza kwa kilimo, ufugaji, uvuvi na kuimarisha mazao ya biashara kama vile karafuu na mwani.

Mhe. Spika**,** tumeambiwa kuwa kuna wazalendo waliogunduwa dawa za asili za kuchanganya unga wa kungumanga na wa karafuu kwa kuulia wadudu waliomo ndani ya embe na matunda mengine. Mhe Spika lazima uvumbuzi huu ufanyiwe utafiti wa kutosha na wataalam wetu wa kilimo. Sifa ya kungumanga kila mtu anaijuwa kuwa ni kulegeza na kulewesha wakati karafuu inakazanisha. Isijeikawa kwa kutumia mchanganyo huu, wadudu wanalewa kidogo halafu wanapata nguvu nyingi za kuzaliana na baadae tukaja kujuta kama ilivyokuwa kwa maradhi ya ***die back*** na ***sudden death*** ya mikarafuu. Hatimae mikarafuu mingi tuliikosa.

Mhe. Spika, sijui zao la karafuu limefanya kosa gani katika Serikali hii. Zao hili ndio zao kuu la biashara na ndio zao linalochangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya visiwa hivi. Ikiwa leo zao hili pamoja na wananchi wanaozalisha kilimo hichi hawakufikiriwa hata kidogo, basi hili ni tatizo kubwa sana. Au ndio tuseme ile dhamira ya Serikali tulioahidiwa miaka mitatu nyuma kwamba zao hili litaanza kubinafsishwa kidogo kidogo ndio sasa hatua hio imeshakamilika ?

IDARA YA URATIB

Mhe. Spika, katika eneo hili, mwaka jana tuliambiwa ahadi nyingi hasa katika ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (ukurasa wa 42 – 43 katika hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi ya mwaka jana). Jee ukiacha mradi wa kiwanja cha ndege ambao umeshaanza ile miradi mingine 4 kama vile ujenzi wa bandari ya Maruhubi, utafiti wa mimea, eneo huru la Afrika ya Mashariki kuwa Zanzibar na mradi wa kuunganisha Zanzibar na bandari nyengine za Afrika Mashariki, kituo cha umwagiliaji na kadhalika zimeishia wapi? Mbona hatuisikii hata kutajwa? Idara hii Mhe. Spika ni lazima ituelezee pahala tulipo kwani wao ndio masuli katika eneo hilo.

Mhe. Spika, bado wazanzibari hatujapata nafasi ya kuelezea au kutetea mambo yetu katika Jumuiya hii. Mkataba ya Jumuiya umetuweka pabaya sana sana sisi Wazanzibari. Mhe. Spika, mambo kama Nishati (kif. 101) cha Mkataba wa Jumuiya, Elimu (102)ya Mkataba huo, Sayansi na Technologia (103), Kilimo na usalama wa chakula (105) mifugo na maradhi ya mifugo (107 – 108), Utalii na wanyamapori (115 – 116), Afya (118) Utamaduni na Michezo (119 -120) na mengi mengineyo sio mambo ya Muungano.

Hivyo basi Serikali ya Jamhuri ya Muungano haina uwezo wowote ule kikatiba wa kututetea haki zetu hizi. Ni wazanzibari wenyewe, kupitia kwa Serikali yao ndio wanao uwezo kisheria kuitetea Zanzibar kwa masuala nilioyaeleza hapo juu ambayo sio ya Muungano. Sasa Jamhuri ya Muungano inapofanya hivyo si inatupora haki zetu kwa mlango wa nyuma? Mhe. Spika, ni lazima Afisi hii ituelezee namna gani wanavyofanya katika kulinda haki zetu hizi.

Haki ya kwenda na kufanya kazi nayo kama hatukuijuilia na kuiangalia kwa makini basi pia nayo itatuweka pabaya sana. Hivyo, tujitahidi ili visiwa vyetu visije vikakumbwa na wageni wengi wanaofanya kazi kwa sababu tu kuna uhuru wa wana Jumuiya kufanya kazi popote. Mhe. Spika, ni lazima tujue nini tukitakacho na uhuru huo mwisho utafikia wapi, vyenginevyo hadithi ya ngamia na mchungaji wake itatuvaa sisi Wazanzibari. Na afisi hii ya Waziri Kiongozi itawekwa Msalabani kwa hayo.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika**,** hichi ni chombo chetu. Tusingependa kukitia midomoni sana, lakini kuna mambo matatu ambayo yanaumuhimu wake kuyataja.

Mhe. Spika, ili Baraza kuwa huru kabisa *(complete independence)* ni lazima liwe linatengewa fedha zake kutoka mfuko mkuu wa Serikali moja kwa moja

na fedha hizo ziwe chini ya uangalizi wa Katibu wa Baraza. Baraza haliwezi kuwa omba omba kwa kugonga hodi mara kwa mara katika Afisi za Wizara ya Fedha. Mfuko huu *"The House of Representatives Fund*" ndio utaolifanya Baraza liende vizuri na kazi zake.

Mhe. Spika, takriban mabunge yote ulimwenguni yanafuata mfumo huu. Hata wenzetu Bunge la Jamhuri wanaendeleza mfumo huu. Bunge Mhe. Spika wamepiga hatua zaidi kwa kupewa ruhusa kisheria kutafuta fedha au misaada yao toka nje na pale wanapoipata fedha hizo hazipitii Hazina, bali zinakwenda moja kwa moja katika mfuko wa Bunge. Pale matumizi yanapobakia kwa mwaka ule, basi fedha itazungurushwa upya kwa mwaka wa fedha unaofuatia. Bunge hivi sasa pia lina mradi wa kumjengea kila mbunge afisi yake katika Jimbo lake ili wananchi waweze kumuona kwa urahisi.

Mhe. Spika**,** nilazima tuuone umuhimu huu na tuiombe Serikali ili iweze kulikubali suala hili. Hapo tu ndio tutalifanya Baraza letu kuanza kuota meno.

Mhe. Spika, suala la pili ni suala la pesa kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo. Fedha hii ni muhimu sana sana kwa maendeleo ya majimbo yetu. Mhe. Spika tunaomba sana suala hili lizingatiwe haraka sana, hasa kwa sababu Bunge la Jamhuri ya Muungano limeshaanzisha mfuko huu. Hivyo tutapokua na CDF ya Bunge na ya Baraza kwa jimbo moja, ninaamini kuwa maendeleo ya majimbo yetu yatapatikana kwa wepesi zaidi .

Mhe. Spika, la mwisho katika eneo hili ni kutaka Baraza hili lianzishe utaratibu wa masuala kwa Waziri Kiongozi. Utaratibu huu si mgeni kwa nchi nyingi za Jumuiya ya Madola. Ni utaratibu unaotumiwa kuichangamsha Serikali papo kwa papo ukilinganisha na yale masuala ya kuandikwa ambayo Waziri muhusika hupata nafasi ya kujiandaa. Utaratibu huu ni mzuri sana kwa sababu unamfanya Waziri Kiongozi kufuatilia Mawaziri wake na Wizara zake ili aweze kuwa muelewa mzuri *(well conversant)* wa utendaji wa Serikali yake. Naamini ushauri huu utachukuliwa na Serikali ili Baraza linalokuja, Inshaalla, kuwe na masuala kwa Waziri Kiongozi.

IDARA YA MAAFA

Mhe. Spika, bado Idara hii haijapatiwa vitendea kazi na mambo mengine yanayohusika katika kuwasaidia watu wetu wanapopatwa na maafa. Mhe. Spika, sina uhakika kama zile ahadi zilizotolewa mwaka jana, kama vile kuwa na sera ya uhakika ya kukabiliana na maafa, pamoja na kurekebisha sharia husika, elimu kwa wananchi pamoja na umuhimu wa kutoa misaada kutokana na maafa hayo kwa wakati muafaka kama zimetekelezwa.

Mhe. Spika**,** hii inanikumbusha kamati hii ya Maafa ilipojipinda kidogo na kutoa msaada kwa watu wa Daraja Bovu walipopatwa na maafa miezi mitatu baada ya maafa wenyewe kutokea. Sijui kama huu ni utendaji mzuri ambao unalenga kweli kumsaidia aliepatwa na maafa.

TUME YA UCHAGUZI

Mhe. Spika, Haki ya kupiga kura kwa Wazanzibari imeelezewa vizuri katika kif. Cha 7(1) na (2) cha Katiba ya Zanzibar. Mzanzibari huyo aliyefikia miaka 18 hatakiwi awe na uraia wa nchi nyengine au mgonjwa wa akili , asiwe amefungwa zaidi ya miezi sita (6) au kukosa kuthibitisha au kukosa kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura pale kinapohitajika.

Mhe. Spika, jukumu hili sasa ni la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kuhakikisha, kama alivyosema Rais wa Zanzibar, Mhe. Amani A. Karume kuwa ***"kila Mzanzibari mwenye haki ya kuandikishwa kupiga kura ataandikishwa"*** Kwa kutumia hekima hii ya Katiba inaonesha wazi kwa mfano, kuwa mzee wa miaka 80 mwenye mvi tele kichwa hatosumbuliwa katika kumdadisi cheti chake cha kuzaliwa madhali inaonesha dhahiri umri mkubwa alionao kuwa ni zaidi ya miaka 18; na kadhalika. Hata sheria ya uchaguzi na ile ya vitambulisho haitoi masharti kama hayo, na hivyo basi kuifanya kazi hivi kuwa nyepesi zaidi.

Mhe. Spika, Tume za Uchaguzi ulimwenguni ndio zinazoweza kuleta vurugu au amani ndani ya nchi husika. Tumeona mifano mingi tu (Kenya na Zimbabwe kwa upande mmoja wa vurugu uliosababishwa na Tume ya Uchaguzi, na Uingereza na Msumbiji kwa upande wa Pili ambapo Tume zao zilikuwa za kiungwana na kuepusha aina yeyote ya vurugu). Ni imani yangu kuwa Tume yetu itayazingatia haya ili tukamilishe ngwe yetu ya uchaguzi Mkuu wa 2010 kwa salama na amani sote, mshindi na alieshindwa wakiwa wamefurahi kwa jinsi ya uchaguzi ulivyokuwa wa uwazi huru na wa haki.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi pia safari hii imeongezewa majukumu ya kufanya kura ya maoni. Nayo hii ni kazi kubwa na nzito ambayo ndiyo itayotowa mwelekeo wa nchi yetu na usalama wake. Tunawaomba wananchi wote waone umuhimu wa kura hii kwa maslahi ya Zanzibar na vizazi vyake kwa kuitikia mwito wa *ndio;* tunaomba Tume pia itekeleze wajibu wake vizuri sana kwa kulenga huko huko kwenye umoja. *Inshalla* Mwenyezi Mungu atuwafikishe.

UKIMWI

Bado maambukizo haya yanatusumbua na bado hatujapata dawa. Dawa mjarab basi ni kujizuia na mambo haya. Mhe. Spika, ninachoomba mimi ni kuwa ni vyema tuelezewe idadi ya maambukizi haya kwa kila wilaya ili tuweze kuchunguza sababu za kuwa na maradhi hayo kwa kiasi hicho kwa eneo hilo.Vile vile ni vizuri kujuilishwa namna gani vijana wetu, hasa wale walaji wa unga walivyoandaliwa angalau kudhibitiwa japo kwa kiwango kidogo katika masuala haya ya unga na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, hili linaweza kutusaidia sana katika suala zima la "*control*" ya ugonjwa huu.

ULEMAVU

Mhe. Spika, mwaka jana tulitaarifiwa kuwa watu wenye ulemavu watasajiliwa. Tunapenda sasa tuelezwe ni wangapi watu wa aina hio ambao wameshasajiliwa, na vipi wamejipanga, kuwasaidia watu hao katika maeneo yao yanayohusika..

Mhe. Spika, jee wananchi wameshaelimishwa kuhusu haki za jamii ya watu wenye ulemavu. Jee pia wameshapatiwa mafunzo? Haya yote yaliahidiwa kipindi kilichopita, lakini kwa masikitiko makubwa hakuna kilichoendelezwa. Wenzetu hawa wanahitaji misaada kutoka kwetu, tujitahidini.

TASAF

Mhe Spika, ni wajibu wetu kuupongeza mfuko wa Tasaf kwa kusaidia sana miradi ya wananchi wetu. Hii ni habari nzuri kwamba mfuko huu umeongezewa muda wa miaka miwili tena. Wito wangu ni kwa wale wadhamini wa maeneo kujitahidi sana kuondoa ubinafsi katika suala la kuamua aina ya mradi unaohitajika katika eneo husika, Maamuzi ya wengi ni lazima yaheshimike, na hapo ndio tutautumia vilivyo mfuko huu.

MWISHO

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru tena waheshimiwa wajumbe kwa kunisikiliza na pia kwa kuniunga mkono katika hoja yangu nilioitowa kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Naamini umoja wetu huu tunaouendeleza utatufikisha pahala pazuri katika kuendeleza nchi yetu. Tusikate tamaa, kama alivyosema mwandishi maarufu wa kizanzibari Said Ahmed Mohammed, "*umeanguka, nyanyuka, simama anza tena kwenda, mradi tu usikate tammaa, na utafika*" Tutetee nchi yetu kabla ya kuweka utashi wa vyama vyetu. Vyama ni baada ya nchi na hapo ndipo tutapofanikiwa. Ninawatakia kila la kheri katika uchaguzi huu unaotukabili pamoja na michakato yake yote. Mungu ibariki Zanzibar na Wazanzibari wake. Amin.

Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusema machache na ninaunga mkono hoja hii, huku nikiamini kuwa yale niliokuwa na wasiwasi nayo basi shaka hizo zitatolewa na Mhe. Waziri Kiongozi. Ahsante sana.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe Fatma Abulhabib Fereji: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuwa leo niwe msemaji wako wa kwanza katika kujadili hotuba hii ya Bajeti ya Afisi ya Waziri Kiongozi. Napenda nianze kumshukuru Mwenyezimungu ambaye ametujaalia kuwa wazima wa afya kuweza kuendelea na shughuli zetu, ambazo zinahusu maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Kiongozi kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake mwenyewe ambayo amesema ni kwa muhtasari lakini imefahamika kuhusiana na malengo na kile ambacho kinategemewa kufanywa na yale yaliyofanywa kwa mwaka uliopita.

Nafahamu kwamba tunabanwa na muda katika kipindi hiki kwa hivyo naomba nianze katika yale maeneo ambayo nimeyachagua kwa leo hii kuweza kuyazungumzia mawili matatu ili na wenzangu nao waweze kuchangia.

Mhe. Spika, mimi naomba nianze kwa kuzungumzia juu ya mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi katika ukurasa wa 21 wa kitabu cha Mhe. Waziri Kiongozi, nipongeze jitihada hizi za SMT na SMZ kutokana na shilingi bilioni 1.2 ambazo zilitolewa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Tukiwa na lengo la kuwaondosha wananchi wetu katika hali ya umasikini ambao umekithiri. Lakini kidogo nina matatizo na ile *figure* ambayo imetolewa. Tulivyoelezewa mwanzo ni bilioni 1.2 lakini baadaye huku inaonekana kuna *figure* zimezidi sasa sijui kama kule kwanza tulikuwa tunafanya tu *approximant* ya 1.2 *billons* lakini idadi halisi ndio ile, hapa nitaomba maelezo au zile za ziada, kuna mtu mwengine ambaye ametuongeza ambaye hajatajwa pale.

Napenda kueleza kwamba kinachokosekana katika kumanage matumizi ya fedha hizi ambacho kimejionesha hapa ni uwiyano wa jinsi ambavyo zimegaiwa kati ya visiwa hivi viwili tabaan Unguja na Pemba. Wasi wasi kwamba uwiyano pia haupo ki Mkoa na ki Wilaya, baya zaidi ni pale panapokuwa hapana uwiyano wa kijinsia. Tunafahamu kwamba katika jamii yetu idadi kubwa ya watu ni wanawake na wanawake ndio masikini sana kiuchumi kuliko wanaume. Lakini kuna *figure* ambayo tumewahi kuiyona kwamba baina ya Julai na Marchi mwaka huu wanawake ambao walipata mikopo ni 224 ikilinganishwa na wanaume 331.

Pia ningependa nielezwe wapo idadi ndogo ya wanawake kuliko wanaume, lakini wasiwasi wangu naambiwa unakaribiana na kweli ni kwamba kiwango cha mikopo hii wanachopewa wanawake ni kidogo mno kuliko kiwango wanachopewa wanaume. Ningeomba Mhe. Waziri hapa anielezee kinaga ubaga kwa nini kwanza tukawa hatukuona umuhimu mikopo hii kuwapatia zaidi wanawake kuliko wanaume. La pili kwa nini tusiwe tumefanya utaratibu kwamba wanawake ndio wakapata fedha nyingi kuliko hawa wanaume ambao tayari kiuchumi wao wapo mbele.

Mhe. Spika, katika meelezo yake Mhe. Waziri alisema na mimi nasema vile vile tunazishukuru taasisi za fedha ambazo zinatoa mikopo kwa wananchi na wajasiri amali, nia ikiwa ni nzuri ya kuwanyanyua kiuchumi. Naomba nitoe indhari kwamba binafsi nimeshuhudia kuna taasisi za fedha ambazo baada ya kuwainua wananchi wetu kiuchumi zinawamaskinisha zaidi. Mfano moja ya hiyo nafikiri inaitwa Blue Bank nilipata mfano pale nikasema kweli basi kama ni taasisi ya fedha hii na BOT ipo na serikali ipo kitu kama hichi kinaendelea kiachiwe kiwatie umasikini zaidi wanachi wetu. Mtu alikopa shilingi milioni moja na thamanini elfu lakini utaratibu wake wa kulipa akaambiwa atalipa miaka mitatu na kila mwaka atalipa laki moja na elfu tisa kwa miezi thathini na sita yaani miaka mitatu.

Mhe. Spika, hii hesabu ni ya kijendawazimu ni ya kumaskinisha wananchi wetu. Mimi ushauri wangu hili ni moja lakini pia niliwahi kukutana na vikundi vya wanawake katika vichochoro vyetu wakanambia kuna taasisi fulani ya wahindi inakopesha, nikazisikiliza zile hesabu zenyewe, kwa kweli wanaibiwa, badala ya kuwanyanyua wanawamaskinisha zaidi. Naiyomba serikali ifanye utafiti katika mambo haya na taasisi zote za kifedha iwe zinatoa mkopo na zisiruhusiwe kuwamaskinisha wananchi wetu. Ikiwa zimekuja hapa ziwe kwa nia ya kuwakomboa wananchi wetu kiuchumi lakini sio kuwazidishia umasikini ambao tayari upo.

Mimi naomba nitoe pongezi vile vile kwa mifuko ya TASAF kwa kweli imeonekana kusaidia na ni mkombozi kweli katika hali yetu hii ya kimaskini. Pongezi zaidi kwa wale ambao wanatusaidia fedha ambazo wameziweka pale milioni 780 kwamba zitagaiwa kwa uwiyano mzuri kati ya visiwa viwili na bila shaka pia zitagaiwa katika hivyo visiwa viwili katika mikoa na kiwilaya kwa uwiyano mzuri kama ambavyo wenyewe wametarajia.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la MTAMBUKA la mazingira. Mhe. Spika, niishukuru serikali kwamba hivi sasa uwezekano wa mwananchi kufikiwa na umeme umefikiwa katika visiwa vyetu vizuri sana. Tuwashukuru Serikali ya Norway kwa kule Pemba pamoja na serikali. Kwa hapa Zanzibar pia tuishukuru serikali kwa yale ambayo yametendeka katika tatizo lile lililotokea na pia

kwamba majenereta ambayo yataweza kutusaidia wakati tunajiandaa kutafuta umeme mbadala ambao utakuwa wa uhakika.

Tatizo tulilonalo si access ya wananchi wetu kwa umeme, umeme upo na haya nitarudia kusema kwa sababu siku moja niliwahi kuyasema hapa sijui kwama mwaka juzi kwamba mpaka chini ya migomba umeme upo. Nina hakika Pemba sasa hivi mwananchi yoyote anayetaka kutiliwa umeme umeme upo, lakini tatizo ni bei ya kuunganisha umeme wenyewe. Lakini pili bei ya umeme wenyewe.

Mhe. Spika, inasikitisha angalau kwa hapa Zanzibar ambao umeme ulikuwepo, kwa mazingira ya mjini wachilia mbali shamba bado kuna asilimia 43 ya wananchi hawajaunganishwa na umeme. Bila shaka sio kwamba umeme haupo na pengine mtu unapita chini ya nyumba yake lakini anashindwa kutokana na bei ya kuunganisha umeme ni kubwa . lakini pili ni ile gharama ya kulipia umeme wenyewe.

Mimi katika suala hili naliona gumu hapa, Mhe. Waziri anapotaka tuwashauri wananchi umeme tutausambaza ili wananchi waweze kutumia nishati hiyo badala ya kutumia kuni. Miti inakatwa kwa wingi na *figure* imeonesha hapa ya kusikitisha kabisa kwamba hata hiyo miti yote hiyo tunayokata inabidi tupate na mengine kutoka Tanzania Bara ili matumizi yetu yaweze kwenda vizuri.
Mhe. Spika, *figure* zilizopo ni ile *house budget survey* ya mwaka 2006. Tuliambiwa *survey* iliyofanywa kwa watu laki moja tisini, mia sita na sabini na sita, katika majumba ya watu hao basi asilimia 75 ya watu hao wanatumia kuni, asilimia 21.2 makaa, asilimia 1.3 ndio wanatumia umeme kwa kupikia na asilimia 2 wanatumia majiko ambayo yanatumia mafuta ya taa. Kwa hiyo bado naona ni kitendawili, serikali bado inahitaji kufanya juhudi za makusudi kuona kwamba bei ya kuwaunganishia wananchi kwenye umeme. lakini labda ku-*supsdues* malipo ya umeme ili wananchi waweze kutumia umeme. Bado tafiti za kutumia nishati ya jua, *gas* ni tayari lakini ni ghali. Wananchi wamejaribu *gas*, kwanza kwanza walikuwa na woga lakini sasa wamejua *gas* iliyopo kwa sasa ni *buyo gas* haina tatizo sana. Lakini bado kikwazo kwamba bei yake ni kubwa.

Mimi ningeiyomba serikali katika hili eneo la umeme ni vizuri *access* tumeshaileta kila pahala umeme upo, basi tuwasaidie wananchi wetu kama tutafanya juhudi za ku- *supsdues* au vyengine vyovyote tupunguze gharama za umeme ili wananchi waweze kuutumia umeme nishati ambayo ipo tayari, ili kukatwa kwa miti nako kupungue au kuondoke kabisa.

Mhe. Spika, jengine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusiana na miradi ambayo imetekelezwa na serikali na kidogo kidogo tu nitagusia. Nianze na

mradi huu wa usambazaji maji safi katika Mkoa wa Mjini Magharibi ambao umefadhiliwa na Japan. Mhe. Spika, awamu ya kwanza ya mradi huu umakamilika. Hususan katika jimbo langu wananchi wengi walitegemea kwamba ukikamilika ile awamu ya kwanza na kuanza kwa awamu ya pili basi matatizo ya maji yengekuwa yameondoka. Lakini mpaka leo kuna matatizo sugu ya maji katika jimbo la Mji Mkongwe, katika maeneo ya Mwembetanga na Michenzani.

Mhe. Waziri Kiongozi ningeomba tujue tatizo liko wapi. Matatizo hayo ni ya muda mrefu yalizidi zaidi umeme ulipozimwa lakini mpaka leo bado ni tatizo sugu na mimi nimechoka kwenda kula maana kila siku nakwenda naomba uje unisaidie katika hilo.

Jengine nitoe pongezi kwa Kampinu SOGIA ya Ufaransa ambayo ndiyo ilipewa kandarasi ya kujenga njia ya kurukia umeme. Pia tunawashukuru Banki ya Dunia kwa kutupa msaada wa kujenga barabara. Tulikwenda kutembelea natuliona kwamba kazi hii itakamilika kabla ya wakati uliopangwa. Tunaambiwa kwamba ni mradi wa kwanza ndani ya nchi yetu ambao utakuwa umekamilika kabla ya wakati uliopangwa. Wanahitaji pongezi wao pamoja na taasisi ambazo zimesimamia. Tunashukuru sana katika hili.

Mhe. Spika, jengine katika hili ni mpango ya kilimo cha umwagiliaji maji. Hapa haukuelezwa sana lakini juzi wakati tunaongelea bajeti ya Taifa kulikuwa na suala la kwamba katika kipindi hiki mafunzo ya ushauri ya kuwashajihisha wakulima katika uzalishaji wa mazao ya chakula kupitia kilimo cha umwagiliaji maji yatatolewa.

Aidha ushahishaji na mafunzo ya kumwagia kwa njia ya matone yatatolewa kwa wakulima wenye uwezo wa kununua vifaa vya matumizi katika maeneo yale ya Zingwezingwe, Bumbwisudi, Makunduchi na kadhalika. Haya si mabaya lakini kuweka neno wenye uwezo linabagua. Mimi imani yangu hapa moja kwa moja nakwenda kwamba haya hayatawafikia wanawake ambao ndio wengi, ndio masikini na ndio wanaojihusisha na shuhuli hizi za kilimo.

Ningeomba hapa busara itumike, hawa ambao hawana uwezo nao wafikishiwe taaluma hiyo na waweze kusaidiwa njia ya kupata vifaa ili na wao waweze kuingia katika ukulima huo wa umwagiliaji.

Mhe. Spika, eneo jengine ningelipenda kulizungumzia vile vile ni suala MTAMBUKA la Ukimwi. Ni muda mrefu hili suala tunalizungumzia tunaambiwa ni asilimia 1 na mambo kama hayo, bado hatujaona data hizi zikipungua kila kukicha hatuikuti ile 1% kupungua. Katika MKUZA ule wa miaka mitatu ambao unamalizika tuliwahi kuweka malengo kwamba

itakapofika mwaka 2010 basi HIV *prevelens* kwa wanawake ambao wana miaka 15-24 ambao ni waja wazito ipungue katika *group* hili kutoka 1% mpaka nukta 5 yaani nusu yake 0.5%. Ningeomba serikali hapa itueleze je, tumefanikiwa vipi katika hili. Kwa sababu najua jitihada zipo Wizara ya Afya katika kulishughulikia hili lakini ningependa tuoneshwe kinaga ubaga, haiwezekani kila mwaka tuwe na *effort* zote na fedha tunaelekeza basi tunashindwa kupunguza.

Jengine pia ambalo Mhe. Spika, napenda kuliongelea katika hili ni kwamba kwa kipindi chote serikali inaliangalia suala la ukimwi kwa mtizamo wa jumla. Hili ni suala la kijinsi na jinsia. Kwa maana ya wanawake wanaathirika zaidi kuliko wanaume. Kijinsia basi kuwe na uwiyano katika ushughulikiaji wake. Wale ambao wanaoathirika zaidi ndio wawe walengwa zaidi. Lakini katika mipango yote tunaiyona inakuwa ya kijumla jumla. Hili ni jambo ningependa sana serikali. Kwa sababu kuna data ilikuwa inatizama wangapi wamekwenda kupima wenyewe kwa hiari kati ya wanawake na wanaume. Ikagundulikana wanawake 90.1% wa Unguja hawakuwa tayari wenyewe kwenda kupima yaani hana Ukimwi lakini akajiangalie kujua afya yake. Pemba ikawa zaidi 95.5, lakini wanaume ni *much beater* wanaume wa Unguja ni 80.6 ndio ambao hawajawa tayari kupima na kwa Pemba ni 77.7. Hili moja kwa moja linajjionesha kwamba linataka litizamwe kijinsi na kijinsia. Wanawake katika mgawanyo wa fedha ambazo zinakwenda kushuhulikia masuala haya wapewe uzito wa aina yake.

Si hayo pia ilifanywa survey kuangalia vijana wanaathirika au wana uwelewa gani juu ya masuala ya Ukimwi na ikaonekana kwa wanawake iko chini zaidi. Wanawake ni kidogo zaidi wenye uwelewa ni asilimia 59.3 ndio wana uelewa ukilinganisha na wanaume ambao wapo karibu asilimia 67. Mimi ningeomba serikali hili litizame kwa jinsi yake. Lakini hata hayo maelezo ambayo Mhe. Waziri ameeleza katika kitabu chake, nimesikitishwa na neno moja humu mpaka nikataka kulia.

Tumeambiwa huu ukimwi unashindwa kudhibitiwa lakini kumetajwa neno moja nikasema dah! Kumbe sasa serikali imeliruhusu au imekuwaje. Hivi Zanzibar tuna biashara ya ukahaba. Mimi s najua kuna watu ambao wana tabia zao chafu lakini sikujua kwamba tayari Zanzibar tunabiashara ya ukahaba. Pengine nipo nyuma sana lakini huo ndio ukweli ambao ninao. Ukurasa 37

Sababu za kushamiri kwa matumizi ya madawa ya kulevya ni pamoja na biashara ya ukahaba na mabadiliko ya tabia. Madawa ya kulevya na mambo kama hayo, kwa kiasi fulani kule tulielezwa madawa ya kulevya na jinsi itakavyoshuhulikia. Lakini hili la ukahaba kama ni biashara ni rahisi sana.

Serikali ipige marufuku tu hii biashara ya ukahaba kama inajulikana ipo. Hii itakuwa ndio njia moja ya kudhibiti hii hali.

Unaona hapo nilivyotaja jinsi na jinsia hapo imetajwa ukahaba ukiuliza kahaba ni nani inakwenda kwa mwanamke, mwanamme haingii. Kwa hivyo ni moja kwa moja kwamba wanawake ndio waathirika zaidi wa masuala haya.

Mhe. Spika, muda wako ni mdogo lakini na mimi ningependa nizungumzie suala la uratibu wa shughuli za serikali. Nilisikitishwa kwamba sikuona taarifa yoyote ya uratibu wa shughuli za serikali kwa Afrika Mashariki na nchi za SADDC ambayo tumezoea kuyasikia. Sasa labda kuna maelezo kwamba labda hizi zimehamishiwa sehemu nyengine Waziri atakuja kulieleza.

Jengine nisingeweza kukaa bila ya kulieleza ni shughuli za watu wenye ulemavu. Mimi nimesikitishwa sana na *performance* ya bajeti ilivyokwenda. Walipangiwa kutumia milioni 225.7 lakini hadi kufikia March ni milioni 65 tu walizoingiziwa ambayo ni asilimia 30. Najiuliza hivi hawa walipanga bajeti hii walikuwa hawana kazi nazo hizi pesa. Huku ukisoma kwenye maelezo wanasema uwezo wa taasisi yao kuwasaidia wale ambao wana *demand* ya kusaidiwa ni mdogo. Mimi naona kazi za kufanya wanazo, fedha hizi zinahitajika ni kwa nini serikali wakawapa fedha ndogo hawa. Sitoelewa mkinambia *resorce* za serikali ni ndogo kwa sababu kuna taasisi ambazo hazina umuhimu mkubwa kuliko walemavu, wamepata fedha zao nzuri. Katika mafungu ambayo nimeyaangalia hili linanisikitisha mno. Lakini zaidi la kunisikitisha ni kuwaona katika kitengo hichi hatukuti shughuli za maendeleo, sasa tunawasaidia kweli.

Sisi ni sehemu ya walemavu kabla hujafa hujaumbika wakati wowote linaweza likafuka hilo, sisi ni walemavu watarajiwa, mtu yeyote anaweza akakuwepo katika kundi la walemavu. Tunawasaidia maanaake huku ni pahala ambapo shuhuli za maendeleo nako zingekuwa zinaonekana kama *group* hili la wenzetu hawa ambao sio *majority* lakini ni wenzetu lingekuwa linashuhulikiwa. Kwanza walichotakiwa kupata wamepata asilimi 30 ni kwa nini. Nimesema jibu la kuambiwa kwamba *resource* ni kidogo hapa sitalikubali kwa sababu kuna watu ambao wana ulemavu walihitaji msaada na wengine wa kwenda kusoma wamenyimwa. Tunakusudia nini kwa wenzetu hawa, hilo naomba nipatiwe jibu. Jengine ni kwa nini hakuna miradi ya maendeleo katika fungu hili.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia taasisi niliyokuwepo ya Baraza la Wawakilishi. Jana nilisema kwamba wakati umefika kitengo chako hiki au taasisi yako hii tukufu nayo iwe na mfuko wake. Katika kitabu hiki upo mfuko unaanzishwa wa maafa basi ni wakati mzuri wa waziri kufikiria.

uanzishwaji wa *parliamentary fund*, kwa ajili ya matatizo na unyeti wa shughuli za Baraza hili.

Lakini kuna kitu wakati nasoma shughuli za Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, imenisikitisha sana. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uongozi na ninavyoelewa masuala ya Wawakilishi huwa yanaamuliwa ndani ya Kamati ya Uongozi. Kama kuna chombo kingine au mwenyewe Mhe. Spika, mtanieleza labda ufahamu wangu mdogo. Katika kitabu cha pili cha Muelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo ukurasa wa 73, kuna mikakati pale inayohusiana na Baraza la Wawakilishi.

Mkakati wa kwanza ni kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa wajumbe na wafanyakazi wa Baraza. Hapa napenda nitoe pongezi kwa hili na niishukuru serikali pamoja na wafadhili wetu ninaowafahamu zaidi ni UNDP pamoja na Afisi ya CAG kwa kutusaidia kujenga uwezo wa wafanyakazi lakini pia Baraza la Wawakilishi na hili naomba liendelee.

La pili linasema kuweka utaratibu utakaoziwezesha taasisi za serikali, naomba *underline* neno taasisi za serikali kutoa taarifa na maoni kuhusu utendaji wa kamati za Baraza. Limenishtua mpaka nikaogopa, nikasema sasa sisi ndio chombo tunachosimamia serikali, leo tena sisi tunaandaa mkakati wa serikali kutusimamia siye. Hivi maoni gani taasisi itoe kuhusu sisi labda sijafahamu lakini naomba niwekewe sawa.

Mimi ninachokiona hapa tunaanza kulipunguzia Baraza. Kamati za Baraza ni Wawakilishi wa Wananchi ambao wao kazi yao ni kuisimamia serikali, iweje leo ukamuulize anayesimamiwa umefanyiwa kazi vipi. Mimi hayaniingii kwenye akili yangu ni uwezo wa kupunguzia Kamati za Baraza kufanya kazi nakuwa sielewi kwa kweli, labda nikieleweshwa naweza nikalikubali. Ninachokiona hapa ni kwamba sasa hata Katiba tunaiweka upande. Maana Katiba imesema chombo hiki ndio kinachosimamia serikali, leo tena serikali tuipe fursa nayo iwe inatoa taarifa na maoni Kamati imefanya vipi hehehe! *This is too much.*

Mhe. Spika, chombo chako kinaanza kunyang'anywa madaraka mimi naogopa sana na wajumbe wenzangu naomba hili mlione. Sisi hatuhitaji kusimamiwa na mtu mwengine. Sisi anayetusimamia ni Kamati ya Uongozi na vyombo ambavyo vimo ndani ya taasisi yetu. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tulikatae, kama ni mkakati huu labda tuelezwe mkakati huu kauleta nani? Mimi nimo katika Kamati ya Uongozi hatujaleta hiki kitu. Na hawa wote shughuli zao zinasimamiwa na Kamati ya Uongozi wa Baraza la Wawakilishi. Nyengine ni Kamati ya Wenyeviti hatujalizungumza hili. Sisi kila Kamati inajiamini na Mwenyekiti wake na inafanya kazi kwa kufuata taratibu, Katiba na Kanuni za

Baraza la Wawakilishi, hivi leo tena serikali ikatusimamie siye, itoe maoni juu yetu sisi, hii ni hatari.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba nimelikumbuka kulisema hilo, maana yake jana nilikaribia kulia nilivyoliona nikasema sijui nani mwenye uwezo huu wa kutaka kunyang'anya Baraza la Wawakilishi madaraka yake.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusiana na Tume ya Uchaguzi. Tume hii ina kazi nzito na mimi niiyombee, niitakie kheri kwamba mwaka huu wana kazi nzito na moja ambayo haijawahi kufanyika ni ya historia ni kura ya maoni. Tumejadili hili suala na sheria tumepitisha hapa na mimi niwaombe Wazanzibari wote nilizungumza sana wakati tunachangia wakati ule leo ninachotaka kusema Wazanzibari waone umuhimu wa Wazanzibari kuwa pamoja. Kitu chochote kinapatikana kuingia baraka kwa watu kuwa pamoja.

Tumeona mfano wa nchi ya Singapur ambayo sitachoka kuisema wao wana vyama vinne vikubwa wamegawika makabila mengi, wamegawika kidini lakini wamefika pale walipofika. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya PAC walipata nafasi ya kwenda kuwaona kwa sababu ya umoja wao. Kwa hivyo siona sababu itakapokuja kura ya maoni sitamfahamu Mzanzibari ambaye atasema *no* japo hiyo ni imani yake na ana haki ya kufanya hivyo. Lakini kwa kweli atakuwa hajaitendea haki nchi hii.

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi ya bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi, Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Kaimu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Pemba na Watendaji wote wa wizara hii kwa shughuli mbali mbali ambazo wanazifanya kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Afisi ya Waziri Kiongozi imekusanya shughuli za wizara zote kwa jumla. Hata katika kitabu chake ili twende vizuri itabidi tu-*rush* tu kidogo tuelekeze yale tunayoyaona, lakini kwenye mawizara husika huko ndiko tutakokuja kuelezea umuhimu wa yote tuliyokuwanayo.

Kwanza nianze na suala la mfumko wa bei nchini. Kwa mwaka uliopita bahati nzuri tunaambiwa kwamba bidhaa zilishuka kidogo na wananchi wakapata

unafuu. Lakini hii ilitokana na sababu ya msingi kwamba mafuta yalishuka bei huko duniani na hapa tulipo sisi ndio dunia yenyewe.

Lakini Mhe. Spika, kwa sasa hivi pamoja na bajeti yetu ya serikali kusema kwamba tuna mtazamo wa kuhakikisha kwamba mfumko wa bei haipandi utadhibitiwa na kushuka, labda hapa nipate na kigezo kizuri na wananchi wa wa Zanzibar wasikie. Kwa kuwa hivi sasa mafuta yamepanda sana tumuombe Mwenyezi Mungu yasiendelee kupanda, lakini kila yakipanda hali ya maisha nayo inazidi kupanda. Je, Mhe. Waziri labda serikali itakuwa na mtazamo gani au kitu gani cha kuweza kuzuia huu mfumko wa bei usiendelee? Hili naliomba sana ili wananchi wetu wa Zanzibar kuwatoa wasi wasi.

Mhe. Spika, tunaamini katika ulimwengu wa leo dunia nzima inapiga kelele kutokana na hatari ya kupanda kwa maisha kutokana na mafuta. Na sisi bado tegemezi letu kubwa hatuna kisima hata kimoja katika nchi yetu tunachokitegemea kuchimba mafuta hayo, lakini kwa kuwa tunanunua kutoka nje basi na bidhaa zinazotoka nje halikadhalika zinakuwa vile vile.

Jengine Sekta ya Biashara ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Katika kitabu hiki Mhe. Waziri kakubali kwamba hali ya biashara kutoka Zanzibar kusafirisha nje imeshuka, lakini hali ya biashara kutoka nje kuingia nchini imepanda. Najua ndio utaalamu wa kibiashara, ukiwa na bidhaa utasafirisha kwa wingi huna itabidi uagize kwa wingi ili wananchi wako wanufaike. Lakini mimi naipongeza serikali pamoja na juhudi hizi nzuri za kuhakikisha kwamba hali ya biashara au sekta ya biashara inaendelea vizuri na kusimamia mambo yake vizuri, na mapato kuyasimamia vizuri ili nchi kunufaika na mapato tunayoyategemea.

Kwa hivyo, naiomba hii pia tuiangalia na tuiendeleze vizuri katika kuwahakikishia wananchi wetu wanapata huduma za lazima za bidhaa ambazo hatuna budi kila siku zitumike hasa chakula na mambo mengineyo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulisemea ni suala la uimarishaji wa miundombinu. Kwa kuwa nilisema haya yote yana wizara zake, lakini kwa kuwa afisi hii inakusanya kila kitu basi na hili nimpongeze kwa kuweka vizuri mtiririko huu, ambapo mjumbe akipata kitabu hiki vitabu vinavyoendelea vitakuwa rahisi kwake kuelekeza. Mimi naipongeza sana serikali kupitia wizara ambazo zimehusika na miradi mbali mbali ya miundombinu.

Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na nyenginezo. Kwa sababu tunaamini miundombinu ndio uhai wa nchi, bila ya miundombinu hatuna uhai katika nchi yetu.

Kwenye barabara Mhe. Spika, kama barabara itakuwa nzuri katika maeneo uzalishaji unakua na mahitaji ya watu yanakuwa rahisi. Kwa sababu usafiri unakuwepo na huduma zinakuwa rahisi kupatikana, kwa sababu kila mwenye biashara yake na mwenye kuweza kufika katika maeneo hayo basi atafika kwa urahisi. Kwa hivyo, naipongeza wizara, lakini nampongeza Mhe. Waziri Kiongozi kwa kukusanya haya lakini hasa nitakuja kuipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi hapo baadae bajeti yake itapokuwa tayari.

Mhe. Spika, jengine zuri lililozungumzwa katika kitabu hiki ni suala ambalo linagusa Uwanja wa Ndege. Kusema kweli tunashukuru, usimamizi mzuri umeonesha dhahiri kwamba Mhe. Waziri Kiongozi kupitia mawaziri wanaohusika wanakwenda vizuri katika kuhakikisha yale yote yaliyoguswa na serikali yetu na miundombinu hii inapata mafanikio. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa kuliona hili.

Mhe. Spika, tukija kwenye maji basi maji ni uhai, bila ya maji hakuna uhai. Kiumbe chochote kinategemea maji. Kwa hivyo, serikali katika hatua yake kubwa ambayo imeipiga hii tunasema ni hatua nzuri. Niipongeze serikali kupitia wizara inayohusika kuhakikisha kwamba huduma hii inaendelea vizuri na wananchi wanaondokana na shida ambayo walikuwanazo kwa muda mrefu.

Ombi langu kwa Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na juhudi nzuri, bado naiomba wizara inayohusika kuhakikisha kwamba ili miundombinu hii idumu kwa muda mrefu, ile ada ndogo inayolipishwa basi ni vyema ikaendelea. Tuliona palipokosekana umeme Mhe. Spika, shida iliyotokea katika nchi yetu. Wananchi wengi walipata shida na walikuwa wanasumbuka, lakini kwa habati nzuri Mamlaka ya Maji kwa ujasiri wake nakusimamiwa na wizara inayohusika au chini ya ushauri wa Mhe. Waziri Kiongozi, serikali haikujali gharama, ilijali kuwatumikia wananchi wake na kupatikana maslahi ya kila siku ya mahitaji hayo muhimu ya maji.

Kwa hivyo, naiomba serikali hili liangaliwe na liendelezwe vizuri na huo mradi wa Mkoa wa Mjini Magharibi utapofikia mwisho, basi utoe huduma safi na wananchi wajihakikishie kwamba wanaishi katika maisha yanayofaa nchini mwetu.

Mhe. Spika, tatizo la umeme katika nchi yetu limeweka historia, naweza kusema kwa Afrika Mashariki itakuwa ni historia ya mwanzo haya Zanzibar. Miezi mitatu kukaa katika giza ni suala gumu sana. lakini bahati nzuri serikali kwa juhudi yake imetumia kila njia umeme huo baada ya kukatika karibu miezi mitatu ulirudi. Kuna wengine walifikiria si rahisi kurudi kwa sababu kulikuwa na *rumour* nyingi za hapa na pale. Kwa sababu nasikia kuna vyombo vya

habari vibaya sana, adui nasikia huyu mtu mbaya sana. Tunaambiwa umeme haurudi miaka mitatu, wengine miaka miwili, lakini naipongeza sana serikali kwa kuhakikisha kuwa umerudi kwa wakati.

Mhe. Spika, tulishuhudia shida tuliyokuwanayo katika nchi hii na wananchi kwa jumla walikuwa wanaona shida hiyo ilivyotokea. Mpaka mtoto mdogo anajua adha, lakini bahati nzuri umeme umerudi. Sasa naomba kuishauri serikali kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kutumia umeme ni ridhaa ya mtu. Kama mwananchi katimiza masharti yake katika nyumba yake kwa mujibu wa sheria na chombo kinachohusika kuunganisha umeme ni chombo kimoja tu Shirika la Umeme Zanzibar hakuna chengine. Nashangaa Mhe. Spika, hadi hii leo wakati Baraza lako hili lilipitisha sheria na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi katika Baraza hili alikiri.

Natoa mfano Mhe. Spika kwamba, kuanzia leo natamka rasmi wafanyabiashara wowote wenye uwezo wa kuagizia vifaa vya umeme walete nchini na wakajitokeza wengi sana na wao walifuatilia kwa wale wanaona hawa vyombo vyao vinafaa zaidi kuliko vyengine ndivyo walivyoamua. La kushangaza Mhe. Waziri Kiongozi kupitia kwako Mhe. Spika, hivi sasa kuna malalamiko mengi sana kwamba wananchi hawaungiwi umeme. Suala la kwanza wanaambiwa *wire* hakuna, pili *wire* umeibiwa wakati umeme ulipozimika. Sasa mimi nikaupate wapi? Maduka mmeyateuwa wenyewe yapo, yaani Shirika la Umeme hao, wameyateuwa kwa kuyapendekeza wenyewe leo wanaambiwa wale wenye vifaa pia wasiuze.

Je, Mhe. Spika, huko si kuwarudisha wananchi nyuma? Lengo letu ni kujenga Zanzibar mpya na kuleta maendeleo kwa kila mwenye uwezo wake. Lakini hili linaleta manung'uniko kwa serikali na hili zaidi nitakuja kulisemea siku ya wizara inayohusika. Lakini kidogo nampa taarifa Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa ndiye mkuu wa shughuli za serikali hili alielewe kwamba kuna matatizo makubwa katika Shirika la Umeme ambalo linaendelea hadi hivi sasa.

Mhe. Spika, hiki ni chombo chetu cha Baraza la Wawakilishi na tutakuwa tuna dhima kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu kama hatutowasemea wananchi wetu. Mimi nimesema hapa sikutumwa, naijua hali halisi, lakini kuna waliyotutuma pia wanajua matatizo haya. Kwa hivyo, leo naamini kupitia vyombo vya habari watasikia, lakini naomba serikali itoe kauli juu ya tatizo hili lililojitokeza.

Tatizo jengine ambalo nitalizungumza ni suala la kukabiliana na maafa. Naamini katika sheria ya nchi au ulimwengu huwezi kusema naweka bajeti ya

kifo. Hakuna hiyo ni suala gumu. Lakini naiomba serikali kupitia Afisi ya Mhe. Waziri kwamba Idara ya Maafa ni chombo cha kuondosha matatizo pale yanapotokea. Namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri aliyoyatoa jana nakumbuka kwamba, likitokea tatizo hatokubali lipate muda wa miezi miwili, mitatu halijafanyiwa kazi.

Mimi namuomba sana Mhe. Waziri watendaji wake anao wazuri sana, yaani mahodari, linapotokea suala kama hilo lisichukue hata wiki moja. Kwa sababu aliyepata maafa wakati ule ana shida, kwa hivyo, itolewe awamu ya kwanza hii ya kusitiri tu, baadae ije hiyo hesabu ambayo itakabiliana na hayo mengine ili kumuweka katika mazingira mazuri ya kuishi vyema kwa ile shida yake aliyoipata. Namuomba sana Mhe. Waziri kwa hilo.

Jengine Mhe. Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu ni suala ambalo tunaamini kwamba binadamu wote ni sawa na kila mtu na alivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. Lakini niseme kwamba wenzetu hawa nao wanajitahidi katika mambo yao mbali mbali, wanafanya shughuli zao mbali mbali, wanakwenda kwenye makongamano, semina mbali mbali na kila kitu. Lakini nimuombe Mhe. Waziri idara hii kupitia Mkurugenzi wake na watendaji wake basi wapite katika maeneo ya vijijini.

Kwa sababu katika vijiji vyetu kuna watu wenye ulemavu ambao hawajui chochote kinachoendelea huku. Naamini maelekezo yanaendelezwa. Kwa mfano, hivi sasa kuna skuli ambazo zinawagusa watu wenye ulemavu kwamba wanatakiwa wawe pahala pamoja, lakini faida ile inapatikana kwa sehemu ndogo tu, sio sehemu kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri Kiongozi na hili aliangalie ili watu wetu hawa wenye ulemavu wapate haki yao ya kuishi sawa sawa na watu wengine.

Mhe. Spika, inakaribia miaka sasa tuko hapa Barazani na tunae Mhe. Waziri Kiongozi. Kutokana na hali ya utendaji wake Mhe. Rais wa Zanzibar kakaanaye kwa kipindi chote hiki na maendeleo yaliyopatikana katika nchi hii naamini Rais wa Zanzibar kasimamia vyema kwa kumuamini Waziri Kiongozi kuwa ni mtu ambaye anamfaa kutokana na mambo mbali mbali aliyoyasimamia mpaka kufikia hapa.

Ni vyema Mhe. Spika, kama Baraza lako tukufu hili tujivunie na tuseme kwamba Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na watendaji wake na mawaziri wetu wote wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inafikiwa kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, chama chochote cha upinzani kina haki ya kuyakubali mazuri na kina haki ya kuyakataa mazuri. Lakini lile zuri lisemwe na lenye matatizo

lielekezwe. Mimi nampongeza kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwahani Mhe. Waziri Kiongozi kafanya kazi kubwa, nzuri na kasimamia vyema maendeleo ya nchi hii hadi sasa tunang'ara nchini hapa. Naamini ushauri mzuri, maelekezo anayopewa na anayoyapokea ndio mafanikio ya mambo haya tuliyoyapata hapa.

Katika Baraza hili tuliokuwepo hapa kuna mambo mengi ya matatizo yamejitokeza. Mimi niliitwa mpaka kwa Mhe. Rais, Mhe. Spika, wewe shahidi, Mhe. Waziri Kiongozi, Naibu Waziri Kiongozi, Mhe. Waziri wa Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakuu wa Mikoa kwa ajili ya matatizo ya wananchi wetu vijijini wanaopata shida katika utalii.

Namshukuru Mwenyezi Mungu, namshukuru Mhe. Rais na Waziri Kiongozi kwa kusimamia vyema hadi leo hakuna manung'uniko kwa vijana wetu wanaofanya biashara za utalii katika ukanda wa pwani. Kwa hivyo, hilo ni suala zuri ambalo linafaa kumpongeza Mhe. Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, la mwisho nilisemee kidogo suala la kura ya maoni. Mhe. Spika, hakuna mwananchi anayepiga kura aliyekuwa hana akili, kila mtu ana akili zake timamu na anajua anachokifanya. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani natoa kauli ifuatayo.

Kura ya maoni ni mswada ulioletwa katika Baraza la Wawakilishi, tuliupitia kwa sababu nasema hata mimi Shihata nikiukataa utapita tu, mfano huo, huna ubavu. Lakini mswada ule kupita katika Baraza la Wawakilishi sio mwisho wa safari.

Narudia kauli yangu niliyoitoa katika mswada ule kwamba, bado wananchi waachiwe huru waamue na waamue kwa maslahi wanayoyaona wenyewe. Mimi nasema hakuna anayeitakia janga nchi hii hata mmoja, lakini mwananchi ana uhuru wa kuamua hili anataka hili hataki, asilazimishwe, asitishwe wala asifanywe chochote. Uamuzi wake uwe wa haki yake hiyo ndio demokrasia halisi.

Hata katika kura zitakazoletwa mimi naishauri Tume ya Uchaguzi tuache kusema ndio inatiwa *right* na hapana inatiwa X hakuna, iachwe *open* kabisa mwananchi asibabaishwe kwa ile *right* akaona hapana, wengine hawajui kusoma. Bado narudia tena Mhe. Spika, uhuru wa mwananchi ndio muamuzi mwenyewe, mimi mpiga kura nina maoni yangu. Hili litaleta demokrasia halisi, litaleta ukweli, na litaleta upendo katika nchi yetu, lakini vyenginevyo tunaepuka matokeo ambayo hatuyategemei.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, baada ya matokeo tunaiomba Tume iwe katika ukweli, isije ikasema asilimia 20 iliyokataa wakaambiwa nyinyi *right*, asilimia 80 waliokubali wakaambiwa *wrong.* Hiyo hakuna dunia nzima Mhe. Spika. Naiomba tume itumie haki na wajibu leo na kesho tunakwenda kujibu haki mbele ya Mwenyezi Mungu tunakokwenda.

Naomba sana Mhe. Spika, tuwe katika ukweli, waamue mwananchi kama kakubali iwe kakubali na kama kakataa basi iwe kakataa. Nasema haya sina chuki wala sina tatizo lolote na nchi hii nataka ukweli na uwazi utokee katika Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naipokea hotuba hii ya Mhe. Waziri Kiongozi na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja na nawaomba wajumbe wenzangu waendelee kuchangia na kutoa maelekezo ili kuleta ufanisi katika kazi zetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru ingawaje muda ni mdogo lakini nitajitahidi kujibana. Nianze alipomalizia swahibu wangu Mhe. Ali Suleiman Ali. Ni swahibu wangu wa siku nyingi katika Baraza hili. Na mimi naomba Tume ya Uchaguzi kama alivyoomba yeye iwe adilifu. *Inshaallah* itakuwa adilifu na wananchi wa Zanzibar tukijaaliwa watafanya maamuzi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mfumko wa bei katika ukurasa wa 9 Mhe. Waziri Kiongozi ametaja sababu tatu. Bahati mbaya sababu zote zile haziko ndani ya udhibiti wetu, sasa usimamizi na uratibu wa afisi yake unahitajika sana kuona kwamba tunaandaa mazingira ambayo tutakuwa na udhibiti nayo. Angalau hili la bei ya chakula katika soko la ulimwengu jitihada ifanywe katika masuala ya kilimo ambayo bado nahisi yako finyu sana kuona kwamba tunazalisha ndani ya kutosha.

Bajeti ya kilimo bado ni ndogo na bila ya kufanya hivyo tutaendelea kuagiza kutoka nje na uagiziaji kutoka nje maana yake watatuuzia kwa bei wanayotaka wao. Kwa hivyo, suala la mwanzo hilo lazima usimamizi wa Afisi ya Waziri Kiongozi uone kwamba bajeti ya kilimo inakuwa kubwa.

Suala la mafuta ni suala ambalo nalo tuna uwezo nalo. Lakini bahati mbaya katika kitabu chake Mhe. Waziri Kiongozi amesema kwamba, agizo letu tuliloiomba serikali kwamba suala la mafuta tulisimamie anasema kuwa amemuandikia barua Waziri Mkuu kuhusu mapendekezo ya Zanzibar ya kuliondoa suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta kuwa la Muungano.

Hofu yangu barua ile akiipata Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Pinda ataipindisha itakaa miaka kumi hakuna jibu. Namuuliza Mhe. Waziri Kiongozi ikifika hatua hiyo itakuwaje, au tutasubiri Mhe. Mizengo Pinda na barua yake kwa sababu wewe ndio ushanawa. Nafikiria tuna kazi kubwa.

Suala la ukame nalo mtihani. Kwa sababu suala la *irrigation* hatujalipa mkazo sana, kwa hivyo na hapa tuna kazi ya kufanya. *Irrigation* ya nchi hii imetajwa Kibokwa, Bumbwisudi na Cheju kazi imekwisha. Sasa hatuwezi kuitoa nchi kutokana na mabonge hayo matatu, kuna mabonde ambayo ni *very potential* ya uzalishaji lakini kwa kweli serikali inayachezea chezea katika suala la *irrigation*. Ni maeneo hayo matatu tu ndio yana *pumping irrigation*, Kibokwa, Bumbwisudi na Cheju; maeneo mengine yote yana *irrigation* ya mvua. Kwa hivyo, ukame ukitokea huko ina maana hakuna *irrigation*.

Sasa kazi ifanywe kuona kwamba kunakuwa na *irrigation* kuondoa suala la ukame, vyenginevyo suala hili la mfumko wa bei ambao tunajivunia leo ni wa muda mfupi sana, kesho na keshokutwa tuta-*shoot up.*

Mhe. Spika, jambo jengine nilizungumze nimsifu Mhe. Waziri Kiongozi na usimamiaji wake katika barabara ya Gando, amekuwa akifanya jitihada kuona inajengwa. Namshukuru kwa hili. Namuomba aongeze jitihada ili waliouahidi kwamba itajengwa angalau Julai, basi tuone. Wananchi kwa kweli wameshaanza kukata tamaa. Mimi nimeshawaambia kwamba waziri Kiongozi anafanya jitihada kubwa, naamini wale wanaomsaidia basi watafanya kazi kubwa ili waone kuwa jitihada wanayoifanya inazaa matunda.

Suala jengine ni suala la miradi ya Mfuko wa Kujitegemea. Mhe. Spika, nimesikitishwa kwamba serikali moja, wizara mbili, ina *data* tofauti kuhusiana na Mfuko wa Kujitegemea. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juzi katika kitabu chake cha bajeti alitwambia Mfuko wa Kujitegemea tayari una vikundi wananchi wajasiriamali 3,853 na shilingi 326 milioni zimetolewa. Leo Mhe. Waziri Kiongozi anatwambia ana wajasiriamali 121 kwa shilingi 59 milioni. Sasa vipi jamani serikali moja, au wajasiriamali kila mmoja ana wake?

Labda tuambiwe kwamba kila mmoja pengine mnapiga debe au vipi ndio wajasiriamali tuambiwe, lakini vyenginevyo lazima kuwe na utaratibu wa kuangaliwa wajasiriamali wapi na kuwe na *uniform* yaani *reporting* inakuwa *uniform*. Wajasiriamali tukijua katika nchi lakini Waziri Kiongozi ataje 121, Waziri wa Fedha anasema 3,853. Waziri Kiongozi anasema shilingi 59 milioni, Waziri wa Fedha anasema 326 milioni. Sasa hawa wajasiriamali jamani kila mmoja ana wake? Isijekuwa ni wapiga debe hawa halafu tukawa tunaita

wajasiriamali. Nafikiri Mhe. Spika, lazima tuwe na *uniform reporting* katika suala hili.

Suala jengine ambalo naomba nilizungumze ni ukurasa wa 48, suala la Afisi ya Uratibu. Naomba ninukuu Mhe. Spika. Jukumu jengine ambalo wamelipangia afisi hiyo ya uratibu.

Kifungu cha 63 kinasema kwamba,

> "Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, idara imepanga kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi wa 2010/2015".

Mhe. Spika, mimi hapa kidogo nitakuwa mgumu. Kwa sababu uchaguzi hatujafanya, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi hujajua kama chama chako kitashinda, leo ni vipi unaipangia afisi hii ya uratibu kazi ya kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2010/2015, ikiwa *bench* je CCM utafanyaje?

Sasa Mhe. Spika, hapa pana tatizo kidogo. *Allocation of resource* zinaekezwa hata chama hakijashinda, vipi Mheshimiwa? Kuna mpango ule ambao sitaki niutaje, lakini kwa hapa kidogo nahisi pana tatizo kidogo. Kwa hivyo, nahisi kwamba kifungu hiki kina tatizo Mhe. Spika, lazima tukubaliane kwamba uratibu utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa chama kitakachoshinda, hapo tutakubaliana, vyenginevyo nazuia shilingi Mhe. Spika, nakwambia kabisa katika kifungu hiki.

Mhe. Spika, naona Dk. Mwinyihaji kafurahi kidogo. Eneo jengine ambalo nizungumze ni suala la kero za Muungano. Naomba sana Afisi ya Waziri Kiongozi basi suala hili kwa kweli tunaomba limalize. Nchi yetu inarudi nyuma na kero hizi. Tunapoteza sana mambo mengi na kwa kweli hatuwezi kuendesha nchi kila miaka sisi tunaendelea na kero za Muungano, tuitafutie *methodology* tufanye maamuzi kama ambayo Muungano ulijadiliwa ndani tunaambiwa muda mfupi tukaamua kuungana. Hatuwezi kulea kero hizi tunakwenda nazo tunaya-*bull-doze* hapana bwana. Lazima utafutwe utaratibu.

Nafikiri *arrangement* hii si nzuri, haijazaa matunda mazuri. Kwa hivyo, serikali lazima ikae iangalie utaratibu mzuri ambao utajadili kero kwa muda mfupi na tupate *solution* tuondoke, tuendeshe nchi zetu bila ya matatizo. Ningetoa ushauri huo.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo nilizungumze kwa sababu muda unakwenda sana ni suala la walemavu. Amesema mwenyekiti wangu hapa, sote hapa ni

walemavu watarajiwa, tunaweza kesho na keshokutwa tukawa walemavu. Nilikuwa nina jirani yangu anatembea vizuri baada ya siku mbili kapatwa na *pressure* ya macho akawa kipofu, hivyo kawa mlemavu.

Sasa katika kitabu chake hiki Mhe. Waziri ukurasa wa 54 kuna jambo limenisikitisha na jana nilimwambia Mkuu wa Mkoa wangu nataka nilizungumze hapa naomba Mhe. Waziri Kiongozi alifuatilie. Ukurasa wa 54 kifungu cha 6, idara ilifanya semina kwa Maafisa Tawala wa Wilaya Pemba na kuzitembelea taasisi za watu wenye ulemavu Pemba. Jambo zuri sana, lakini nina wasi wasi Afisa Tawala wangu wa Wilaya ya Wete ama hakuhudhuria hii semina au hakufahamu maudhui ya semina yenyewe. Kwa nini?

Pale katika jengo la Afisi ya Mkuu wa Wilaya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa zamani Mzee wetu Moh'd Mahmoud aliwapa watu wenye ulemavu wa macho afisi yao ili kutekeleza shughuli zao. Na aliwaweka pale kwa sababu ni njiani kwa hivyo, kwa hali yao hawawezi kuwaweka katika eneo ambalo litakuwa na matatizo kidogo. Kwa mfano, wakishuka na gari au wakitembea na zile fimbo zao ni rahisi kupafika. Lakini juzi Afisa Tawala amewapa barua ya kuhama katika afisi na bahati mbaya amewaambia waingie katika kichochoro ambacho achilia mbali mtu mwenye ulemavu, basa hata mtu mwenye macho yake kufika ni mtihani kidogo.

Mimi Mhe. Spika, kwa kweli hili jambo limenisikitisha sana, kwa sababu mtu hujui leo, kesho na keshokutwa hali itakuwaje. Wale watu sasa hivi wanatangatanga hawajui wafanye wapi shughuli zao. Ningemuomba sana Mhe. Waziri Kiongozi, hili suala alifuatilie na anipe jibu. Sipendi kumuamrisha kwa sababu ni swahibu wangu sana, lakini ningeomba atume vijana wake wafuatilie hili suala.

Jana nimeshampa kazi mimi Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, bahati mbaya leo hayupo hapa, lakini hili suala limenisikitisha sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri Kiongozi alifuatilie suala hili na ikiwezekana katika majumuisho anipatie majibu. Anayo *missionary* namna gani ya kupata jibu kwa haraka ambalo litanisaidia mimi na yeye suala hili.

Mhe. Spika, eneo jengine ninalotaka nizungumze kidogo ni Baraza la Wawakilishi. Suala la kwanza ni suala la Mfuko wa Baraza. Ama hili ni jambo ambalo mimi linaniudhi katika nafsi, kuona hadi leo Baraza hili na keshokutwa tukijaaliwa tunakwenda kuhamia katika jengo jipya, basi Katibu au Spika afike pahala aende akapige goti kwa Omar Kingi, kwa kweli hili mimi linaniudhi. Utaratibu huu hakuna katika mabunge sasa, mabunge yote unayotembelea wana *Parliamentary Fund*, sisi mpaka lini mashaka haya Mheshimiwa?

Kwa kweli suala hili hata Spika mwenyewe lile koti lake linamfanya ajibanebane, yaani hajitanui abadan. Ana safari muhimu anataka kwenda aah, ashike tama kwanza afisini, matibabu ya wawakilishi mtihani. Kwa kweli hili namuomba Mhe. Waziri Kiongozi alisimamie, naamini akilisimamia hili Mwenyezi Mungu atampandisha daraja.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa utamu huu na dua hii naomba nimalizie hapo.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Said Ali Mbarouk kwa mchango huo mzuri. Nina orodha ndefu kidogo ambayo ningewaomba wale wanaotangulia wajikumbuke kuwa majina yao yapo na tujitahidi kufika mapema kwa ajili ya kuendeleza mjadala jioni. Nao ni Mhe. Omar Ali Jadi, Mhe. Ali Moh'd Bakari, Mhe. Hamad Masoud, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ashura Abeid Faraji mama yetu, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu na wengine wengi.

Kwa ujumla tufike mapema ili tuendelee na mjadala kama tulivyojipangia.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na tukawa bado ni wazima wa afya zetu. Pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu katika Afisi ya Waziri Kiongozi, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/11.

Mhe. Spika, tatu nimshukuru Mhe. Waziri Kiongozi na watendaji wake wote wa wizara kwa kuiandaa bajeti hii na hadi leo iko mbele yetu na kuweza kutoa michango yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli hakuna kizuri chochote ambacho hakina kasoro na hakuna binadamu yeyote ambaye amekamilika katika utekelezaji au ukaaji wake kwa siku ambazo Mwenyezi Mungu amemuweka. Hiyo ndio sifa ya binadamu, kuwa na upungufu au kasoro.

Mhe. Spika, nianze kuchangia katika bajeti hii pahala alipoachia mchangiaji mwenzangu wakati wa kikao cha mchana Mhe. Said Ali Mbarouk. Mhe. Spika, nilitegemea mimi kama siasa itautumikia uchumi, sio uchumi ukautumikia

siasa. Ndio maana ikawa hatufiki tunakokwenda, kila siku tunasuasua tuko pale pale.

Mhe. Spika, kuiandaa ilani ya chama kabla ya kufika wakati unaohitajika. Hapa ndio nikasema hakuna binadamu asiyekuwa na kasoro au mpungufu. Hata mimi suala hili nilipoliona likanichanganya kidogo, kwa nini? Kwa sababu ilani ya mwaka 2000/2005 na 2005/2010 tayari, lakini hapa tunakwenda na sakata jipya. Hapajajulikana mtoto aliyekuwa tumboni, kama atazaliwa Sharif au atazaliwa Makame. Lakini tayari ameanza kubashiriwa mtoto ni huyu. Hili mimi limenitia wasi wasi. Lakini nina imani ni ukoseaji wa binadamu sio mategemea ya Waziri Kiongozi wala watendaji wake ni makoseo tu, hakutegemea kama afanye hivyo. Nina imani akija atatuelekeza vizuri na upungufu uliotokea ni ubinadamu.

Mhe. Spika, sasa niende katika bajeti. Katika ukurasa wa 40 nianze na Idara ya Mipango na Sera. Mhe. Spika, hii ni idara kubwa sana na tunategemea idara hizi katika wizara au sekta husika itupangie mipango ambayo itakuwa ni endelevu katika uchumi wa nchi yetu. Lakini idara hizi au idara hii ambayo tunaizungumza hivi sasa, hakuna mwelekeo wowote wa utafutaji wa mbinu za uchumi. Wao wako tayari katika idara hii sera yake kuchukua yale anayokuja na kuyatumia tu.

Mhe. Spika, kama baba nyumbani anatakiwa atafute sio apewe wakati bado ana nguvu. Sisi wakati ni wizara kuu ya serikali na idara ambayo ni muhimu kwetu basi ingetafuta nyenzo, ikatafuta angalau mambo ambayo yatatuongezea sisi uchumi kuendeleza uchumi wetu. Lakini hilo halipo.

Mhe. Spika, nimekiangalia kitabu hiki katika mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011 basi miaka hiyo yote malengo hayo hayapo, ilipomalizia ni ile sera na ilani ya CCM. Lakini nina imani kwamba kwa upeo wa Mhe. Waziri Kiongozi basi haya atakuja kuyafafanua vizuri, madhumuni ya idara hii na kazi zake.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye Idara ya Maafa, kila moja ina uono wake na kila moja ina upeo wake. Mhe. Spika, jana tulipokuwa katika maswali na majibu hapa asubuhi basi kuna waheshimiwa wengine walisema wanataka wafahamu, huyu mtu aliyefikwa na janga mmoja mmoja. Tuseme ni maafa au tuseme ni ajali, lakini maafa ni maafa yakiwa ya mtu au yakiwa ya watu. Majanga ndio ni kitu tofauti, kwa sababu majanga ni ya kitaifa. Lakini Mhe. Spika, ningetegemea Idara hii ya Maafa tusingeipangia fedha za matumizi pale yakitokea maafa. Tungeipangia bajeti kubwa ya kukabiliana na maafa pindipo yakitokea. Kama tayari yameshatokea maafa tunachokwenda kuokoa ni msiba.

Mfano Mhe. Fatma alizungumza hapa jana meli ambazo zilitaka kutekwa, basi yale ndio majanga. Kwa hivyo, idara hii masuala yale ikabiliane nayo kabla hawajapata matatizo wale watu. Lakini masikitiko yangu ni kwamba hakuna vitendea kazi hata kimoja. Hatuna uwezo wa kupata ndege, lakini japo maboti tunashindwa!

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi na kwa sababu muda unamaliza na bajeti tayari imeshapangwa, basi apange mipango kwa watakaokuja tukijaaliwa ili waone umuhimu wa Idara ya Maafa na kazi zake, ili yanapotokea maafa au ajali na majanga mengineyo, basi tusiwalaumu watendaji kwamba wameshindwa kufanya kazi wakati hawana vitendea kazi. Kwa hili tutakuwa hatuwatendei haki.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika sehemu ya watu wenye ulemavu, wenzangu wameshatangulia kusema, kwamba kila mmoja ajikadirie wakati ni binadamu hajamaliza kuubwa wala haijulikani atakuwa vipi. Mhe. Saidi Ali Mbarouk yeye kasema kuna jirani yake mmoja kapata homa tu basi akapofuka macho. Lakini sio hayo tu yanatokea majanga mbali mbali kwa binadamu. Kwa hivyo, idara hii tungeipa umuhimu na kuwathamini watu hawa wenye ulemavu, tukawapa haki zao na wakapewa vitendea kazi katika sehemu walizo.

Mhe. Spika, la kusikitisha na kushangaza kule kisiwani kwangu au kijijini kwangu Kojani wako watu wenye ulemavu, kwa bahati nzuri ilikuja ruzuku ya kupewa watu ambao watajisaidia katika maslahi yao. Akatokea kijana mmoja akapewa ruzuku ile kama ni mlemavu. Sijui kama alielekezwa hivyo, mimi naamini hakuelekezwa hivyo. Lakini utashi wake na viongozi walioko chini kule, basi wao ndio waliopanga majukumu hayo kama nitakavyoyaeleza. Kwa bahati nzuri walikuja vijana wenzake kutaka kwenda kujiunga na vikundi vile walivyopewa katika kujisaidia. Jibu alilotoa kijana huyo, akawaambia kwamba mimi siwezi kuwashirikisha, kwa sababu mimi pamoja na ulemavu wangu mnavyoniona nimeambiwa nichukuwe kadi ya CCM na wenzangu watakaokuja basi walete kadi zao za CUF au kadi za vyama vyengine, wachukuwe kadi za CCM ndio wajiunge na kikundi hiki! Kwa kweli yule kijana mimi nilimshangaa sana na majibu aliyotoa nikamwambia sio imesema serikali, msipotowe maneno mnayopewa. Kama ni watendaji wadogo walioko chini basi naweza kukubaliana nayo, lakini kama ni maagizo yanayotoka juu basi sio kweli.

Mhe. Spika, ndio maana nikamwambia Mhe. Waziri Kiongozi katika bajeti iliyopita, kwamba wangepata siku wakafuatilia, wasiwaache wakapaka matope tu hawa. unachokitenda wewe huku serikali mbali na wanaokitenda walioko chini yako mbali, ni matatizo kwa kweli.

Kwa hivyo, ningemuomba tena Mhe. Waziri Kiongozi, japokuwa muda huu umeshamaliza, lakini bado wasaa wa kufanya kazi upo. Mfano mdogo jana ulitokea kwenye maswali na majibu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, alipoulizwa eneo la kujengwa steni Chake Chake. Yeye alisema amepokea taarifa hajawahi kufika. Sasa kupokea taarifa na kuona mwenyewe ni kitu mbali. Kwa hivyo, bado nasaha yangu Mhe. Waziri Kiongozi ni mtu mahiri kwa kazi zako, kwa hivyo jaribu kufuatilia. Wasiipake matope serikali, wala wasiwapake viongozi wa serikali matope wakati sio dhamira yao.

Mhe. Spika, nikiendelea niende katika Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali. Mhe. Spika, hii ni idara ambayo tunaitegemea kwa shughuli zote katika nchi yetu. Nina imani kuna mambo mengi imefanya vizuri, kama mfuko wa TASAF. Nathubutu kusema sio majimbo mengi ambayo hayajafikwa kupata misaada yao au takriban yote kwa Unguja na Pemba. Kwa sababu wamepewa fursa wananchi kuchangua miradi wanayoitaka wao, isipokuwa utashi wa wananchi wenyewe au makundi kwa makundi kupingana, wale wanataka huu na wale wanataka huu. Basi ingekuwa ni vyema kwa awamu hii inayofuatia kwenye mradi huu wa TASAF, wananchi wakitoa mapendekezo yao na serikali izingatie tatizo lipi kubwa zaidi kwa sababu kuna matatizo mengine ni makubwa zaidi. Wengine wanahitaji vituo vya afya, ni tatizo huko kwao, lakini wengine wanahitaji barabara pengine ndio tatizo lao.

Mhe. Spika, sasa tukisema tuwachukulie tu kwa kuwa wanataka hili na wale wanataka hili itakuwa hatufiki pahala, yale malengo yaliyokusudiwa na mfuko huu au azma iliyokusudiwa na serikali tutakuwa hatuipati.

Katika idara hii hii Mhe. Spika, kuna kitu kimoja kimenishtusha, ndio maana nikasema hakuna binadamu asiyekuwa na kasoro wala aliyekuwa mkamilifu. Nilipokuja kukisoma hiki kitabu katika ukurasa wa 44, kupata yale majibu ya Waziri Kiongozi kama amemuandikia barua Waziri Mkuu. Tayari imeshamfika barua ile kwa kufanyiwa kazi katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu limenishtua.

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 12 Januari mwaka huu, kama sitakosea nafikiri kitabu chake cha hotuba ninacho hiki, katika ukurasa wa 34, samahani Mhe. Spika. Ukurasa wa 34 hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alizungumza hivi naomba nimnukuu,

Ukurasa wa 34

> “Anapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kukubali katika mambo ya nishati, mafuta na gesi asilia kutolewa kwenye orodha ya matatizo ya Muungano”.

Watu tukashereheka sana pale. Leo tunapokuja hapa tukaambiwa ameandikiwa barua Waziri Mkuu, Baraza hili tumeshapitisha maazimio. Tulichosubiri bajeti hii ni kuona utaratibu mzima wa upangaji mwezi gani mafuta yataanza kuchimbwa, lakini kumbe tunaanza kuosha nguo sasa wakati nguo ilikuwa imeshakauka imeshatiwa pasi, leo tunaichukua na kuipeleka mtoni tena. Mhe. Spika, haya ni masikitiko kwe kweli. Nataka tujiulize kuna nini?

Nikiendelea kumnukuu huyu huyu Mhe. Rais Karume alisema, "Tumeungana nchi mbili zilizohuru mambo ya kiuchumi ya nchi watajishughulikia wenyewe". Leo kama wenzetu wameshakula dhahabu zao na almasi zao, jamani hili tone tu ambalo ni dogo kwa nini na sisi tusilifanye ni letu tukalifanyia kazi. Kwa kweli Mhe. Spika, hapa kuna jambo.

Mhe. Spika, kwa kusema tusubiri Mhe. Mizengo Pinda aijadili barua, Mhe. Spika, samahani, lugha unajua zinatofautiana kwenye midogo. Mhe. Waziri Mkuu Mizengo Pinda akae kitako aijadili barua, hivi ni kuturudisha nyuma ni kwamba Baraza hili litakuwa halina maamuzi. Wananchi wote wanatusubiri sasa hivi ni hatima ya uchimbaji wa mafuta Zanzibar, sio jenginelo. Leo tukiambiwa mjadala uanze itakuwa ni yale yale aliyoyazungumza Mhe. Fatma kwamba Baraza halina meno tena ya kuweza kuamua mambo yake.

Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri Kiongozi suala hili asilifumbie macho na kama Mwenyezi Mungu akitujaalia ni Urais *Inshaallah* Mwenyezi Mungu keshampa na atazidi kumpa. Lakini masuala yetu ya Zanzibar ya kiuchumi tuwaachie wenyewe Wazanzibari. Sio suala la kura, hatupi kura kwenye CCM lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutamuombea dua nyingi sana azipate hizo kura. Lakini masuala ya Zanzibar kuhusu masuala ya kiuchumi tuwaachie wenyewe Wazanzibari tujadili mambo yetu, tuone faida au tuone hasara ndio kujifunza. Nafikiri Mhe. Spika, hili litakuwa limeeleweka.

Mhe. Spika, jengine nchi yetu imekabiliwa na mambo mawili makubwa ambayo kwa kila mwaka kama huu yanatupa tafrani. Kabla ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi wa Oktoba kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu akituweka hai ni kwamba tumekabiliwa na jambo ambalo hilo litakuwa lina kazi ngumu kuliko mengineyo.

Mhe. Spika, juzi wakati wa maswali na majibu Mhe. Mohamed Ali Salim alitoa mfano kuwa jamani kwa nini kama sisi ni Wawakilishi wa wananchi hapa tusiweze kuliamua hili jambo likawa limekwisha kama ndio twende hivi, wakati wananchi wanatuamini. Mimi nasema wananchi wangu wa jimbo langu wananiamini mia juu ya mia kuamua jambo hapa likawafika wao. Kama kuna mtu ambaye anasema hapana, mimi jimbo langu mpaka wakaulizwe tena,

itakuwa hajafanya haki. Lakini nina wasi wasi na kwa sababu wananchi wengi hawasikilizi vyombo vya habari, basi lile jambo likashindwa kufika pale tunapopataka. Ndio maana nikafanya wasi wasi yale mabadiliko ya mfumo huu tunayokwenda nayo na ile furaha ya makubaliano ikaja ikarudi njiani wakati sio azma yetu.

Mhe. Spika, ningeiomba serikali kwa nia njema kama itakuwa sio kazi kubwa sana, basi tungekaa wawakilishi tukaliamua jamani jambo hili tunakoelekea ni sawa, ili tukafuata uchaguzi unaokuja sasa. Lakini leo keshokutwa kura ya maoni, keshokutwa uchaguzi na wananchi wetu wengi waliomo vijijini kuwapa taaluma wanahitaji kuwafundisha.

Mhe. Spika, mfano mdogo tu ulio hai, ndani ya jimbo langu juzi katika kura za maoni nilikuwa nina wanachama 4243, waliowahi kupiga kura zao ni wanachama 3746. katika sehemu niliyogombea mimi kura 403 ziliharibika. Mhe. Spika, sio kwamba walikuwa wanakataa kumchagua mgombea, ilikuwa hawajui pamoja na taaluma yote iliyopita, mgombea fulani nambari fulani na mgombea fulani nambari fulani. Lakini kwa sababu wananchi wetu wako mbali na taaluma hizi za uchaguzi, matokeo yake ni kura mia nne na kidogo kuharibika kati ya kura zaidi ya elfu tatu.

Mhe. Spika, kwa hivyo wasi wasi wangu na huku tunakoelekea inawezekana wananchi taaluma isije kuwaingia vichwani, hatima yake tukapata sifuri badala ya ziro. Ndio nafikiri Kiswahili mmekielewa hicho, sijasema kwa kukosea. Kupata sifuri badala ya siro maana yake ni kupata kitu ambacho hatutegemei kama kitatokea. Huku ukenda hapana na huku ukenda hapana, ikawa ndio ule uchaguzi ambao tumeuzoea huko nyuma. Ukichagua picha ya mtu ndio na ukichagua kiza unaambiwa ndio ni huyo huyo hapana mtu mwengine. Kwa hivyo, maana yangu ni kwamba tungekaa kama viongozi tukalitafakari tena vyema na tukaleta maamuzi kama tumepitisha hoja tukakubaliana.

Mhe. Spika, mimi kwa kweli nataka niheshimu muda wako. Jengine niende katika sehemu ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kwamba Baraza lipewe haki zake kimsingi kuwa na mfuko wake wa kujitegemea. Mhe. Spika, tusitegemee kwamba siku zote tutakuwa wazima tu hapa, lazima wakati ni binadamu tukumbuke na ugonjwa na lazima kama binadamu tukumbuke na matatizo mengine. Leo Mhe. Spika, ni aibu kama Baraza hili linataka kutiwa rangi mpya mpaka tukasjudie kwa kutaka Shs.1,000,000 ni aibu!

Mfano mdogo uliokuwa hai Mhe. Spika, wewe mwenywe juzi ulinithibitishia, nilitaka fedha za matibabu ukaniambia pesa hazipo. Ukatoa mfano hai wewe mwenyewe ukaniambia ‘Mimi mwenyewe nilikwenda kutaka nauli ya kwenda

Dar es Salaam haipo". Sasa hiki ni kitu cha aibu! Mimi uliponiambia vile *Wallahi* nilitetemeka mwili, nikasema kama ningekuwa nina mtumbwi wangu uliokuwepo hai ningeuuza nikakupa nauli. Ni masikitiko jamani Baraza tulipeni haki zake, hiki ni chombo muhimu katika nchi. Katika mihimili mitatu kimoja ni hiki Baraza kipewe mfuko wake na tuwaamini viongozi wa Baraza. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mimi naamini Katibu wa Baraza hili na Spika wa Baraza hili pamoja na watumishi wake wataifanyia haki fedha ile haitokwenda vinginevyo. Lakini kila siku kwenda kumsujudia Omar Kingi, sijui ndio Omar gani? Hii ni aibu! Kwa hivyo, mimi ninasema bado narudia kauli yangu tufanyeni utaratibu kama mabunge ya wenzetu duniani. Lipewe fursa na lipewe mfuko wake kwa kujitegemea, vyenginevyo itakuwa ni aibu. Mhe. Spika, kuniambia nauli ya kwenda Dar es Salaam haipo, bora mtu wa dala dala anaweza kuipata, maana mwendo mmoja wa pili keshapata nauli ya kusafiri, lakini Spika wa Baraza la Wawakilishi ni aibu.

Mhe. Spika, nafikiri kwa hayo machache naomba nikae kitako naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Kiongozi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Afisi ya Waziri Kiongozi kwa umahiri wao walivyokiandika kitabu hiki ambacho maelezo yake yote yanafahamika na yanaonekana vizuri na kupata kuchangia kwa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupata ugeni hivi karibuni kutoka Uturuki Istanbul, ambapo ugeni huo umekuja kwa nia safi ya kutaka kuanzisha usafiri wa ndege, kutoka Istanbul moja kwa moja mpaka Zanzibar, Zanzibar - Istanbul. Kwa hivyo, hili ni jambo la fahari la kutaka kuzidisha kufufua uchumi wetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa tunategemea kupata ndege za kutoka nchi hiyo ya Uturuki, kwa hivyo hii itakuwa ni moja wapo ambayo itakuwa ni changamoto, ili kuimarisha sekta ya utalii ambayo itasaidia katika vyanzo vyetu vya kukuza uchumi ndani ya nchi yetu. Baada ya kuwa na vitega uchumi vyengine mbali mbali, kwa hivyo pindi tukikikuza na kitega uchumi hiki kwa kupata wageni, watalii, wafanyabiashara mbali mbali kutoka nchi kama hizo kwa kweli itatononesha mfuko wa uchumi katika nchi yetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Rais kwa kupata ugeni huo.

Vile vile nije katika ukurasa wa 19 kifungu cha 13 kuhusu sekta ya biashara na utalii. Mhe. Spika, kwa kuwa tunategemea kupata usafiri kama huo, sijui serikali imejiandaa vipi kutayarisha nyumba za wageni hapa mjini? Vijijini *Alhamdullilah* tuna nyumba nyingi tu na ni nzuri za watalii na wageni mbali mbali wanaofika, lakini hapa mjini tumejipanga vipi au tumejitayarisha vipi? Kwa sababu kama wageni hawa tukiwa nao mijini na vijijini italeta faida kubwa kwa wale wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ili kufanya biashara zao kwa kutembelewa na wageni kama hawa na wengi wao kufanya biashara na wafanyabiashara wetu hawa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri na suala hili akaliangalia sana kwa kuweka mikakati mapema ya kupata hoteli za kudumu na za sifa ya kileo, ili wageni wetu wakija hapa mjini na wao wasisumbuke.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, nakuja katika ukurasa wa 11 kifungu cha 15.0 Uimarishaji wa Huduma za Jamii, Sekta ya Elimu. Katika kuinua kiwango cha elimu Zanzibar Mhe. Spika, kunahitaji walimu wa fani mbali mbali, hususan walimu wa sayansi. Kwa kweli tumekuwa na upungufu sana wa walimu wa sayansi hasa katika madarasa ya sekondari na juu, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu. Kwa hivyo, katika kuelimisha sekta ya elimu Mhe. Spika, kama tutaimarisha walimu wa masomo haya, kwa hivyo kiango cha elimu katika nchi yetu kitakuwa cha hali ya juu na kitapanda vizuri zaidi na vile vile ni vyema baada ya walimu tuliokuwa nao kama tutapata nyongeza zaidi kupata walimu wa nchi jirani ili kusaidia nguvu angalau walimu wawili wawili kwa kila skuli za *secondary* kama vile kutoka Kenye, Uganda hata Uingereza hii itasaidia sana kuwapa kipaji wanafunzi wetu na kuwa na hamu ya kusoma zaidi.

Kwa mfano kuna kipindi hivi Skuli ya Makunduchi ilikuwa ikitembelewa sana na wageni kutoka nje, na walimu kwa hivyo wanafunzi walikuwa na hamu ya kwenda kusoma, japokuwa yule mwalimu mgeni anasomesha sawa sawa na mwalimu wao wa hapa nchini lakini vile akisikia sifa kapata mwalimu mgeni mwanafunzi anakuwa na hamu na bashasha ya kwenda skuli na kujitahidi kusoma. Kwa hivyo Mhe. Waziri katika kuimarisha elimu hili ningeomba nalo liangaliwa na lifikiriwe.

Mhe. Spika, kutoa mikopo kwa elimu za juu hili Mhe. Waziri ningeomba aangalie sana kwa sababu limekuwa na malalamiko sana baadhi ya wanafunzi wa vyuo vyetu vya Unguja huwa wanakosa mikopo hiyo ambayo inatolewa ndani ya Jamhuri ya Muungano, kwa hivyo Mhe. Waziri anayehusika na mambo haya ya Muungano ningeomba hapa apaangalie sana ili na wanafunzi wetu hawa wanaosoma vyuo vya hapa Zanzibar wapate mikopo hiyo ili wajiendeleze. Kama inavyoeleweka wanafunzi wengi hapa kwetu wanaotoka

katika mifupa ya kimasikini, sasa wakifikiriwa kupewa mikopo hii na wao watakuwa na hamu ya kusoma na tutafanikiwa kupata wanafunzi bora katika vyuo vyetu.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa kumi na tano kifungu cha ishirini kuhusu huduma ya maji safi, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri Kiongozi hongera sana kwa watendaji wake wa Wizara hii kwa kuwa kamati yangu ilipangwa kutembelea wizara hii ya Maji tulitembelea sehemu nyingi tu tukakuta juhudi zao wanazofanya za kuboresha haya masuala ya maji, ukija kwa masuala ya kujenga matangi wamefika hatua nzuri. Tumetembelea matangi ya Dole, Kinuni pindi yakimalizika na kujazwa maji kero ya maji katika majimbo haya itakuwa limeondoka wananchi huwa wanasema watapeta, wizara hii imejitahidi vya kutosha safari hii tumeona kwa ushahidi wetu wanavyotandika mabomba na wanavyochimba visima na kuweka matangi, usumbufu wa maji wakimaliza utaondoka kwa Zanzibar na Pemba yake.

Isipokuwa tu kuna tatizo baadhi ya wastaafu waliokuwa sio waadilifu wanafanya mambo ambayo sio sahihi wanaunga maji kiholela bila ya taarifa ya Mamlaka ya Maji na uungaji wao huu ndio unaosababisha upotevu wa maji yasiwafikie wananchi, kwa hivyo hili ningeomba likafanyiwa uchunguzi wa kutosha ili kuwafichua wakorofi kama hawa na kuwachukulia hatua zinazostahiki. Baadhi ya mitaa mingi bomba zimo zimetandikwa na wananchi yakifunguliwa maji wanapata lakini kwa ukorofi wao tu wanaunga maji bila ya taarifa ya Mamlaka na kuzuia maji yale yasiende kwa wale wananchi waliolengwa, kwa hivyo hili linaleta usumbufu katika masuala ya maji.

Mhe. Spika, mimi naipongeza Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa juhudi iliyochukua kipindi kilichopita kwa kuwa maji yalikuwa mchangio wake mkubwa lakini kwa makusudi serikali hii ikakubali kilio cha wananchi na kuwapunguzia nusu kwa nusu, baada ya kuwa elfu nne sasa elfu mbili . Kwa hivyo hili nawapongeza sana serikali kwa kufanya juhudi hii na kubwa tu nawaomba wananchi wenzangu tuchangie mchango huo ili tupate kufanikisha mle mlimokuwa na kasoro ya maji yanapotokezea.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala la umeme kila mtu juhudi ya serikali hii kaiona jinsi ya hatua kubwa iliyochukuliwa ya kusambaza umeme katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwa muda mrefu kulikuwa na usumbufu huo hususan kisiwa cha Pemba lakini mpaka leo *Alhamdullillah*, ukienda Pemba baadhi ya watendaji wengi wamejumuika katika kazi zao za sekta binafsi za uchongaji, kuweka samaki kwenye friji, kuchoma mageti sasa hivi tenda nyingi wanapata kwa kupatikana umeme huo. Kwa hivyo naipongeza serikali kwa juhudi yake hiyo iliyochukua.

Mhe. Spika, isipokuwa pamoja tu kidogo kuna tofauti hili nitaomba lifanyiwe kazi zaidi ili kuondosha usumbufu mdogo mdogo, kubwa katika usomaji wa mita za kawaida ambazo tunazo tokea zamani na wasomaji wa mita za TUKUZA kuna mambo mengine yanaingia ambayo sio ya kutegemewa, utakuta mtu anapigwa mzigo mkubwa wa deni ambalo sio matumizi aliyotumia hili deni la makisio. Ukija kwenye TUKUZA utakuta kuna viashirio vingi vinatiwa vya ulipaji wa *unit* zile baada ya kutumia malipo mawili utakuta magurupu kama manne, kwa hivyo hili linaleta usumbufu kwa watumiaji wa umeme, kama inavyoeleweka umeme ni kitu muhimu katika matumizi ya binaadam na njia moja wapo ambayo inapunguza ukali wa maisha leo umeme ukiwa bei juu, kodi ya nyumba bei juu, maji unachangia hata ukipata posho lako la kula inakuwa usumbufu.Ningeomba sekta kama hizi zikaangaliwa vizuri ili nazo wananchi wetu wakafaidika nazo kuepukana na ule usumbufu wa matumizi makubwa.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa ishirini na tatu kifungu thalathini na moja hifadhi ya mazingira baadhi ya wananchi wanakata miti maarufu ya matunda kama miembe, midoriani, mifenesi, mishelisheli n.k. hii kwa kweli tumeacha zile mila za zamani ilikuwa mara nyingi mila za zamani wazee wetu wengi wenye mashamba hauchukui muda wanapanda miti kwenye mashamba yao lakini sasa hivi tumeacha, kwa kuwa wenzetu walituhisisha hivyo na mfano mdogo tu ukipita Bungi unaona dalili ya miembe jinsi ilivyopandwa na imekaa kwa laini, lakini tokea kuondoka miaka hiyo mpaka leo hakuna watu wanaoendeleza kama vile.

Kwa hivyo ningeomba taasisi husika ikazidi kutilia mikazo kwa wataalam ili kwenda vijijini kwa wenye mashamba wakawapa taaluma na miche ya kupanda miti yetu hiyo ili tusiwe na upungufu wa matunda yanayotokana na matunda ya miti hiyo. Masuala haya ya kukata miti yanakuja kwa ajili ya kuni, mkaa na kujengea na unaleta athari kubwa kwa watumiaji wananchi hili kama linavyoeleweka eneo letu ni dogo la nchi yetu hii ya Zanzibar kwa hivyo hatuna miti ya kutosha, watu wakitumia miti hii kwa kukata kuni au kujengea au makaa tutakuwa na upungufu mkubwa. Kwa kuwa tunayo nchi jirani hapa mambo haya yanapatikana ya makaa na miti na nishati nyengine zinazotokana na miti ningeomba taasisi husika angalau ikapunguza masharti ya uagiziaji kwa wale wanaoagizia ili nishati hii ikaletwa kwa wingi ili kupungua huu ukataji wa miti kidogo tuliyokuwa nayo katika maeneo yetu.

Kwa hivyo ningeomba Mhe. Spika, hapa pakaangaliwa sana ili kuepuka kutumia hii nishati ya miti ambayo tunayo kidogo, katika suala hili la kupunguza utumiaji wa nishati kuna utumiaji wa gesi na majiko yake yanasaidia sana kupunguza uharibifu wa mazingira, lakini tatizo lililojitokeza yale majiko ya gesi yanakuwa rahisi kwa kutumia gesi ile lakini kwa wale

wamiliki ambao wanauza gesi chupa ina uzito wake na gesi inayotiwa mule ina uzito wake, lakini tatizo linalojitokeza kwa makusudi ikiwa chupa ina lita ishirini na gesi inayotaka kutiwa mule ni lita ishirini. Lakini kwa uzito wa chupa tu basi mwananchi anauziwa chupa pamoja na gesi yake ya lita kumi sasa zinapungua zaidi ya lita kumi.

Kwa hivyo utakuwa kwa kuwa hajui na pale alipokwenda kununua hapana kipimo kwa hivyo utakuta mtu yule anadhulumika halafu anatumia chupa ya gesi kwa muda mfupi tofauti na wingi wa gesi iliyokuwemo na manunuzi aliyonunulia, kwa hivyo ningeomba kitengo husika kikajaribu zaidi kutoa taaluma na kuangali ili yule anayeuziwa gesi ilea pate kuuziwa kihalali.

Mhe. Spika, kwa kuwa leo nimesikia ndani ya redio ni siku maalum ya mazingira, kwa hivyo ningeomba siku hii ikawa inatumiwa kwa taasisi husika kutoa taaluma zaidi kwa wananchi wetu angalau ikachukua kama siku mbili tatu kwa kuelimisha na kutoa taaluma jinsi ya kutumia mazingira na kuhifadhi mazingira yetu.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa ishirini na tano kifungu thalathini na nne kinachohusiana na ukanda wa pwani kwa shughuli za kilimo, uvuvi na utalii tatizo kubwa lililojitokeza kumezuka baadhi ya wananchi wetu kuchimba mchanga, kuchimba kifusi, kuvunja kokoto kwa hivyo utakuta mazingira yale yanaharibu haiba na uzuri wa fukwe zetu. Hili limesemewa kwa muda mrefu kwa hivyo ningeomba likafanyiwa utaratibu ili kuepukana na kuja kufurika kwa maji ya bahari kuingia ndani yetu ya ardhi, kwa hivyo hili liangaliwe sana na lipigiwe kelele ili kujiepusha na masuala kama haya.

Kwa kumalizia nije ukurasa wa hamsini kuhusiana na masuala ya TASAF hii imeleta mchango mkubwa sana kwa jamii na imepunguza makero mengi ya wananchi katika maeneo yetu, isipokuwa tatizo tu lililokuwepo kipindi kilichopita mikutano iliyopita ya baraza nilijabu kuzungumza haya masuala ya TASAF kwa kuwa majimbo yetu haya sio mengi ni machache tu kwa hivyo tujaribu kutizama kwa uwiano wa majimbo. Kama jimbo halijaleta mradi wa TASAF basi kamati ikaelimishe au ikatoe ufafanuzi kwa kuwa kuna miradi mingi ili na wao wapate mradi ule wa TASAF, lakini leo itakuwa mradi wa TASAF unakwenda jimbo moja miradi sita mpaka saba kuna majimbo mengine hayana au yana mradi mmoja tu.

Kwa hivyo hapa katika suala la kupunguza umasikini itakuwa liko mbali nasi, kwa hivyo ningeomba wahusika na masuala ya TASAF wajaribu kuangalia hivyo katika *black board* zao majimbo gani yaliyokuwa hayajafanikiwa kupata mradi huo wa TASAF na kama wamepata mradi mmoja wengine wamepata

miratu, kwa hivyo nawao wafanikishwe ili kufufua uchumi na kuwapa maendeleo wananchi wetu.

Mfuko wa Maafa katika kutekeleza malengo yake mimi nampongeza sana Mhe. Waziri Kiongozi na wizara yake jinsi inavyofanya mikakati ya kuimarisha na kusimamia huu mfuko wa maafa, kama inavyosema hapa Maafa ni vyema walivyomuweka yule mama wa maafa anajitahidi vya kutosha tena muadilifu na mkweli na ana huruma na wananchi, akisika pahali pamefika maafa amefika na anahudumia vilivyo. Kwa hivyo nampongeza sana na suala la kuchukua muda kuchelewa ni nzuri sio mbaya kwa sababu unatafutwa uhakiki ili kikitoka kikabidhiwe yule aliyelengwa, naipongeza wizara hii kwa juhudi yao kuwabwa wanayochukua.

Isipokuwa moja tu katika Idara hii ya Maafa imeweza kuendeleza kulipia gharama za mafunzo kwa watu wawili, ningeomba kama kunawezekana hapa wakaongezwa na wengine wawili ikawa jinsia tofauti isiwe jinsia moja tu, ikawa jumla wanne kama kutakuwa na hali inayoruhusu wakafanya hivyo.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa arubaini na saba kifungu cha tatu kutozwa kodi katika bidhaa zinazotoka Zanzibar na kuingia Tanzania Bara hazitotozwa kodi tena, hili naliunga mkono sana kwa kuwa kilio hiki kilikuwepo kwa muda mrefu usumbufu na kero hizi kwa kuwa biashara ukitoa Zanzibar unalipia tena mara mbili kwa kulipia Tanzania Bara, kwa hivyo leo hii yametoka matamko rasmi kwa Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa biashara hizi zikishalipwa Zanzibar hazitolipiwa tena Tanzania Bara. Kwa hivyo hii naipongeza sana ambayo itakuwa changamoto ya kusaidia wafanya biashara wetu kuvutika kuja kufanya biashara hapa nchini kwetu Zanzibar.

Kwa hivyo hili nalipongeza na liwe endelevu lisiwe limetangazwa kwa muda wa miezi sita au mitatu likawa limekatwa liwe linaendelea ili kuwapa fursa wafanya biashara wetu ili na wao wasichoke katika biashara zao, mimi nampongeza Waziri Kiongozi na wizara yake na watendaji wake kwa juhudi kubwa anayochukua katika kuwashughulikia mawizara mbali mbali ili kufanikisha malengo na maipango mbali mbali ya kimaendeleo katika mawizara hayo.

Mhe. Spika, kwa hayo tu naunga mkono hotuba hii kwa kushirikiana na wananchi wenzangu wa jimbo la Amani mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika, *(Makofi)*

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, kwanza kabisa nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kufikia siku hii ya leo tukiwa bado tuko hai, pia nikushukuru na wewe uliyenipatia fursa jioni hii

ya leo kwa kutoa machache miongoni mwa yale ambayo wenzangu wameshatangulia kuyasema.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Waziri Kiongozi kwa uwasilishaji wa hotuba yake hapa barazani namna alivyoweza kuiwasilisha katika chombo hiki na sasa tunaichangia, lakini pia nimshukuru Mhe. Abubakari Khamis Bakary Waziri Kivuli wa wizara hii kwa namna alivyoweza kumshauri Waziri Kiongozi juu ya zile kero ambazo ameziona, pale alipokosoa amekosoa lakini hatimae alielekeza ili kupata kitu cha maendeleo ya nchi yetu na faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kabla sijachangia nataka nimuombee dua rafiki yangu Mhe. Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba Mwenyezi Mungu amjaalie awe Makamo wa Kwanza wa Rais katika nchi hii, akishirikiana na anayetarajiwa waweze kuongoza nchi hii kwa uadilifu tukiamini kwamba kufanya hivyo kutaleta maendeleo katika nchi yetu. Kwa sababu Mhe. Waziri Kiongozi tumekaa nae hapa kwa kipindi cha miaka kumi tunamjua sifa yake na uwezo wake katika kutenda kazi kwa hivyo nafasi hii namuombea Mwenyezi Mungu ampe na tujumuike nae.

Mhe. Spika, baada ya dua hiyo na wewe nikuombee kwamba Mwenyezi Mungu atujaalie tuwepo pamoja katika chombo hicho ili uweze kutuongoza na kuwafundisha wangine wale ambao watakuwa na nia za kugombea kuwa spika ziku za mbele ili kusudi utapokuwa umetoka uwe tayari umeshawaachia vijana kazi nzuri, baada ya hapo niseme tu kwamba nakwenda kwenye michango yangu sasa.

Mhe. Spika, niende katika uimarishaji wa huduma za jamii katika nchi yoyote ile unapotaka kuimarisha huduma za jamii ni lazima watu waelimishwe au wasomeshwe na tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba watu tunawasomesha hapa Zanzibar, lakini watu wakishapata taaluma serikali sijui kwa sababu gani inakuwa haiwatumii wataalam wale na kwaana hiyo sisi tunasomesha tu lakini baadae tukishasomesha basi hatuwatumii wataalam tuliowasomesha na badala yake wanaondoka. Kwa hivyo katika kuimarisha huduma za jamii kwa kuwa watu tukishakusomesha wanaondoka wanakwenda kwengine kwa kuangalia maslahi yao, lakini ile taaluma yao hapa nchini inaondoka na wanabaki wale wale tu ambao kimsingi uwezo wetu ni mmoja na tunaongozana hivyo hivyo tu kimabavu na unakuta mambo hayendi vizuri.

Mhe. Spika, kwa hili niseme kwamba karibuni hivi sisi tulipata safari ya kwenda Maleshia lakini tulipofika huko kimsingi tulijionea mambo mengi, lakini baadae Mwenyekiti wa Kamati yetu Mhe. Fatma Abdullhabin Ferej akatutaka twende tukatembee na mji jirani wa Singapore na tukafanya hivyo,

lakini tulipofika kule tuliweza kujionea mambo mengi sana. Moja tuliyoona kule ni vile walivyojipanga au serikali ilivyojipanga kuweza kuimarisha uchumi wa nchi na kuweza kuinua vipato vya watu wao, leo Singapore ni nchi iliyokuwa duni san asana katika dunia sisi hapa kwetu Zanzibar alhamdullillah tunapata uhuru wan chi yetu tuna rasilimali nyingi tu katika nchi hii.

Lakini wale wakati wa uhuru wao walikuwa wakiungana na Malaysia kwenye miaka ya sitini na sita na sitini na saba lakini wale Malaysia wao walikuwa hawamiliki hata ukwaju hawana mti wowote wala hawana kitu cha kukitumia isipokuwa ni bahari yao. Sasa walikuwa wameungana na Malaysia lakini muungano wao walipokuja kuona kwamba wataburuzwa na watakuwa hawana maamuzi na vibaraka wa muungano walilolifanya ni kujitoa katika muungano ule wao wakawa na nchi yao na wale wakawa na nchi yao.

Mhe. Spika, Malesia wewe umeshakwenda sana si mgeni wale kila siku wana maji mengi halafu wanayatumia kwa vitu vingi, halafu wana michikichi mingi na vitu vingi tu ambavyo kule Singapore kulikuwa hakuna lakini walilolifanya wakawaambia nyinyi Malaysia mnajitoa katika Muungano huu nyinyi mtakufa kwa njaa, wakasema sisi tukifa mkipenda njoni mtuzike hamkupenda basi tuacheni lakini hatuwezi kuwemo kwenye muungano huu.

Sasa leo nenda Singapore ukaone wamekuwa ni nchi tajiri duniani kwa sababu walichokifanya wao ni kusomesha watu wao kwa ajili ya kuja kuikomboa nchi yao, halafu kuna paipu ya maji kutoka Malaysia mpaka Singapore yale maji ambayo wao wananunua kwa matumizi yao bado maji yale wanauza kwa biashara zao na yale mameli yanayokuja pale Singapore wanayauza na wanapata faida kubwa katika nchi. Kwa hivyo Mhe. Spika, katika kuimarisha uchumi ni lazima tujipange na tutoe elimu, lazima tusomeshe watu wetu na tuwe na mkakati maalum kwamba hawa tukishawasomesha lazima warudi kuitumika nchi yao.

Sasa mtu hawezi kujisomesha halafu anakwenda kusomeshwa kwa kuwa elimu yake imsaidie yeye mwenyewe lakini na baadae taaluma yake iweze kusaidia nchi yake, sasa wanakuja watu wameshasomeshwa kwa gharama za wavuja jasho halafu mtu huyo akija unambeza yeye ataondoka, sasa akiondoka utabaki na wale wale matokeo yake nchi haiendi mbele kwa sababu tunashinda kutumia wataalam wetu vizuri. Sasa katika jambo hili ni lazima serikali ione na ijipange upya kuona kuna haja ya kuwatumia wataalam wetu tukishawasomesha ni lazima tuwatumie.

Nashukuru kwamba sasa hivi Wizara ya Fedha tunae Dk. Mwinyi hapa kwa kweli mambo yanakwenda vizuri anatumia taaluma yake vizuri, yupo na safu yake vizuri basi mambo mengi yanakwenda vizuri na yamejitokeza mengi kwa

kuwa watu waliokuwepo pale wana taaluma na wamekubali kuitumikia nchi yao, sasa mambo yanakwenda vizuri kadiri ya uwezo wetu tuliokuwa nao. Lazima tutoe taaluma na sisi tukishatoa taaluma lazima tuwe na mkakati maalum na mikataba ya kuwa mtu akisomeshwa halafu anabaki katika nchi yake na kuitumikia kwa kipindi hiki, sasa hapo tena ukiamua ndio utakwenda kutafuta maisha yako sehemu yoyote ile, lakini lazima nguvu za wavuja jasho uje uzitumikie ili usaidia matatizo ya nchi yako na kuifanya nchi ionekane kama nchi vyenginevyo tutakuwa tunalaumu lakini matatizo tunayo sisi ya kutokuwa na mikakati.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende katika huduma ya maji safi. Mhe. Spika, mwanadamu yoyote au kiumbe yoyote aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu anategemea maji kwa asilimia mia kwa mia ni kweli tuna misaada, lakini bado maji tuliyokuwanayo hapa Zanzibar hayajaweza kutumika vizuri na hayajaweza kuwafikia wananchi ukija Mji Mkongwe wananchi hawajafikiwa na maji, ukenda Bububu bado maji hayajafika humo barabarani mmeshajengwa vizuri kesho unaona inachimbwa kupitishwa maji. Lakini bado miundo mbinu hii haijakuwa makini kwa hivyo mimi nadhani suala lainakuja pale pale katika taaluma si kila mweupe ni mjapani au mchina au ana taaluma kwa sababu ya weupe wake, lazima tutafute wataalam ambao wataweza kufanya jambo litakaloonekana kwa macho na hatimae kuleta faida kwa watu.

Leo hapa Unguja ni eneo dogo sana ambalo tusingekuwa na tatizo la maji kwa sababu maji yapo lakini bado taaluma haijatumika vizuri na ndio maana ukakuta kuna maeneo yanapata maji, kuna maeneo maji hayajafika tokea enzi za Nabii Nuhu mpaka leo alimradi imekuwa ni balaa tu. Sasa mimi nadhani hapa taaluma haijatumika vizuri kwa hivyo maji kwenye ardhi yapo mengi sana lakini bado hatujaweza kuwatumia wataalam wetu ili kupata maji safi, lazima tukubali kwamba suala la maji ni mahitaji ya kila kiumbe kilichokuwa hai na anahitaji maji kama anavyohitaji waziri.

Sasa baada ya hapo naomba tushughulikie suala la maji na tuwape unafuu wananchi wetu kwa sababu sasa hivi kulingana na huu mfumko wa maisha ukweli viwango hivi vya kulipia maji navyo vinataka kuangaliwa upya, kwasababu tulikuja tukapitisha hapa tukaona kwa kiwango hiki inawezekana wakamudu kulipa. Lakini kutokana na hali ya uchumi wetu na hali ya maisha ya mtu mmoja mmoja basi jambo hili inabidi liangaliwe upya sambamba na huduma ya nishati ya umeme.

Mhe. Spika, hapa katika kisiwa chetu cha Unguja tulikuwa na tatizo zaidi ya miezi mitatu kwenye nishati ya umeme ulipata matatizo kila mtu anajua, lakini kwa sababu ya kitu kimoja kikubwa kilichotuunganisha sisi kama wapinzani tulikuwa na uwezo wa kuisema serikali kwa sababu tulikuja kwenye kikao

hapa, lakini hakuna mpinzani yoyote au mtu yoyote aliyesema ndani ya Baraza au nje ya Baraza juu ya kadhia ile na kama mtu alikuwa akisema nje ya Baraza alisema kwa utashi wake tu, lakini tumebaki kuwa kimya tukaliangalia jambo hili tuliliangalia katika huruma kubwa na sisi tulikuwa tunao uwezo wa kusema.

Lakini kutokana na umoja uliokuwepo ulituzuia kusema jambo lolote juu ya suala lile mpaka *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu kajaalia pamoja na jitihada za serikali umeme umerejea katika hali yake ya kawaida. Pamoja na kwamba umerejea bado jitihada nyengine zinahitaji kutumika ili tupate umeme wa ziada litakapokuja kutokea tatizo hili basi tusipate athari tena ya kile kilichotokea. Ni aibu kubwa kwa mtu ambaye ni binaadamu ana akili timamu kuumwa na nyoka mara mbili katika shimo moja itakuwa ni makusudi.

Pamoja na kwamba umeme huu tumeupata pia ni changamoto ya kuhakikisha kwamba tutafute *resource* nyengine zitakazotuwezesha kuwa na umeme wa ziada ili litakapotokea tatizo tuweze kuwatoa wananchi wetu katika matatizo na tupate nishati hii katika hali ya kawaida.

Mhe. Spika, nije katika sekta ya kilimo. Sisi Wazanzibari tunategemea sana kilimo hasa wa mashamba. Sekta hii ya utalii sisi haitusaidii zaidi mtu mmoja mmoja inaisaidia serikali kwa sababu ya kupata mapato na kuendesha serikali, ukija katika wananchi mmoja mmoja kinachotusaidia ni kilimo.

Mhe. Spika, nasikia kuna shule za kilimo, ukenda kwa walala hoi (mashamba) kwa kweli hakuna taaluma yoyote watu wanalima walivyozoea, watu hawaelimishwi, hao mabwana shamba sijui mabibi shamba hawafiki huko. Nashukuru sana kwamba serikali kupitia Wizara ya Kilimo hapa karibuni ilitoa mahonda mengi kwa maana ya kuwafikia wakulima lakini bado hawawafikii, labda kwa shamba za Unguja lakini shamba za kwetu Tumbe na maeneo mengine hazifikiwi, likitokea tatizo la shamba kuingia maji tu basi hawajui wafanye nini.

Vile vile katika jambo hili mashamba yetu ardhi zinakweza, mazingira yanaharibika sana, lakini humuoni mtu wa mazingira wala wa kitu chochote. Tukija hapa kwenye bajeti tunataja tu mazingira lakini mazingira yanaharibiwa, wasimamizi wanalipwa na serikali lakini hawaendi *fild* huko wakaona ile hali halisi yenyewe ilivyo. Labda wanakaa maofisini halafu wanawaletea makaratasi wanakwambia bwana tumekwenda huku na huku.

Mhe. Spika, kwa kweli ukenda huko mashamba vijijini utakuta uharibifu mkubwa wa mazingira hautokani na makusudi, unatokana na watu kutokuwa na taaluma kwa sababu watu hawaelimishwi kitu chochote kile, tukija hapa

mkishakaa huko mawizarani na maofisini na maidarani basi wanasema wamekwenda, wakati hawapewi taaluma yoyote kuhusiana na kilimo. Bado watu wanalima katika hali ile ile ambayo wameizoea.

Mhe. Spika, mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi pia unahitaji taaluma unachukua pesa milioni nzima unakwenda kukitafuta kikundi cha wanawake au wanawake wanaomba hizo pesa lakini hakuna mtu yeyote wa kwenda kuwapa taaluma ya aina yoyote. Wewe unategemea kwamba pale pazalishwe au hizo pesa ziliwe.

Mhe. Spika, mimi nadhani kama tunakusudia kuwawezesha watu kiuchumi na kuwatoa katika jambo hili kuu la umasikini wa kipato basi nadhani kabla ya kuwapa hizo pesa ambazo tumekusudia kuwapa mimi nadhani kuwe kunatolewa taalum ya nini watafanya na halafu washauriwe na serikali lile wanalolifikiria wao na ile fikra ambayo watapewa na wale wataalamu lipi linaweza kuwa bora zaidi kwao. Ingawaje si kila unachokifikiria kwamba kwako ni bora, unaweza ukafikiria kitu lakini ikawa kwako si bora akaja mtu ambaye ana taaluma akakueleweshe kitu hicho kikawa bora zaidi kuliko kile alichokifikiria wewe.

Mimi nadhani isiwe tunazichukua hizi pesa kuwapa watu bila ya kuwapa taaluma na ndio maana zikipelekwa hivi pesa maeneo mengi zinakuwa hazirudi kwa sababu watu wanakula au wanapata hasara hazirejei kwa sababu hawana taaluma ya kitu chochote wanachotaka kukifanya.

Mhe. Spika, nadhani bado hatujawasaidia watu mimi nafikiri serikali tujipangeni katika kuwaondoa watu wetu kwenye matatizo. Vijijini huko wetu wengi hawakusoma, watu hawana elimu ya aina yoyote wala hawana taaluma ya aina yoyote. Wanategemea zaidi *La illah hailallah Muhammad Rasulullah* mtu kenda shamba kapata muhogo ale, huyo ukimpa pesa ukimwambia afanye biashara wakiiomba basi tegemea zaidi ile pesa kupotea kuliko kuzalishwa kwa sababu hana taaluma ya kitu chochote wanachotaka kukifanya.

Mimi nadhani bado hatujawasaidia watu, mimi nafikiri serikali tujipangeni jamani katika kuwaondoa watu wetu na matatizo kwa sababu vijijini huko watu hawakusoma, watu hawana elimu ya aina yoyote wala hawana taaluma. Makundi yapo mengi ni vyema sana kuelimishwa jamii kabla ya kuwapa kitu chochote.

Mhe. Spika, niseme na huu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF umetoa mchango mkubwa kwa jamii. Umetusaidia mambo mbali mbali katika maeneo tofauti kutokana na kero zile tulizokuwa nazo.

Mhe. Spika, kidogo nimepata mashakili kwa rafiki yangu Mhe. Waziri Kiongozi, kuna eneo moja kuna bonde langu kule Tumbe nimeambiwa kwamba bonde hili limetumiwa shilingi milioni 38 kwa ajili ya kuinua muinuko wa kuzuia maji ya chumvi. Mimi nilipokiona hichi kitabu nikaanza kujiuliza bonde gani hili na muinuko gani huo uliotumia milioni 38 nisioujua miye. Mimi nakaa Tumbe na hayo mabonde nayajua, maeneo yanayoingia maji ya chumvi mimi nayajua. Hakuna eneo ambalo limetumia pesa hizi, pesa hizi kazitumia nani. Hii pesa kama imetumiwa imeliwa, kuna wajanja wameshaila wakaona watu wa Tumbe wamekaa kimya sasa ngoja tuwasingizie wao kwamba pesa wamezitumia.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri Kiongozi hili suala alifuatilie kwa sababu ndani yake halina ukweli hata kidogo. Hakuna bonde lolote, hakuna eneo lolote ambalo limetumia milioni 38 kwa kuinua muinuko kwamba kama tuta ili maji ya chumvi yasipite, hapana hata sehemu moja. Sehemu ambazo zinaingia maji ya chumvi ni mbili tu, ni sehemu ya pale pwani ulipokwenda bandarini pale eneo moja linaitwa kwa mwana. Lakini hili eneo la kwa mwana ni mimi na Mbunge wangu ndio tuliokwenda tukainua ule muinua pamoja na kushirikiana na wananchi wa eneo lile, haikutoka hata pesa serikalini.

Kama wanazungumzia pwani pale ni kweli. Kuna vijana wawili wa kibara walipewa tenda ya kupiga ule muinuko kuinua msingi ule mkubwa. Lakini wale ingelikuwa wamepewa hizo milioni 38 watu wawili wale sasa hivi wangelikuwa wameshakuwa matajiri na wangelikuwa hawapo tena pale Tumbe wangelikuwa wameshaondoka kwenda kwao.

Mhe. Spika, pesa hizi zilitumika vipi na alipewa nani. Hili mimi sikubaliani nalo na wala sikusudii rafiki yangu kumpigia buti ya aina yoyote nimeshamuombea dua halafu nije nimpigie buti itakuwa kama sikumtendea haki. Nilazima afatilie kwa sababu ili aone kwamba ukweli uko wapi, wanaotoa pesa hizi ni wananchi wanyonge katika nchi hii. Wanatoa kodi kwa ajili ya kuimarisha nchi yao, kwa ajili ya kutatua matatizo yao, halafu mtu akenda akizila baadaye anasema Waziri Kiongozi zile pesa miye nishazila lakini nitasingizia Tumbe kule kuna muinuko nimeupiga. Hivi sivyo, serikali haiendeshwi kimagube. Serikali inaendeshwa katika misingi ya kuwatoa watu katika matatizo, ukikusudia magube kwa kweli hatutofika.
Mhe. Spika, baada ya hapo nije kidogo katika Tume ya Uchaguzi. Tume ya uchaguzi imekabiliwa na mambo makubwa sana mawili. Suala la kwanza ni kura ya maoni na suala la pili ni uchaguzi mkuu. Mhe. Spika, wewe mwenyewe binafsi ukija humu katika Baraza sisi wapinzani tukiwa haturidhiki tunasema serikali hatuitambui nakuona binafsi unavyosawijika kwa sababu kila linalosemwa kule sisi tunalikataa. Na wewe wakati mwengine kama refarii unalazimika kupendelea timu yako lakini unafika mahali unashindwa, sasa

unasarijika kwa sababu hakuna umoja katika Baraza. Lakini leo uko *comfortable* kwa sababu ndani yake kuna umoja, unajisikia raha kabisa, unajisikia kuendesha vikao vizuri, unajisikia tena kuwa Spika, kwa sababu ya hii hali iliyokuwemo ndani, kama ingelikuwa ni matatizo usingekubali.

Mhe. Spika, tumekwenda kule Malesiya tukenda kwenye Bunge lao kule, anainuka mtu wa serikali kusema kitu fulani, na huku anainuka mtu wa upinzani anamwambia wee muwongo, kaa kimya, kaa chini. Lakini sisi hatujafikia hapo, ingawa vile tulivyokuwa tunakwenda anainuka mtu kule anazungumza wa huku nae anainua hamuungi mkono, aliyoyazungumza inafika mpaka Mhe. Shamsi ni rafiki yangu mkubwa lakini bajeti yake siikubali hata kama ningependa niikubali lakini siikubali kutokana na misimamo ya chama. Sasa Mhe. Spika, hujisikii raha inakuwa si mambo mazuri. Haya yote yalikuwa yakisababishwa na Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu aijaalie Tume ya Uchaguzi hii ione hapa tulipofika tunahitaji kuendelea zaidi mbele sio kurudi nyuma tena. Tumechoka matatizo, hata Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini kila siku anapopata nafasi ya kuongea anaonesha uchungu, anaongea kwa hamasa kutokana na hali ambayo anakutana nayo Pemba mara tu baada ya uchaguzi. Yeye kule anafika mahala hajisikii raha anaona hata kama atamuuliza mtu jambo hatojibiwa vizuri kutokana na hali za kisiasa sisi ni binaadamu na anayesababisha haya ni Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, naomba tume ya uchaguzi isimamie uchaguzi. Kuna watu si kila kitu kizuri wanakipenda kwa sababu kuna watu wenafurahishwa na mambo mazuri. Lakini kuna watu wachache hawapati neema yoyote ndani ya vitu vizuri wao yatokee mashaka ndio wapate neema. Hili ndio asili ya dunia tokea enzi ya Nabii Adam haya yapo kwamba walio wengi wanapenda mema, wachache wakorofi wanapenda mabaya kwa sababu wao katika humu ndio kwenye maslahi yao na hapa Unguja wapo.

Mimi juzi nilipita Kisonge nikakuta bao limeandikwa pameandikwa “Anaetaka mseto ale asilazimishwe” Mimi nikawa nikajiuliza lakini sikusema kitu pale, mimi nikapita nikenda zangu, nikaona sasa hizi ni nyimbo mbaya. Maana nyimbo mbaya haibembelezewi mtoto. Wewe unakwenda unaandika mabango kama yale yanasomwa na watu wengi. Leo tuangalie matatizo tusiangalie kwamba kukitokea matatizo watu wataiba humu, watapata faida mbali mbali. Sasa hayo wanataka yasiondoke lakini jee, ni haki?
Mhe. Spika, katika hili lazima kila mmoja atekeleze wajibu wa jukumu lake alilopewa hapo ndio tutaweza kufika katika malengo tuliyokusudia. Aliyeshinda tukiingia katika uchaguzi apewe haki yake ili kusudi tupate ule uwiano, umoja na mshikamano wa kweli katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, ukitembea katika nchi na ulimwengu siye tuko mbali, siye tuko Akhera na wala hatujafika huko tunakokwenda. Mimi nimeshangazwa sana kujakusikia Ikulu kaja kiongozi sijui kama ni wazungu au warabu eti wametusifu kwa hali ya maendeleo na uchumi. Uchumi gani tulionao? Maendeleo hayo yakowapi hapa? Leo hatuna hata mji wa kuringia. Eti utasikia Mji Mkongwe ndio mji Mkuu wa Zanzibar aah! Hatuna eneo la kuringia hata moja. Bustani ukenda pale Dubei ukiiangalie bustani utatamani ukalale pale pale. Leo hatuna bustani hata moja ya kuringia hapa ya kusema kwamba eneo hili ni eneo zuri. Hata wataalamu wa kusimamia bustani hapa hatuna.

Katika hali hii bado tupo nyuma mno, haya yote tumesababishwa na mivutano na mifarakano ya kila siku isiyo na maana yoyote kwa sababu tu eti siasa. Mtu akitoka huko hatumtaki, akitoka huku ndiyo mwenyewe, hayo sasa yameshapitwa na wakati. Zanzibar hii ni ya Wazanzibari wote sio ya mtu mmoja peke yake. Suala la kwamba kuna watu fulani walipinduwa na wengine hawakupindua walikuwa hawapo wakati huo. Hapana huu ni urithi tuliopewa na Mwenyezi Mungu kwa hiyo hii haki yetu sote. Kwa hivyo tukae pamoja tuwafikiane na tukae tuzungumze tupange mambo yetu kwa pamoja halafu yale tutakayoafikiana ndiyo tuyatende na yale ambayo kuwa hatukuwafikiana tuyaache kwanza mpaka tutakapoafikiana. Lakini isiwe ni sababu ya kugombana.

Mhe. Spika, mimi nimesikitika sana kuona kwamba kuna baadhi ya wajumbe wako humu ndani ya Baraza wanakaa na hamasa wanavyochangia kwamba eeh! Watu wasikilizwe isijekuwa asilimia 20 ndio ikubalike.

Mhe. Spika, katika kutafuta umoja hata asilimia 2 ina nafasi ya kusikilizwa madamu wewe unataka ummoja na wakitokea watu elfu hawataki ummoja wasisikilizwe, hii ndio ahadi hata ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema wanapohitilafiana watu wawili au makundi mawili yasuluhisheni likapotokea kundi moja likakataa katika suluhu ile basi nyie mliotaka suluhu na wale ambao wamekuja kusuluhisha kaeni pamoja muwapige wale mpaka muwatoe katika nchi ile.

Sasa watu wanapokaa wanahubiri tu lugha ambazo hazinamantiki yoyote katika nchi, tunawapeleka watu katika nchi, tunawaleleka wapi watu. Mhe. Spika, likitokea balaa hapa wanaoathirika ni mama zetu, wanaopata matatizo ni ndugu zetu, wanaoathirika ni wazee wetu sisi tunakimbia tunaacha familia zetu. Mpaka lini mambo haya?

Mhe. Spika, ili hali hii iyondoke ni lazima tume ya uchaguzi iwe na uwadilifu. Na uwadilifu huanza mwanzo. Yale masuala ya kachukua kaweka waaaah,

yemeshapitwa na wakati. Sisi tunachokitaka tuingie katika uchaguzi kwa upendo kwa amani atakayeshinda ajione kashinda na atakaeshindwa ajione kama kashindwa lakini ana kila haki ya kumuheshimu aliyemshinda. Isiwe tena balaa hapapitiki, ukija pale Mtendeni kuna mabomu yanavurumishwa watu wanazingirwa inakuba balaa, mashaka makubwa. Huko siku tunakokwenda, tutakwenda huko mpaka lini.

Mhe. Spika, mimi nadhani kwa tulipofika basi hatuhitaji kurudi nyuma hata kidogo. Mimi nakuona wewe peke yako ulipokaa katika kiti chako jinsi unavyosawijika kuona kwamba, mimi nikiisema kidogo serikali unaona ah! sikuitendea haki. Kwa kweli hili sio jambo jema hata kidogo na niiyombe Tume ya Uchaguzi watuandikishe hawajatumaliza, kuna watu tele wanasifa za kuandikishwa wanaachwa tu.

Mhe. Spika, kuna mzee mmoja pale Tumbe miye namjua alikwenda kutaka kuandikishwa akaambiwa alete cheti cha kuzaliwa. Miye nilikuwepo mwenyewe kwa sababu siku hiyo nikuwa nawahudumia wale ambao hawana sifa fulani kuwapeleka Konde. Akawambia ikiwa mnataka nikupeni cheti yule mama ako anacho cheti, lugha zilianza hapo, anamwambia maneno hayo Sheha. Mtu keshapiga kura miaka mia ya nyuma iliyopita halafuu leo unakuja kumwambia akupe cheti cha kuzaliwa, ule umri aliokuwa nao hautoshi kuamini kwamba ana miaka 18 au zaidi, mtu keshokuwa ana mvi kama hizi zangu halafu unakuja kumwambia akupe cheti cha kuzaliwa, kama si kumkejeli ni kitu gani.

Sasa kuna mambo tusiyapalilie kwa sababu ya kuvipanga visheria visivyo na mantiki, mtu mtulie mashaka mdogo ambaye unahisi kwamba huyu mri wake una mashaka naye lakini mzee, keshajukuu halafu unamwambia bwana hapa kana huna cheti cha kuzaliwa hapa huandikishwi kwa kweli hili si jambo zuri.

Mimi Mhe. Spika, niiyombe Tume ya Uchaguzi ili itupe imani zaidi kwamba sasa umefika wakati wa kuwaandikisha wale waliowaacha kwa kumalizia. Tutaingia katika uchaguzi vizuri tu naamini kwa uwezo wa Mungu tutawashinda halafu tutaunda serikali pamoja hakuna tatizo masihofu hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu hii Idara ya Maafa. Katika nchi huwa yanatokea maafa yanayosababishwa na upepo, hali ya hewa, mvua. Lakini kwa sababu ya fungu hili ambalo linaingiziwa ni fungu dogo sana Mhe. Spika. Sasa mimi niiyombe serikali kwamba iyone umuhimu wa Idara hii kuboreshwa zaidi ili yatakapotokea matatizo ya aina hii kwa kweli waweze mara moja kwenda. Juzi kule Tumbi kulinyesha mvua siku mbili kubwa kwa kweli kuna nyumba zaidi ya 17 zilipasuka viwambaza nyengine zikatitia. Watu hawana vya kufanya, hawakupata misaada ya aina yoyote.

Mhe. Spika, naomba serikali ione kwamba kuna haja ya baadhi ya vitengo vyake kuviimarisha zaidi ili itakapotokea dharura yoyote iweze kufika kwa jamii na kuweza kusaidia.

Mwisho kabisa niingie hii Idara ya Watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa kabisa kwamba pesa walioidhinishiwa shilingi milioni mia mbili na kidogo wakapewa asilimi 30 ya pesa hizi, kwa kweli hatukuwatendea haki. Idara hii inahitaji ichukue kutoa taaluma na sio tu kukaa afisini tu. Kule mitaani kuna watu hawajui lolote juu ya hawa watoto wenye ulemavu, wanataka wafikwe, wapewe taaluma. Maana yake yule ukimwambia nenda skuli Mhe. Spika, kwa kweli jamii haiko tayari. Mtu anaona ishakuwa bahati mbaya mtoto wangu hatembei basi, maana hana mtu wa kumshauri juu ya hilo. Lakini watu wa aina yao watakapokwenda kule naamini kama watawezeshwa kifedha wataweza kusimamia vizuri zaidi jamii ile ambayo Mwenyezi Mungu kairuzuku ulemavu.

Mhe. Spika, sisi Mwenyezi Mungu asitufikishe huko *Ishaallah*. Lakini kama tumefika tunahitaji tuweze kuwa na kitengo chetu ambacho kina nguvu, kina uwezo wa kuwafikia watu, kuweza kuwapa taaluma, kuweza kukutana na jamii ambazo kwa kweli zimekata tama na matokeo haya ili kusudi tuwaelimishe na hatimae wawape misaada mbali mbali. Kule Tumbe kuna watu watatu (3) mmoja mwanamke hata siku moja kama kaendewa na mtu yeyote yule kupewa msaada wa aina yoyote. Yeye masikini hajui lolote labda asubuhi akitoka pale kwake basi, lakini hata taaluma yoyote. Na wazee wake katika familia nzima hakuna aliyekwenda skuli wala chuwoni. Mtu kama huyo unategemea aishi vipi.

Sasa kukiwa na kitengo kama hiki kimewezeshwa kinakuja kwetu sisi Wawakilishi, tunawaelekeza sehemu za kuenda ili kusudi wakakutane na hii jamii ili kuwasaidia kielimu na kimawazo. Lakini pesa hii waliyotiliwa kwa kweli ni pesa ndogo mno. Mhe. Waziri Kiongozi, rafiki yangu nakuomba sana kwamba kuna baadhi ya maeneo inabidi uyaangalie kwa fungu la huruma sana. Najua sio wewe lakini ni huko Hazina na Mhe. Waziri wa Fedha yuko hapa ananisikia vizuri, naamini ana huruma, ana imani na anamapenzi na nchi yake, ataangalia kitengo hiki ili kusudi kukuwezesha na kuweza kufanya kazi zao ili na wao kujisikia kwamba hawakuwa na bahati mbaya yoyote Mbele ya Mwenyezi Mungu ila hayo ni mapenzi yake.

Mhe. Spika, baada ya hapo ahsante sana. Naunga mkono hoja.

Mhe. Ashura Abeid Faraji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nikushukuru na tena namshukuru Mwenyezi Mungu na Mtume wetu

Muhammad (SAW) kwa kutufikisha hapa leo tukawa pamoja wote na wenzangu wakubwa na wadogo mimi ndio bibi yao hapa.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa ustahamilivu wako, uvumilivu, penye raha hapaachi karaha, tusamehe sana, kwa sababu huu ni wakati wetu wa kutoka na kurudi.

Mhe. Spika, pia namshukuru Rais wa Zanzibar Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ina nakishukuru Chama Chetu cha CCM. Tunamshukuru kwa kutuletea umeme kule Pemba na mengine hayasemwi ni mengi maana tukisema hapa mpaka asubuhi kweupe tunataa tunamurikwa sasa.

Pia namshukuru na nampongeza mjukuu wangu Mhe. Waziri Kiongozi, namshukuru kwa uhodari wake, kwa umahiri wake, mto mzuri kwa mambo yake. Mambo yake anayaendesha vizuri kwa muruwa, mambo yake ya chama na serikali, hongera baba hongera.

Mhe. Spika, unajua zamani watoto wengi walikuwa wakizaliwa wana makengeza, sasa watoto macho yao mazuri. Labda sisi watu wazima ndio tunaoumwa na macho, lakini sasa watoto wote wana nuru nzuri ndio maana ukawaona wanasoma na wanapasi kweli kweli.

Mhe. Waziri Kiongozi nakupongeza sana kwanza kwa ufatiliaji, hukuyabeza mambo ya ufatiliaji ni mengi sana Pemba huondoki, mengine sikwambii lakini nampongeza baba huyu sana kwa kazi zake nzuri, kajiamini, uwezo anao na maarifa anayo.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana kwa sababu mambo ya kukaa hapa kutwa nikasema siyawezi. Nishakuwa mtu mzima pumzi zangu kidogo. Nawashukuruni pia waheshimiwa wa Baraza hili mulivyo kaa na miye kwa utuuzima wangu. Nawaomba radhi kama nimewakosea lakini sikuwakosea maana kama ningewakosea mngenita siri na kunambia aaah! Bibi wewe mbona una hashuwo, lakini hamkunitapo hata siku moja. Nashukuru mambo yalikwenda sawia (*Vicheko*)

Mhe. Spika, na Mhe. Waziri Kiongozi nawajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wakubwa na wadogo lakini hakuna mkubwa wa kunizidi miye, mkubwa weni ni mimi peke yangu tu. Tuombeane heri murudi na mimi muniombe nirudi, maana hapa mimi kazi yangu ni kula pencheni tu tangu huko ninakotoka mpaka niko hapa. Nawaombeni sana Kusini na Kaskazini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi namkumbusha tu Waziri Kiongozi zamani tulikuwa tukisema Zanzibar ni Njema Atakae Aje na sasa imekuwa zaidi ya hapo. Na

mimi nakuarifu kwamba kule Pemba sasa imekuwa sio Pemba ya kale ni Pemba ya sasa. Ilikuwa nyumba kubwa ilikuwa ina ghorofa moja sasa kuna maghorofa sita, dogo hilo.

Mhe. Spika, karibu tutapata majumba yenye ghorofa 33 kama niliyoiyona kule Ujerumani. Kwa sababu ninakosema ni huko sina kwengine maana miaka yangu inamalizika lakini hujanambia hata siku na mimi nikatembee. Naisha miaka yangu lakini nikirudi unipeleke nchi yoyote nikatembee.

Mhe. Spika, namkumbusha Mhe. Wazirii Kiongozi kama nilivyokwambia kwamba ile sasa Pemba mpya, unajua wewe ukenda unakuwa upo kwenye gari, hebu siku moja ushuke wende kwa miguu utizame mambo. Magari yote yanakaa kwenye maduka hayana pa hala magari yakaka na wenye maduka na wao wakapata nafasi ya kuuza maduka yao, ukweli wa mambo. Hilo tunakuomba siku moja utembee na mimi niwemo humo nikuonesha mambo yaliyokuwepo. Magari yanaanza tangu Benki pale mpaka kama unausikia mji wa Miembeni. Na huku zimeaanza tangu hapa Hoteli mpya mpaka sokoni mpaka njia ya kichungwani kule.

Mhe. Spika, tunaomba haya magari yatafutiwe mahali pa kukaa, kwani wenye maduka ndio wenye maendeleo nchi yetu, kama nchi yetu haina maduka haina maendeleo. Hatupati kwenda madukani tukakata vitambaa vizuri, wanawake wakapita pita wakajijua niko wapi. Hatupati nafasi hiyo, nakuomba uje utizame hali ya nchi ni nzuri sana Pemba ya zamani ilikuwa ikiitwa "P.J" sasa Pemba mpya. Maana ya "P.J" unaijua? Maana yake ilikuwa ni "Pemba ya kijinga" .

Mhe. Spika, namuomba tena Mhe. Waziri Kiongozi ule mkopo unaokopwa wa Karume na Kikwete, hawapewi walio husika hata kidogo. Maana utaambiwa na wewe twende ukaoneshe duka lako, uoneshe maendeleo yako. Ana duka gani na hujampa hizo pesa akafanyia hayo maendeleo na kwa wanawake ndio kabisa, ukenda kwa hao maofisa wenyewe wanakwambia aa ngoja kesho, katafuteni pesa kwamba mtie Benki. Utawambia haya hizi pesa tushachangishana laki mbili katoa benki ili tufungue *account* haya. Tukenda tena katafuteni pesa za mabuku haya njoo utufundishe. Serekete humuoni.

Mhe. Spika, na Mhe. Waziri Kiongozi uwaite wale waliohusika na kutoa hizi pesa zetu hizi Mungu katuletea kwa Maraisi wetu kwa nini zinafichwa fichwa, wengine wanaziolea. Kwa hivyo tunakuomba uwatafute hasa wale wanyonge wenyewe masikini wanawake. Wanawake wanyonge wale mpaka leo, ijapokuwa mnawaowa wanne wanne lakini bado mnauzidisha huo unyonge.

Mhe. Spika, jengine askari wetu, yale majumba yetu ya zamani waliyojengewa toka enzi ya Ukoloni mpaka leo sasa mabovu yanaanguka, basi wafanyiwe

repair kidogo, japokuwa yanajengwa lakini hayajamalizika, yamalizeni wajisikie na wao.

Mhe. Spika, nakuomba tena katika wanawake wenye wadhifa ni kidogo. Baraza la Wawakilishi mnatupa watatu tu, vipi mambo haya? Mbona wanaume wengi, tuzidishie. Hio hio omba omba kwa wanawake wenzetu tuzidishie angalau tuwe watano, watatu kidogo.

Mhe. Spika, nakuomba Wakuu wa Mikoa na wao wawemo wanawake, uwezo wanao, Wakuu wa Wilaya wapo wanawake wazuri kama nini na wanasoma wanaziweza wilaya kwenda hapa na pale wakajua kilimo, maendeleo, yote wanayajua. Sasa tunaomba wanawake nao wachaguliwe. Kwa sababu zamani tumepiga kelele mpaka tukamwambia Mwalimu Nyerere na sisi tupe nafasi, tunashukuru hivi sasa tunapata nafasi mbali mbali wanawake sihaba nashukuru.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawashukuru tena kwa mara ya pili na ya tatu, kwamba msiwe na hofu wala wasiwasi, wa majimbo watarudi na akinamama watarudi. Tuje siku hiyo tupongezane hapa tubebane. Lakini wenyewe wasanii wanasema mambo mazuri hayataki haraka, twendeni hivyo hivyo kidogo kidogo Mwenyezi Mungu atatujalia.

Mhe. Waziri Kiongozi na wewe kila la kheri Mwenyezi Mungu atakujalia, usitie hofu wala wasiwasi uhai wa Mwenyezi Mungu na mimi bibi yako.

Mhe. Spika, la pili, nawapongeza na kuwashukuru wale wapiga kura wangu wote wa Mkoa wangu wa Kusini na mwaka huu nakuja tena mnipe kura wanangu. Watu wakale wanasema, “isio kongwe haivuuku” na “mtu mzima dawa”. Mnaweza mkakosana au mkaumwa na tumbo akenda akawatafutia dawa.

Nawashukuru sana na ninawashukuru wanawake wenzangu wote wa Tanzania, wale viongozi wetu wa UWT na wale waliokuwa tangu ASP mpaka wakaja CCM mpaka hivi sasa wako hapa, ndio tupo hapa. Kwa hivyo, tunaomba na tunawashukuru sana na wale watakaojaaliwa kwenda kwenye majimbo safari hii nyuso zao ziwe za kheri, zijulikane, mmwagiwe kura nyingi mpaka muone leo hiki nini.

Mhe. Spika, mimi kama unavyonijua nikitaka tena kuchangia unipe, nitakuja kumchangia rais kwa sababu sijamsifu humu rais.

Mhe. Spika, naiunga mkono hoja mia kwa mia tatu. *(Kicheko)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu katika kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba leo mkutano mkuu huu wa 20 bado tuko pamoja na unamalizika Zanzibar hii ikiwa ina mageuzi makubwa. Mageuzi ambayo chanzo chake ni maridhiano ya viongozi wakuu wa siasa hapa Zanzibar. Lakini vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, nataka pia nimpongeze Mhe. Waziri Kiongozi kwa hotuba ambayo si ndefu kama Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi na unaona hamu kabisa unapoisoma. Ni mambo ambayo ni mafupi lakini yanajieleza yenyewe.

Naanza kwa kumpongeza Mhe. Haji Omar Kheir kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa hotuba yake nzuri tu na kwa kweli ya aina yake aliyoitoa asubuhi ya leo kama mchangiaji.

Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri Kivuli wa Afisi ya Wazisi Kiongozi kwa hotuba ambayo mimi ilinisisimua sana. kwa sababu kama tutayachanganya yaliyomo kwenye hotuba hii, hotuba ya Mhe. Haji Omar Kheir na hotuba ya Mhe. Abubakar Khamis, Waziri Kivuli, tukaijadili kwa kina naamini kabisa majumuisho atakayofanya Waziri Kiongozi yatakuwa ya kuvutia mno.

Mhe. Spika, hapa Barazani tupo wengi na tunasema mengi, bahati nzuri kila linalosemwa basi linarikodiwa na ukilitaka unalipata kwa njia ya *hansard*. Sasa kwanza nianze na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sikusudii kujibu hoja za waliosema, lakini nakusudia kukumbusha. Hapa bahati nzuri nina *THE REFERENDUM ACT OF 2010*. Naomba katika kuikumbusha Tume ya Uchaguzi nisome *SCHEDULE ORDER FOR REFERENDUM (Made under section 3(1))* ya *article* hii. Inaesma hivi:

> "*To the Chairman of the Zanzibar Electoral Commission. IN EXERCISE of the powers comfered upon me under section 3(1) of the Referendum Act of 2010, I,* Amani Abeid Amani, *President of Zanzibar and Chairman of the Revolutionary Council, do hereby command you to cause to be held a referendum to determine……,* kuna mambo yamejazwa pale. *That, the said Referendum be held on….. day of…… 2010. SIGNED and SEALED by the Seal of the President this…… day of……,2010 and signed the President.*

Hii inaitwa *Order for Referendum.* Lakini *section 3(1)* ya *article* hii naomba vile vile kwa sababu wengine hawana niisome. Inasema hivi:

"Order for referendu. 3(1) Whenever resolution passed by the House of Representatives for holding referendum to ascertain the view of voters on any question or issue or where the President in his opinion things it is necessary or desirable so to do, the President shall, by order in writing published in the Official Gazette, command the Commission to hold the referendum to ascertain the view of voters on that question or issue.

Mhe. Spika, nasoma *Act* hii kwa sababu gani? Nimesema sikusudii kujibu hoja lakini nasema hapa tuko wengi na tutasema mengi. Wengine wanasema yanayosemwa hapa ni kama amri na ndio maamuzi, lakini kwa *section 3.1* ni kwamba, ni Baraza hili lililopitisha azimio la serikali kuleta mswada wa *referendum*. Mswada umeletwa, tumejadili hapa kwa mapana na marefu. Kwanza nataka nikuhakikishie, mimi binafsi na wananchi wa Jimbo la Ole tunaunga mkono asilimia mia moja mswada huu na kwa sababu zifuatazo.

Kwanza ni azimio la Baraza hili lililopendekeza kuletwa mswada huu. Lakini ni sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi nikiwemo tulioujadili mswada na hatimaye kuupitisha na sasa Rais wa Zanzibar tayari ameutia saini na hii *order* tayari ipo.

Sasa Mhe. Spika, kote huko nilikuwa nakusudia kusema haya. Na hapa ndio nawakumbusha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. *Section 7.1* ya *Act* hii inasema hivi:

Ballot paper. "The commission shall be responsible to prepare the ballot papers for voting at a referendum".

7.2, "The ballot papers for voting in a referendum shall state the question or issue to be answered in form of "YES" or "NO".

Tume ya Uchaguzi hamtakiwi kuandika mashairi katika kukubali au kukataa, mkifanya hivyo kinyume cha sheria hii mtakuwa mnavunja sheria. Sheria ambayo tumeipitisha sisi na ni sheria ambayo kwa mantiki yake inaleta mageuzi makubwa katika uendeshaji wa serikali ya Zanzibar.

Nikiendelea na Tume ya Uchaguzi, katika kitabu hiki Mhe. Spika, ukurasa wa 79 kiambatisho Nam.9, kuendeleza daftari la wapiga kura 2010. Mhe. Spika, sisi *CUF* kama wadau au miongoni mwa wadau wakuu wa uchaguzi unaokuja 2010 keshokutwa, tulipata toleo kutoka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Sasa nilipoangalia jedwali Nam. 6 katika kitabu cha hotuba ya Waziri Kiongozi, halafu nikaangalia na karatasi yenye maandishi tuliyopewa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar nikaona kwamba, jedwali hii au karatasi tuliyopewa na Tume ya Uchaguzi moja katika hizi zina kasoro kubwa.

Jedwali hii inaeleza kwamba, “Jumla ya wapiga kura walioandikishwa kwa kila wilaya, Wilaya ya Kati hakuna tofauti ya karatasi mbili hizi, Wilaya ya Mjini hakuna tofauti ya karatasi hizi mbili, Wilaya ya Magharibi walioandikishwa kupiga kura kwa mujibu wa kitabu cha Waziri Kiongozi ni 81,332, lakini kwa mujibu wa karatasi ya Tume ya Uchaguzi ni 81,671. Hapa kuna tofauti ya waliojiandikisha 339.

Wilaya ya Kaskazini ‘B’ hakuna tofauti, Wilaya ya Kaskazini ‘A’ kuna tofauti upungufu wa wapiga kura 5 waliojiandikisha. Wilaya ya Mkoani hakuna tofauti, Wilaya ya Micheweni hakuna tofauti, Wilaya ya Wete kuna tofauti. Kitabu cha Waziri Kiongozi kinasema jumla waliojiandikisha ni 36,001, lakini karatasi ya Tume ya Uchaguzi ina 35,918, tofauti ya waliojiandikisha 83. Wilaya ya Chake Chake kuna tofauti ya mmoja, Wilaya ya Kusini kuna tofauti ya watu 7.

Kwa ufupi tu ni kwamba, tofauti ya jumla ya waliojiandikisha wilaya zote 10 kwenye kitabu cha Waziri Kiongozi ni 4,008,267, lakini karatasi hii ya Tume ya Uchaguzi ni 4,008,536. tofauti ya wapiga kura waliojiandikisha ni 269.

Katika uchaguzi kama huu kura moja ni muhimu sana wachilia mbali kura zaidi ya 200. Sasa mimi suala langu Waziri Kiongozi atapokuja hapa atuelekeze vizuri. Ipi katika hizi mbili ni sahihi, hii ya Tume ya Uchaguzi au hii iliyomo katika kitabu cha Waziri Kiongozi?

Waheshimiwa wenzangu wametangulia kusema hapa kwamba hali sasa hivi ni nzuri na hakuna mtu yeyote mwenye akili yake na anayeipenda Zanzibar hii ambaye anataka hali hii ichafuke. Lakini wengine wamesema vile vile kwamba, chanzo cha migogoro ya uchaguzi vidole vyote vinaelekezwa kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Sasa chanzo ni hiki, Mhe. Waziri Kiongozi utapokuja hapa nakuomba kwa heshima na taadhima utusahihishie mambo haya ili tuondoke hapa tukijua ipi ni sahihi.

Mhe. Spika, leo nimebahatika kuja na Gazeti la Mwananchi la leo. Gazeti hili katika ukurasa wa 12 habari za kitaifa kutoka Bungeni Dodoma, naomba ninukuu ili niende kwenye hoja yangu. “Spika wa Bunge azuia maswali ya uchokozi. Spika wa Bunge Samuel Sitta jana alipangua na kuyakataa maswali matatu yaliyoulizwa na Wabunge kutoka Zanzibar yaliyohusu Muungano, kwa maelezo kuwa yalikuwa ni ya uchochezi”. Naruka hapo.

“Hata hivyo, Spika, huyo alipangua kwa kuyakataa maswali hayo matatu yaliyokuwa ya nyongeza kutoka kwa Mbunge Yahya Kassim Issa, Jussab Ismail Ladu na Hafidh Ali Tahir”. Naruka.

“Baada ya kupangua swali hilo, Spika alipangua pia swali la nyongeza la Jussab aliyetaka kujua mtu aliyeruhusu kuchezewa kwa hati ya Muungano na kuruhusu kuongezwa kwa mambo mengine nje ya 11 ya awali wakati hati hiyo haielezi wala kutoa fursa ya kuongezwa mambo mengine”.

Mhe. Spika, nukuu ya mwisho katika gazeti hili ni hii ifuatayo.

“Hata hivyo, Spika, Sitta alipinga tena swali hilo na kuongesha kushangazwa na Wabunge hao. Leo sijui mkoje”, anakuwa *quoted* Spika wa Bunge. “Yote haya yaliletwa humu Bungeni yakajadiliwa, yakapitishwa, kama mna hoja nyengine si mlete hapa? Kama sarafu iwe ya Zanzibar lete, kama Zanzibar iwe na Baraza lake la Mitihani si mlete”. Alisema Sitta akiwahimiza pia kuleta hoja zao Bungeni.

Mhe. Spika, nasoma haya na naunganisha na haya ambayo nimekusudia kusema. Rais wa Awamu ya Tano wa Serikali hii *Commando*, baada ya kutafakari na kushirikiana na kukaa kitako na wenzake nakushauriana, alitaka kuiingiza Zanzibar katika *OIC*. Hoja hii sote tunakumbuka ilikuja wakati Marehemu Mwalimu Nyerere yuko hai. Lakini wakati huo huo Sheikh Ali Hassan Mwinyi alikuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mkutano kabisa Sheikh Ali Hassan hoja hii aliikubali, akasema wenzenu wana jicho moja kwa maana ya Wazanzibari, lakini nyinyi mna macho 50, mna dhahabu, mna almasi, mna nini na nini.

Kwa hivyo, kwa misingi hii naungana kabisa na kwamba Zanzibar iweze kujiunga na *OIC*. Lakini kama nilivyosema kwamba wakati huo Mwalimu Nyerere alikuwa yuhai na Mwalimu Nyerere kasema hapana. Zanzibar wajitoe halafu Tanzania, tena kasema Zanzibar jitoeni kwa mlango wa nyuma au wa mbele hapa sina hakika vizuri, lakini akasema Tanzania itaingia kwa mlango wa nyuma, lakini ilimradi Tanzania itaingia.

Sasa hii Mhe. Spika, imekuwa ni *issue* siku zote hizo, Bungeni imekwenda lakini hadi leo kama nilivyosema Rais wa Awamu ya Tano hakukaa tu hivi asubuhi akaamka na wazo hili, alishauriana na wenzake watendaji wakuu wa Serikali hii ya Zanzibar, wakaona manufaa ambayo Zanzibar itapata katika *OIC*. Lakini Waheshimiwa hadi leo hii suala hili limekwenda mpaka kama limeyeyuka. Baraza hili waheshimiwa nawakumbusheni lina uwezo mkubwa, Baraza hili ndio mdomo kwa Wazanzibari, bado hoja hata kama imefifia lakini wapiga kura wangu na wananchi wa Jimbo la Ole wanasema rasmi leo niifufue.

Kama Wabunge wa Zanzibar walitakiwa kuleta waliyonayo kama Spika, anavyosema. “Leo mkoje, kama mna yenu si yaleteni”. Mhe. Waziri Kiongozi

hii si kero hili ni tatizo. Nakuomba utakapokuja hapa kutoa majumuisho utwambie tunajiunga na *OIC* au hatujiungi. Nakuomba utwambie tunajiunga au hatujiungi, na kama hatujiungi basi Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa sababu wanatuzuia na wao hawataki kujiunga wafidie kila ambacho tungekipata katika *OIC*. Ndio.

Sasa hivi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali angekuwa hahangaiki tena keshajengewa vyuo vikuu. Mozambique wamejiunga na *OIC*, si nchi ya Kiislamu na Waisilamu ni wachache mno ukilinganisha na Tanzania au Zanzibar. Kwa sababu Zanzibar zaidi ya asilimia 90 ni Waisilamu. Uganda wamejiunga na *OIC* nani hajui, manufaa wanayoyapata ni makubwa kupita kiasi, roho imeundwa na choyo.

Mhe. Waziri Kiongozi nasema hili si kero, afisi yako ndio inayoshughulika na mambo haya, tunataka liibuke upya tujue Tanzania inajiunga na inajiunga lini na kama hawajiungi basi watufidie sisi wanaotuzuia. Kwa sababu ni ajabu jamani mambo kama haya, wewe hutaki kujiunga wenzako wanataka kujiunga wapate manufaa tena manufaa kwa ajili ya nchi hii, wewe bado unazuia maana yake nini? Joka la mdimu. Haiwezekani Baraza hili uhai wake kabla hatujaachana keshokutwa.

Angalau sisi *CUF* huku wengine tushajijua nusu nusu, wenzetu roho juu juu, wengi hawapo hapa sasa hivi wako majimboni huko. Wanataka warudi humu lakini atakayerudi *Inshaallah* kama hoja hii haijesha tunaanza na hoja hii, *Inshaallah* serikali iwe na uhuru wala si awamu ya saba hiyo. Kwa sababu *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu haitakuwa Serikali ya Chama Kimoja. Semeni Amina basi.

Wajumbe: Amina. (Kicheko)

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Niungane mkono na Mhe. Mwakilishi wa Tumbe kusisitiza dua aliyoomba. Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri Kiongozi, Shamsi Vuai Nahodha kuwa makamo wa kwanza wa Rais serikali inayokuja.

Mhe. Spika, nilisoma *article* moja ya *parliamentarian* unatupa magazeti hayo. Katika Mabunge kunakuwa na *jocks, acceptable jocks* wanasema. Na hili lilikuwa Bunge la Australia, wakasema hivi, kulikuwa na mmoja katika Wabunge ni mfupi kama *Eskimo* hivi. Sasa wakati anapewa nafasi kama niliyopewa mimi kusimama na kuchangia basi kwa ule ufupi wake alikuwa haonekani. Sasa walioko *back benchers* wanamwambia Spika, tunaomba Mbunge asimame, yule aliyekuwa anachangia alikuwa keshasimama *full height*. Sasa hivi ni *jock*, lakini hii dua si *jock.*

Mhe. Spika, jengine. Nakushukuru sana kwamba mwaka 2008 mimi na Mhe. Waziri wa Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ulituteuwa kuhudhuria katika mkutano mmoja wa *CPA* uliofanyika Uingereza. Mkutano huu ulifanyika tarehe 17 – 21 Novemba, 2008 huko London kwenye majengo ya Bunge *West Minister*.

Mhe. Spika, washiriki wa mkutano huu maalum walikuwa ni Wabunge 90 kutoka Mabunge 41. Mabunge hayo 41 mengi yalikuwa ya *Common Wealth*, lakini vile vile walikuweko Wabunge katika nchi ambazo sio *Common Wealth.* Senegal, Peruu, Czechoslovakia, Jordan, France, lakini kwa ujumla wetu tulikuwa 90 kutoka nchi 41.

Madhumuhi ya mkutano huu Mhe. Spika, ulijulikana kwa jina la *International Parliamentary Conference, International Development, Scrutinizing AID Effectiveness.* Wabunge wakae waangalie namna fedha za misaada zinavyotumika. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kitu kingine ambacho Baraza hili nawakumbusha, ni kuangalia ni vipi fedha iwe ya misaada, iwe ya wavuja jasho, inatumikaje na watumizi ni nani. Ni serikali.

Sasa taarifa ya mkutano ule yote tuliiandaa pamoja na viambatisho vyote na tukaileta kwako. Sasa leo nakusudia kusema haya yafuatayo: Katika taarifa ile tulipeleka mapendekezo na ninaomba haya hapa leo niyasome.

Mhe. Spika, moja katika mambo hata jana tulikuwa na *professor* mmoja alitaka kujua, Baraza linalokuja ili kuwe na mabadiliko katika kuli-*promote* tufanyeje? Sasa hapa kuna mambo ambayo sijaona yakifanywa na ni hayo ambayo yalipendekezwa na yalipendekezwa kutokana na hiyo *conference* ambayo naizungumzia. Inasema hivi.

“Washiriki wengi wameeleza umuhimu wa Washirika wa Maendeleo kualikwa na kueleza Barazani au Bungeni, misaada inayoipa serikali, namna wanavyoitoa na masharti ya misaada hiyo, ili nalo Bunge au Baraza liwe na ufahamu wa kutosha juu ya misaada hiyo ya maendeleo na hivyo Baraza au Bunge kuweza kuhoji serikali na wafadhili juu ya utekelezaji wa miradi inayotokana na misaada hiyo”. Naamini kanuni zetu zinaruhusu, anaweza akaalikwa mtu yeyote hapa tukishaweka azimio tu kwamba kesho tumualike nani basi tukikubaliana anaalikwa.

Sasa ili njia moja ya kufanya Baraza hili, liwe *effective* katika ku-*Scrutinize AID* misaada basi tualike, maana yake hapa inakuja serikali tu. Dk. Mwinyihaji alisema pale nawashukuru Sudan na wengine.

Sisi tunataka inavyowezekana kwa sababu wengine wapo, basi waje hapa watueleze. Nasema waje watueleze kwa sababu wakija kutueleza wao hawatatueleza kama serikali inavyotueleza, serikali wanatueleza wanavyotaka sisi tufahamu, lakini wale watatueleza utandu na ukoko kwa sababu ya madhumuni makubwa kwamba sisi tuweze ku-*scrutinize,* yaani kuchambua na kuangalia vizuri namna msaada au fedha hizi zilivyoletwa na kwa masharti gani. Ndipo sisi tunaweza kuibana serikali kuwaambia *no*, sharti ni hili na hili mbona mnakwenda huko. Maana ya hii ni kwamba vile vile inaongeza demokrasi.

Mhe. Spika, suala hili wabunge walichangia kwamba mabunge ya namna hii ambayo yanawaalika wafadhili, basi wale wafadhili wenyewe hushawishika kutoa misaada zaidi, kwa sababu mule huwa wanapata sio maswali tu, lakini vile vile na mambo mengine ya kusaidia au namna ya hata kuondoa baadhi ya masharti. Sasa Mhe. Spika, nashauri Baraza lako hili liige jambo hili zuri. Naamini kwamba hii itakuwa ni moja katika njia ambazo zitaongeza ufanisi wa Baraza lako linalokuja keshokutwa *Inshaallah*.

Mhe. Spika, sasa nirudi tena katika kitabu cha Mhe. Waziri Kiongozi. Katika ukurasa wa 45 wa kitabu hiki, kifungu cha 61.4. Hii ni katika utekelezaji wa mwaka 2009/2010. Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imeweza kutekeleza yafuatayo.

Kifungu cha 61.4

> "kuratibu kikao kimoja cha Mawaziri wa Muungano na Zanzibar kilichofanyika tarehe 03/05/2010, hapa Zanzibar".

Mhe. Spika, maswali yangu katika hili ni haya yafuatayo.

1. Mhe.Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2010/11 ni vikao vingapi hasa kimefanyika ukiwacha hiki kimoja au ukijumlisha na hiki kimoja kilichofanyika Zanzibar?

2. Je, huko Bara vilifanyika vingapi?

3. Ni mambo gani katika vikao hivi yamepatiwa ufumbuzi?

4. Kikao hiki cha Zanzibar cha tarehe 03/05/2010 kiligharimu kiasi gani?

Mhe. Spika, mwisho kabisa naiomba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar wajitahidi na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia kuhakikisha kwamba neema na kudra iliyotuvaa hawaivui. Wenzangu wamesema hapa miezi mitatu ya kiza

totoro, ingekuwa ni enzi zile za mivutano basi wengi hapa mngekuwa hamji Barazani, maana yake pale ndio sisi tungepata uwanja, kama ni kuponda ni pale. Lakini hata sisi, kama kulikuwa kuna mtu miongoni mwetu anataka kusema kitu ambacho kitaudhi basi tulikuwa tunamzuia. Tulikuwa tukilaumiwa sisi.

Mhe. Spika, kuna mwandishi wa habari tena wa BBC aliniambia wewe mwaka 2008 wakati umeme ulipozima kila siku magazetini na waandishi wa habari, mbona leo kimpya. Nikamwambia kwani niliposema vile walifanya nini? Kwa hivyo naona ninyamaze kimya, kwa sababu hata nikisema ukweli unaonekana, hata ungewaambia wafanye wangefanya nini? Lakini mimi nasema pamoja na yote tusingeshindwa kugeuza hoja, kilichotufanya tuwe *very stable* na amani ya uhakika ni maridhiano, nani ambaye hajui? Maridhiano haya yameleta mpaka leo tunazungumzia *referendum* ya tarehe 31 Julai, ni haki ya kila mtu kusema *yes* au *no*.

Lakini Mhe. Spika, maridhiano yametupeleka hapo maana yake ni kwamba sisi wenzetu wametufikisha hapa kwa hivyo huko mbele tufyeke zaidi. Mimi na wewe leo tuko Barazani hapa, wengi wamejutia maamuzi yao ya hamasa kwenye Baraza hili na leo hawapo. Wanasema mimi nilikuwepo pale lakini ningefanyaje?

Mhe. Spika, mimi nasema sheria hii ya *referendum* iwe mbaya iwe nzuri, iwe mbovu, iwe inanuka au inanukia ni sheria iliyopitishwa kwa azimio la Baraza, ni sheria tuliyoipitisha hapa, wewe uwe ulikataa ua hukukataa! Nina amini kabisa kuwa ni wachache ambao walikataa au hawakukataa kwa kunyamaza. Wengine walitoka kabisa tulihesabu sisi upande huu, sitaki kuwataja majina, sio vizuri kufufua makaburi saa hizi. Lakini nasema tunaelekea kuzuri na nimeanza hotuba yangu kwa kuisifu hotuba ya Mhe. Haji Omar Kheir, ni Mnadhimu Mkuu wa kambi ya CCM huko. Nani anayemshinda kwa cheo yeye? Yeye kaona mbali mwenzetu na Watumbatu wote wameona mbali. Watu wa Jimbo la Ole tumeona mbali kuliko Watumbatu.

Mhe. Spika, tunaiunga mkono sheria hii na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie Tume ya Uchaguzi ifanye *referendum* kwa utulivu na amani kubwa, matokeo yote yatakayotokea ndio maamuzi ya watu. Nakubaliana kabisa na Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba watu wasitishwe, kampeni za usiku usiku ukifanya hivi itakuwa hivi zikome. Mtu aelezwe vizuri na kazi hiyo imeachiwa Tume ya Uchaguzi, watawaelimisha watu elimu ya uraia. Nina hakika mimi kwamba katika suala hili na Mhe. Waziri Kiongozi nakutwika mzigo mwingine Tume ya Uchaguzi iko kwenye afisi yako, waambie utaratibu utakaotumika katika kampeni nipi.

Mhe. Spika, kutakuwa kuna makundi mawili, moja linazungumzia hoja zao kwa hapana na jengine linazungumzia hoja zao kwa ndio au kuna utaratibu gani? Suala hii uje utueleze Mhe. Waziri Kiongozi, maana yake kila mtu sasa hivi hajui kuna nini? lakini nina hakika wewe kama Waziri Kiongozi basi unajua tunakwenda wapi? Hili sio siri ni jambo la watu, *this is for public*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nampongeza sana Rais wa Zanzibar kwa ukomavu wake wa kisiasa, sheria nyengine nyingi zinachukua muda mrefu kuzi-*assent*, lakini hii haikuchukua muda mrefu tunazo taarifa. *Order* hii pia haikuchukua muda mrefu, mara tu ilipotolewa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi aliueleza umma kwamba tayari nina hati na ninaandaa *referendum*. Tuiombeni Tume ya Uchaguzi iandae *referendum* nzuri, tushirikiane nayo katika *referendum* hii ili ilete matunda sahihi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hotuba hii, lakini Mhe. Waziri Kiongozi asisahau hoja zangu. Nakushukuru sana.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru na wewe kwa kuniweka katika orodha ya wachangiaji wako kwa siku hii ya leo.

Namshukuru Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuandaa hotuba hii akisaidiwa sana na wasaidizi wake mahiri, hotuba ambayo imeweza kusomeka vizuri na kufahamika vizuri. Nawashukuru pia wajumbe wenzangu wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na mchango mdogo sana, lakini pengine utakuwa na hoja nzito. Mhe. Spika, hoja zangu zitakuja katika maswali kwanza, lakini baadae nitafafanua vizuri.

Mhe. Spika, kwanza mimi sitaki kuungana na wenzangu waliozungumzia suala la mafuta iwe kama yapo au hayapo au lini yatapatikana. Mimi nataka kuuliza kwamba katika serikail hii lini jibu la kuwa suala la mafuta limeshaondoshwa katika kero za Muungano. Ni kutaka jibu tu, serikali itujibu tu kwamba tayari au keshokutwa au uchao, basi suala la mafuta litakuwa tayari limeshaondolewa katika masuala ya kero za Muungano, kwa sababu hili limeshatajwa sana na limeshazungumzwa sana na Baraza hili. Haidhuru watu wanaona kwamba Baraza hili halina maamuzi, lakini nasema hili ni Baraza la wananchi, maamuzi tunayo.

Mhe. Spika, lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano ameshaeleza na amelizungumza kwa kina kirefu na kuzitaka pande zote mbili zitekeleze hilo agizo la kuondolewa katika kero za Muungano. Mhe. Spika,

lakini kuna *delaying tactics* zinafanywa na ndugu zetu wa Tanzania Bara au ndugu zetu wa upande wa pili wa Muungano. Sio vizuri.

Mhe. Spika, Rais anaposema na wale wanaohoji kwamba labda ipelekwe kwenye bunge, lakini wamesahau kwamba Rais ni sehemu ya bunge. Rais wa Zanzibar ni sehemu ya Baraza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya bunge. Kwa hivyo, maamuzi yake hayawezi kuhojiwa tena, sasa tunapokuja kuhoji hoji, tusipotekeleza agizo ambacho ni kilio kikubwa cha Wazanzibari, ni kero za Wazanzibari na ni jambo ambalo linaleta kuonesheana vidogo, hilo ni tatizo.

Mimi nadhani Rais anaposema ingawa hatuendeshani kwa amri lakini inakuwa ni amri au ni sheria. Lakini sisi wanajeshi tuliopitia uaskari, kuna *volume* za jeshi, nafikiri *volume* 2 ya jeshi, sina hakika maana ni muda mrefu sana nimeacha. Mwenzangu ananikumbusha ni *disciplinary order*. Kuna *section* moja inasema *obey fast then you complain latter.* Lakini hili agizo kwa nini halitekelezwi. Mkuu wa nchi ameshasema, viwizara vidogo vidogo vinababaisha babaisha, vinatupa kero au vinatupa matatizo. Vinatuletea hofu na shaka juu ya Muungano wetu.

Mhe. Spika, jambo hili limezungumzwa sana na bado ufumbuzi wake hatujaupata. Waziri Kiongozi anasema wameshawasiliana na Waziri Mkuu linafanyiwa kazi, lini litafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, tunataka katika Baraza lijalo Mwenyezi Mungu akitujaalia suala hili liwe limeshapatiwa ufumbuzi. Kwa sababu Baraza lijalo litakuwa jipya, pengine litakuwa ni la mchanganyiko, nasema pengine, sina hakika maamuzi ya wananchi yatakuaje, lakini nasema pengine litakuwa ni Baraza la mfumo wa vyama vingi lakini ndani ya serikali shirikishi.

Mhe. Spika, najua wazi kwamba Rais ajaye wa Zanzibar atatoka ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, ni kutokana na uzoefu wa ndani ya Baraza. Mhe. Spika, watu walikwisha kuonesha nia na kujitangaza ndani ya magazeti. Kama Rais hatokua Waziri Kiongozi basi atakuwa ni Maalim Haroun, kama sio maalim Haroun basi atakuwa ni Maalim Shamuhuna. Lakini Rais ajaye atatoka ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa nini? Kwa sababu uzoefu wangu ndani ya miaka 15 na mimi nikiwa ni muasisi wa mfumo wa vyama vingi ndani ya Baraza hili basi nina uzoefu kwamba Komandoo alikuwa ni mwakilishi na ushahidi kwamba Dk. Aman alikuwa mwakilishi. Lakini nina ushahidi kwamba Rais Mkapa alikuwa mbunge na Rais Jakaya alikuwa mbunge.

Mhe. Spika, huu unanionesha kwamba basi kuna harufu harufu ya Rais ajaye akatoka ndani ya Baraza la Wawakilishi. Lakini atatoka kwenye CCM. Kwa

hivyo, tunataka Rais ajaye asimamie vizuri Mhe. Spika, masuala ya kero za Muungano zinatufikisha pahala pabaya sana.

Mhe. Spika, kama hiyo haitoshi kuwa ni kero ya Muungano. Jengine nataka kumuuliza Mhe. Waziri Kiongozi, hili suala najua liko afisini kwake, inawezekana amesahau kuliingiza kwenye hotuba yake, ni binadamu sio kwa dharau pengine amelisahau. Kwa hivyo, ningependa kumuuliza Mhe. Waziri Kiongozi kwamba ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawaeleza, itawaambia, itawatangazia au itawajulisha wananchi kwamba suala la ongezeko la bei ya mafuta liko katika *tariff* moja na bei ya Tanzania Bara. Narudia.

Mhe. Spika, Zanzibar tunauziwa umeme na wenzetu Tanzania Bara kinyume na maelekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumepandishiwa kwa asilimia 168 ukilinganisha na asilimia 27 ya Bara. Sasa hili suala najua liko afisini kwako Mhe. Waziri Kiongozi. Nakushukuru sana Mhe. Waziri Kiongozi kwa hekima yako na kuumwa na nchi yetu, hili suala wewe umeshalifanyia kazi. Lakini Tanzania Bara EURA na TANESCO wanalipiga mpira.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Afisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshatoa agizo kwamba bei zote ziwe sawa sawa. Bei wanayouziwa wateja wa Tanzania Bara na bei wanayouziwa wateja wa Zanzibar zote ziwe sawa sawa, hiyo ni amri imetolewa na waziri mkuu mtendaji mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametoa agizo hilo kuipeleka Wizara ya Nishati na Madini, lakini utekelezaji wake haupo.

Mhe. Spika, wizara isiyosikia agizo la mkuu wa serikali, inataka isikie agizo la nani. Mhe. Spika, serikali ni pamoja na kutii, serikali lazima iwe na nidhamu na uongozi ni lazima uwe na nidhamu. Haiwezekani hata siku moja kiongozi wako wa juu akakupa agizo wewe wa chini ukawa unalipiga chenga ukawa hulitekelezi. Serikali kama hiyo itakuwa haina nidhamu, wizara itakuwa haina nidhamu.

Mhe. Spika, na hiki ni kilimo kikubwa sana cha Wazanzibari, naomba uniruhusu ninukuu ripoti ambayo kamati yangu imepata ripoti ya umeme, inasema;

“Mnamo tarehe 24 Disemba mwaka 2007 mamlaka ya udhibiti wa huduma za nishati na maji EURA ilipandisha bei za umeme kwa wateja wa upande wa Zanzibar, ambayo iliongezeka kwa asilimia 168 kutoka Shs. 28 kwa *unit* moja ya *kilowatts* hadi kufikia Shs.75 kwa *unit* moja. Kwa upande wa wateja wa

Tanzania Bara umeme ulipanda kwa asilimia 21.7 tu, bei hiyo mpya ilianza rasmi tarehe 1 Januari mwaka 2008.

Mhe. Spika, sasa kwa kuyaona haya, Afisi ya Waziri Kiongozi, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na Afisi ya Waziri Mkuu waliliona hili ni tatizo ndio maana Afisi ya Waziri Mkuu ikatoa agizo kwa Wizara ya Nishati na Madini ya Tanzania Bara, kwamba hili ni tatizo na walifuatilie. Haiwezekani nchi tunasema nchi mbili au nchi moja, maana Zanzibar ni nchi, lakini wanavyosema Zanzibar ni nchi ndani ya Muungano, sawa. Sasa Muungano wenyewe umeshakuwa na kasoro ndogo ndogo kama hizo, umeshakuwa na matatizo makubwa makubwa kama hayo. Zanzibar ni nchi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Sasa ndani ya Jamhuri ya Muungano kunafanywa manyanga kama hayo, tutaionaje sisi wizara hii.

Mhe. Spika, nasema hili ni kero, lakini kero hili ndio namuomba Waziri Kiongozi, pamoja na kwamba wizara yake imeshafanya juhudi kubwa sana ya kulifuatilia suala hili, lakini bado tunapigwa dana dana. Je, ni lini serikali itakuja na jibu rasmi kwamba bei za umeme Bara na Zanzibar zinalingana, kwa kuwa sisi ni wateja wao wakubwa. Mhe. Spika, naomba suala hilo lizingatiwe.

Mhe. Spika, suala jengine la mwisho ni kwamba Baraza letu hili la wawakilishi tunakaribia kuagana, tumekaa vizuri, tumekaa kwa ustaarabu mkubwa, tumeheshimiana, tumeridhiana, tunacheza pamoja, tunatembea pamoja na tunakula pamoja kwa hali hii hatima yake ina muelekeo mzuri.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, katika Baraza lijalo asaa kheri Mwenyezi Mungu anaweza akatujaalia tukaweza kurudi tena wengine katika Baraza hili. Kwa hivyo, tunaomba utaratibu mmoja uje utumike. Mhe. Spika, sisi wawakilishi wako tuna masikitiko makubwa sana. Mmetupa *passport* jamani, *passport* zile zimekwisha muda wake miaka mitano, zikaendelea kwisha tena muda wake miaka mitano na zikaendelea tena kwisha miaka mitano, hazina hata muhuri wa kwenda hapo Kariakoo Dar es Salaam.

Hili ni tatizo sugu Mhe. Spika, haiwezekani mtu anakaa miaka 15 ndani ya Baraza hili hajenda popote, ndio maana hata wengine tulikuwa tunaomba tuumwe angalau tusafirishwe. Maana yake mtu unajiombea uumwe ili upate kusafirishwa. Mhe. Spika, suala hili najua ni kutokana na ufinyu wa bajeti, pesa zilikuwa kidogo. Lakini zingatieni katika kipindi kijacho kuwaona na wawakilishi wanapata fursa kama hizo. Dk. Mwinyihaji wawe wanakwenda safari zinazowalazimu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 95, asilimia 5 nakupunguzia Mhe. Waziri Kiongozi mpaka pale utakaponipa

maelezo sahihi ya kero hizo nilizozizungumza. Nakushukuru Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu. Mhe. Omar Ali Jadi yeye juzi alitaka kunirejeshea *passport* hiyo, alisema kwamba hana haja nayo kwa hivyo bora niichukuwe niifadhi iwe kama kumbukumbu kwamba aliwahi kupewa na yeye. Tutajitahidi. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Ali Haji Ali.

Mhe. Ali Haji Ali: Mhe. Spika, kama nilivyoona utamaduni wa kikao chako cha mara hii cha bajeti na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama, kwa hivyo kila aliyesimama alimtaja Mwenyezi Mungu kwa nguvu zake zote.

Kwa hivyo, na mimi naona nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi na afya njema ya kuweza kupata nafasi ya kushiriki katika mjadala huu wa Afisi ya Waziri Kiongozi katika bajeti yake ya mwaka wa fedha wa 2010/11.

Pia Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi na kukupongeza kwa umahiri wako wa kuendesha Baraza letu hili kwa busara na hekima kubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu kila uchao na wewe akuzidishie na ikiwezekana pengine na wewe uwemo katika hao watarajiwa.

Tatu, Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Waziri wake na wataalamu na Katibu Mkuu kwa kazi njema wanayoifanya na yeye pia namuombea kila la kheri na Mwenyezi Mungu ampe kila lililo na kheri alilolitaka.

Mhe. Spika, Zanzibar imepiga hatua kubwa za maendeleo katika nyanja mbali mbali, ambayo haya ndio matokeo ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na Baba wa Taifa hili Mzee wetu Abeid Aman Karume, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amuweke yeye na wenziwe huko waliko mahala pema peponi, amin.

Mhe. Spika, mimi katika kuanza mchango wangu nataka nianze na suala la MKUZA. Mhe. Spika, kama unavyojua MKUZA una *class* zake tatu. Uchumi na upunguzaji umaskini, huduma na ustawi, utawala bora na umoja wa kitaifa. Sasa hapa ndipo ninapotaka kuanzia Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika kuanza kwangu naanza na swali. Mhe. Spika, katika mazingira haya tuliyokuwa nayo hivi sasa, hili suala la Rais wa Zanzibar kuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linazungumzika au halizungumziki? *(Makofi).*

Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo Wazanzibari limekuwa linatupa mfarakano, linatupa kwamba sifa ya Muungano wenyewe vile vile unaonekana kama sio sahihi ni suala la Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamo wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, swali langu. Je, basi sio wakati muafaka kwa Wanzanzibari kuliongea jambo hili na likapata majibu yake kama yalivyopata majibu mengine? Hilo la kwanza Mhe. Spika.

La pili, nchi yetu kama zilivyo nchi nyengine, vijana wetu ambao tunawafundisha kwenye shule zetu za sekondari mpaka vyuo vikuu, wengi wao wanakosa kazi na wakikosa kazi wanaamua kwenda nchi za nje kule wanapata kazi na hatimae wengine wanaomba uraia na wanakuwa raia wa nchi zile, lakini uwezo wao wa kifedha waliokuwa nao ni mkubwa lakini hawawezi kurudi hapa nyumbani kwa sababu kwanza wameshakuwa na sura ya kwamba wao wageni. Je, hivi kwa nchi yetu haijafika wakati hivi sasa kuwa na *dual citizen ship* ili kuhakikisha kwamba uwezo wa vijana wetu kwa nguvu zao wamekwenda na wamefanya kazi wamepata pesa ili waje wazi-*invest* hapa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kuna jambo moja labda nitakosana na wenzangu lakini basi pengine ndio mawazo yangu kuna lugha ambayo kwa nafsi yangu siipendi, hawa tunaowaita washiriki wa maendeleo mimi naona ni wanyonyaji tu lazima niwe mkweli hata hawa wanyonyaji nao wanahama kwao kwa sababu ya *technology* waliyokuwa nayo na vifaa walivyokuwa navyo wanakuja hapa wanatuibia wanakwenda kwao ku-*invest*. Lakini watoto wetu sisi wanakwenda kwao kufanya kazi kutoka jasho wanapata pesa, mimi nitashangaa kama mtafikiria kwamba kurudi kwao wao ni dhambi, kuwa na uraia wa nchi mbili ni dhambi hivi hawa wenzetu wa Marekani wanajua, Waingereza wanalo hilo, Australia walo hilo, Canada wanalo hilo na msingi wake mkubwa wengine ni kwenda kuwaibia wengine na wakarudi kwao na kutengeneza nchi zao hawana chengine. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nadhani ni wakati mzuri kutafakari jambo hili hivi sasa, maana hawa tunaowaita washirika wa maendeleo wanakuja katika nchi zetu na makampuni, wanakuja wakishatuibia wanakwenda kwao wanazipa zile serikali zao pesa tano wanarejesha huku lakini wanatuibia mia hilo la pili.

Jengine Mhe. Spika, tukubaliane basi kwamba nchi yetu imepiga hatua za maendeleo kisiasa na kiuchumi, sasa kama hivyo ndivyo tunavyo vyama vya siasa katika nchi yetu lakini kunako vyama vya siasa hivi liko tatizo la demokrasia ya kweli kwa mfano. Unaweza kukuta chama cha siasa kinawawakilishi kwenye vikao hivi vya kutunga sheria lakini wamejazana mjomba shangazi na mtoto wote ukimuuliza wewe nani mimi fulani, baba yangu fulani, na mama yangu fulani sasa wapo shangazi na mjomba wote lakini

ni chama cha kisiasa, sasa walio kwenye chama kile kwa sababu wanataka siasa wanaogopa kusema kwa sababu wakisema watafukuzwa na wakishafukuzwa hawana kazi ya kufanya.

Lakini basi kwanza kwenye vyama kusiwe na kubanwa mtu awe na uhuru wa kujieleza na kuwe na kinga ya kujieleza, mimi nadhani wakati umefika hivi sasa awepo *Independent Candidate* kwamba unasema kwenye chama unavyotaka na kama unajiamini unachosema ni halali unajua nikitoka mimi nitaungwa mkono, lakini leo hata kama watu wanazungumza mambo ya ajabu kwenye chama kwa kuwa siasa unaipenda itabidi uvumilie. Mhe. Spika, Mhe. Mhunzi asifikirie namsema yeye aa simsemi yeye hata kidogo lakini uwe unafika pahala unatoa mawazo yako, lakini ukishaudhi wakubwa wako na siasa unaitaka hakuna katika nchi yenu nafasi ya *Independent Candidate* uwe unakaa vipi na hamu yako kuwa mwanasiasa.

Mimi nadhani sasa hivi Mhe. Spika, tufike mahala basi tukubaliane kwamba katika nchi yetu suala la *Independent Candidate* tulikubali, hakuna namna nyengine tutaimarisha vyama vyetu na demokrasia ndani ya vyama hivyo itakuwepo si hivyo kutakuwa na wababe kwenye vyama na wataona vyama vyao wao na baba zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nizungumzie mambo mawili kwa wakati mmoja rasilimali watu rasilimali fedha, serikali inayoongozwa na Dk. Karume na serikali nyengine duniani huwa zinachukua *contract* kwa wananchi kwamba sisi tunataka tushibe, utulivu, amani, elimu, afya na mambo mengine wanasema hiyo *contract* tunaitaka, sasa kama mnaitaka basi tunakuruhusuni mtutoze ada, tunakuruhusuni mtafute wawekezaji wa nje waje, kodi tutoe. Mradi mambo yetu sisi tunayokupeni ni hayo na njia za kuweza mkatutumikia ni hizo basi wanasema sawa.

Sasa kunako rasilimali fedha katika nchi yetu Mhe. Spika, nataka niseme tumefanya vizuri ingawaje bado uchumi wetu ni tegemezi lakini kwa kweli tunafanya vizuri sana, ukitaka kujua kama tunafanya vizuri nenda kasome hichi kitabu cha pili ambacho zote sekta tatu humu zinazungumzwa, ukizisoma hizo hakuna hata jambo moja kunako sekta moja ambayo tunazungumza sisi kwa sababu ukizungumza elimu bora humo mmeshazungumzwa na mkakati wenyewe, uchumi imara wameshasema humo, sekta imara wameshasema humo. Kwa hivyo utakuta haya maneno mengi tunayozungumza humu yanakuwa yameshasemwa kwa hivyo la kujiuliza mbona bado tuko hapo hapo hilo ndio jambo ambalo utalikuta. Kwa maana nyengine kwamba uwezo wetu wa kuandika mambo ni mkubwa zaidi kuliko utendaji, sasa hilo la rasilimali fedha utakuta kama nilivyosema.

Lakini sasa twende kunako rasilimali watu Mhe. Spika, kila kwenye taasisi utakayaopita utakuta kuna upungufu wa wafanyakazi na wataalam, lakini kisingizio cha kwanza ni kwamba hakuna sera lakini pili hakuna hata hiyo *program ya training* na ajira inafahamika kuna zile ajira za kubabaisha tu. Lakini serikali haina *Program* ya kujua kwamba katika suala zima la rasilimali watu *Program* yangu mimi hii ndio ninayotakiwa kuwa nayo ili niweze kuwa na ile *Contract* niliyokubali. Sasa mimi ombi langu serikali iharakishe kuleta hiyo sera ya utumishi na iwe na *Program* ya uhakika juu ya rasilimali watu vyenginevyo kutakuwa hakuna maendeleo yoyote.

Mhe. Spika, jengine dogo ambalo ni madaraka mikoani hili limekuwa kama hadithi mimi mwenyewe nilibahatika kura Waziri siku moja wa Tazala za Mikoa hiyo hiyo jambo hilo tumeanza nalo tokea wakati wangu kwa hivyo ni mwaka wa kumi na tano sasa hivi, lakini hakuna *achievement* yoyote na hii maana yake ni kusema kwamba pale tunapowapa nafasi wananchi kushiriki katika maendeleo ya taifa lao hapa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iombe radi maana ndio haitaki.

Bila ya kuwa na serikali za mitaa madaraka mikoani sasa yalioko ni yale ya *Argent* kwa maana ya *General Order* nashukuru inafanya vizuri, pili ni lile ya *Consultation* ambayo ni baraza kati ya serikali na serikali kamba unamuweka Mkuu wa Wilaya, unamuwaka Mkuu wa Mkoa ndio wewe mwenyewe serikali kwa serikali lakini ile madaraka mikoani *by devolution* haipo. Sasa ikiwa hiyo haipo maana yake Serikali kuu mmeamua kubaki peke yenu na kwa maana hiyo mnaweza kubabe kila kitu jambo ambalo si kweli, matokezeo yake ndio hayo mnapunguza uwezo wa kuwashirikisha jamii katika maendeleo ya kuuchumi kwa hivyo mnakuwa na mambo mengine mengi.

Pili mnashindwa hata kusema tusipandishe kodi sasa mtapandisha kodi vipi huku wakati jamii kubwa mmeweka, pili hamjaiandaa vizuri kiuchumi kuweza kukidhi kweli lazima hapa matatizo yawepo. Kwa hivyo kunako hili mimi nilikuwa naomba kwamba serikali ijitahidi hii sera iharakishwe, lakini la kushangaza wakati mwengine mimi huwa najiuliza hivi jamani hizi sera za utumishie serikalini mpaka tukaombe pesa au sisi wenyewe tuna wataalam lakini tunashindwa kujua tunataka kufanya kazi gani na wafanyakazi wa aina gani. Mimi hilo napenda nielimishwe mbona linanipa matatizo kidogo mimi kulifahamu.

Mhe. Spika, jengine dogo suala la utafiti. Mhe. Spika, utafiti ni moja katika kichecheo kikubwa sana cha kutekeleza mambo kwa uhakika lakini mimi nimesoma panapo hutuba ya bajeti si hii wala nyengine, lakini hiyo *element* ya utafiti haiwekwi kabisa na nchi zote duniani zilizoendelea na kupata mafanikio makubwa basi pamoja na mambo mengine lakini siri nyengine ni kufanya

utafiti mwingi wa kina, lakini inaonekana sisi tunafanya mambo yetu bila ya utafiti hilo ni kosa.

Kwa sababu hata ukienda kwa mganga wa kienyeji, ukifika anatoa ubao wake na tumbaku anapiga anakwambia huyu ni *shamsirohara* kuna mambo makubwa hapa, anakwambia kama hukuja leo wewe hatari, anatoa ubao wake kutizama mambo yako je? Sasa nyie mnajifanyia tu hii ni hatari kubwa.

Ninachoomba Mhe. Spika, kwamba kiji-*element* hichi kikue tuwe na ubao tusijaribu tu kufanya mambo bila ya kuwa na uhakika nayo ni hatari, najitahidi Mhe. Spika, naacha mambo mengi kidogo.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye Baraza letu kwanza nikushukuru wewe mwenyewe binafsi umetusaidia sana mimi ambaye nimeshawahi kukaa kwa miaka kumi na tano umelibadilisha mno kiasi ambacho uelewa wetu na uwezo wetu wa kufanya kazi ni mkubwa sana, hata wasaidizi wako nao vile vile wametusaidia sana.

Mhe. Spika, lakini tuliwahi kupata nafasi mimi na Mhe. Haji Omar na Mhe. Ame Mati tulikwenda kule Boswana kule tulijifunza kidogo kwamba ile Afisi yao inakwua na kila aina ya wataalam, kwa mfano mimi naleta hoja ya kilimo kwa hivyo mtaalam wa Kilimo yupo namwendea bwana wewe mimi nataka kuleta hoja ya kilimo basi yeye ndio ananitafutia siji kubabaisha tu kama tulivyozoea humu, kwamba unakuja kujitetea mwa mwa aa haifanywi hivyo inakuwa na utaratibu kidogo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ningeomba kwamba baraza liendelee kuimarishwa nakushukuru baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/6/2010
Saa 3.00 asubuhi)